

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini – Tarehe 3 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano na leo ni Kikao cha Ishirini. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Maswali.

SPIKA: Katibu njoo kwanza kabla hatujaanza maswali.

Katibu tena.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo tayari mnafahamu, ndugu yetu Dkt. Reginald Abraham Mengi alifariki huko Dubai usiku wa kuamkia jana tarehe 2 Mei, 2019. Dkt. Mengi alikuwa ni Mtanzania ambaye kwa bidii, juhudhi na maarifa aliweza kukua kiuchumi kutoka maisha duni ya kijiji hadi kufikia kuwa mmoja wa wafanyabiashara wakubwa hapa kwetu Tanzania, Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla.

Katika kuomboleza kifo na msiba huu mkubwa, sisi Bunge tunaungana na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, familia ya Marehemu na Watanzania wote tukimshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa wote na tukimshukuru Mheshimiwa Mengi kwa mchango wake mkubwa usiopimika kwetu Watanzania. Tutamkumbuka daima kwa jinsi ambavyo alisaidia sana hifadhi ya mazingira hasa maeneo yanayozunguka mlima Kilimanjaro kwa kupanda miti mingi sana kwa mamilioni bila kuchoka.

Alikuwa ni mmiliki wa vyombo mbalimbali vyahabari zikiwemo televisheni, redio na magazeti kadhaa, alikuwa mmiliki wa viwanda kadhaa hasa kwenye sekta ya *manufacturing*.

Pia, Dkt. Mengi alikuwa ni kiongozi wa Umma akiwa ni Mwenyekiti wa Bodi mbalimbali ikiwemo *IPP Limited* na mengine mengi ya binafsi na ya Umma kama kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mazingira, Mwenyekiti wa *NBAA*, Kamishna wa *TACAIDS*, Mwenyekiti wa *CT/na nyadhifa* nyingine nyingi.

Pia Dkt. Mengi katika maisha yake alipata tuzo nyingi za Kitaifa na Kimataifa.

Dkt. Mengi alijulikana kwa utoaji wake mkubwa wa misaada ya kijamii (*philanthropist*), alitoa sana katika ujenzi wa misikiti, ujenzi wa makanisa; alitoa sana kwa masikini na wasiojiweza, wanyonge na walemovu. Alisaidia sana katika maeneo ya tiba ya wagonjwa mbalimbali wakiwemo wagonjwa wa moyo.

Ni hivi majuzu tu ambapo Dkt. Mengi alichangia shilingi milioni 50 kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutuunga mkono kwenye mradi uliobuniwa na Wabunge Wanawake (*TWPG*) wa kujenga vyoo vyahabari kwa mtoto wa kike katika majimbo yote Tanzania.

Bwana alitoa, Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe, Amina.

Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

Na. 158

Barabara Inayounganisha Umba na Mtae

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Mafuriko yaliyotokea Mlalo mwaka 1993 yalisababisha uharibifu mkubwa kwa barabara inayounganisha Tarafa za Umba na Mtae:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kukarabati barabara hiyo muhimu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Tarafa za Umba na Mtae yenye urefu wa kilometra 12.7 inajulikana kama barabara ya Mtae – Mtii – Mnazi. TARURA Wilaya ya Lushoto imekamilisha usanifu na tathmini ya kuifanyia matengenezo makubwa, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kinahitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kugharamia matengenezo hayo kwa kuwa inatambua umuhimu wa barabara hii.

SPIKA: Mheshimiwa Shangazi, nimekuona.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu hayo, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa barabara hii ya Mtii – Mtae – Mnazi, kilometra 12.7 pamoja na Kwekanda – Hekcho – Rugulu hadi Mkomazi kilometra 17.5, zote hizi tumeziweka katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 na bajeti tayari tumeshapitisha. Je, Serikali inatoa tamko kwa wananchi wa Mlalo?

(b) Kwa kuwa, barabara hizi siyo tu kwamba zinaunganisha Tarafa za Umba – Mlalo na Mtae, lakini pia zinaunganisha wilaya jirani za Korogwe na Same: Je, Serikali haioni kwamba kwa kutofanya wepesi wa kurekebisha barabara hizi inakuwa ni kikwazo kwa fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Mlalo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kipekee kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Shangazi, amekuwa akipigia kelele sana kuhusu barabara hii ya kwenda Mtae na mara nyingi sana amefika ofisini kwetu. Naomba nimpongeze katika hilo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake anaulizia kwamba tayari bajeti imeshapitishwa, nini tamko la Serikali kuhusiana na ujenzi wa barabara hiyo? Bajeti ambayo imepitishwa kwa ajili ya Wilaya ya Lushoto ni jumla ya shilingi bilioni 1.8. Kama katika bajeti yao na barabara hii ipo, ni vizuri wakahakikisha kwamba barabara hii ni muhimu ikaanza kutengenezwa mapema.

Mheshimiwa Spika, kwa vile bajeti inahusu shilingi bilioni 2.5 ambayo siyo rahisi, Bajeti ambayo imepitishwa ni 1.4 na wao wanahitaji shilingi bilioni 2.5; na kilometra katika

Wilaya ya Lushoto ni jumla ya 935. Naomba Meneja wa *TARURA* ahakikishe katika vipaumbele vya barabara za kutengenezwa iwe pamoja na barabara hii.

Mheshimiwa Spika, katika swalı lake la pili, anaulizia je, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza barabara ya kuunganisha kwenda Lushoto na wilaya nyingine kwa maana ya fursa ya kiuchumi? Ni ukweli usiopingika kwamba maeneo ambayo barabara haipitiki tunakuwa tunawanyima wananchi fursa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika pia kwamba bajeti yetu haiwezi ikakidhi kwa mara moja maeneo yote. Naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira na yeze mwenyewe ni shuhuda, tangu tumeanzisha chombo cha *TARURA* kazi inayofanyika ni nzuri na hakika na barabara hii itawekwa kipaumbele ili iweze kutengenezwa. (*Makof!*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Barabara, Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalı dogo la nyongeza. Barabara ya Ikola – Kasangantongwe imeharibika sana na mvua zilizonyesha na kusababisha wananchi kushindwa kutumia barabara hiyo na kuanza kutumia njia ya majini ambayo siyo salama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha kuijenga barabara hiyo ya Kasangantongwe?

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Josephat S. Kandege, Mbunge wa Kalambo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) Mheshimiwa Spika, nimepata fursa ya kutembelea Jimbo la Mheshimiwa Kakoso na katika maeneo ambayo barabara zinajengwa unaona thamani ya pesa ni pamoja na Jimboni kwake. Yeye mwenyewe anakiri kwamba barabara hii ambayo anaitaja

imeharibika kutokana na mvua ambazo zinanyesha na ni ukweli usiopingika kwamba katika maeneo ambayo mvua ni za uhakika ni pamoja na Jimboni kwaake.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumwagiza Meneja wa *TARURA* ili akaangalie uharibifu wa hiyo barabara namna aone namna ambavyo anaweza angalau akafanya maboresho katika maeneo korofit sana ili barabara hii iweze kuendelea kupitika na wananchi waendelee kufaidi matunda ya CCM.

SPIKA: Tunahamia swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 159

Barabara ya Segerea – Sheli – Kipawa

MHE. ANATROPIA L. THEONEST aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Segerea – Sheli kwenda Kipawa kupitia Seminari itaanza kutengenezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais *TAMISEMI* naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Segerea – Sheli – Kipawa kupitia seminari yenyewe urefu wa kilometra 2.93 inasimamiwa na *TARURA* Manispaa ya Ilala, imesajiliwa kwa jina la Majumba Sita, Sitakishari. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, barabara hiyo imechongwa kwa *grader* ili kuiwezesha kupitika. Hata hivyo, barabara hii inakatisha katika mto Msimbazi ambapo hakuna daraja. Daraja linalohitajika kujengwa ni kubwa na usanifu wake ulishafanyika.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo inatokana na mto kutanuka, hivyo inahitajika kufanyiwa *study* ya kina na mapitio ya usanifu wa awali ili kupata mahitaji halisi ya ujenzi wa daraja kutokana na changamoto hiyo. Mara baada ya kukamilika kwa mapitio ya usanifu na tathmini ya gharama Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kujenga daraja na kuifanya matengenezo makubwa barabara hii. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali kuitia *TARURA* imeitengea barabara hii jumla ya shilingi milioni 43 kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofii.

SPIKA: Mheshimiwa Anatropia swali la nyongeza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ni zaidi ya miaka 15 wananchi wa Segerea kuitia hiyo barabara ya Majumba Sita, Sitakishari wamekuwa wanapitia hiyo adha ya kukosa daraja, lakini ni kiungo kikubwa cha Gereza la Segerea, Seminari na sekondari mbalimbali: Je, Serikali haionti ni wakati sahihi wa kutengeneza hilo daraja ili kuondokana na hiyo adha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Changamoto ya madaraja katika kata mbalimbali za Jimbo la Segerea ni kubwa, nikianzia na Kata ya Tabata, Segerea, Kimanga na nyingine: Je, nini kauli ya Serikali kuondoa hii adha ukizingatia kwamba hili eneo letu halina barabara nyingi za lami na halina mitaro ili kuondoa adha inayowakabili wananchi wetu? Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Anatropia, unauliza swali hilo kama Mbunge wa Jimbo! Yuko mwenyewe bwana! (*Kicheko*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikuwa namkumbusha tu Mheshimiwa Anatropia. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zangu naamini ziko sahihi kwamba ni mara ya tatu Mheshimiwa Anatropia anaulizia barabara hii. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo

amekuwa akifuatilia kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika swalilangu la msingi, changamoto ambayo tunakutana nayo kuhusiana na daraja hilo ni namna ambavyo mto unapanuka. Pia naomba yeche pamoja na Wabunge wote wanaotoka Dar es Salaam niwape maneno ya faraja kwamba ndani ya mwezi huu tumeweza kusaini kandarasi ya jumla ya shilingi bilioni 260 ambayo pia inashughulikia na adha ambayo inatokana na mafuriko mvua zinaponyesha na maeneo mengi ya Dar es Salaam yatakuwa yanafaidika katika hilo. Naamini hata hili suala la mto kupanuka baada ya kwamba kingo zimejengwa, adha itapungua.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuiamini Serikali maana yeche mwenyewe anashuhudia jitihada zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, katika swalilake la pili, ameongelea madaraja mengi. Naamini katika *package* ya shilingi bilioni 260 nayo itakuwa imekuwa *covered*. Kama haitoshi, tumeweza kuweka taa 5,000 ndani ya Mji wa Dar es Salaam kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaendelea kufaidi matunda ya chama chao. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Mifugo na Uvubi, swalilinaulizwa na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani.

Na. 160

Kuwasaidia Wavuvi Wadogo Kujikwamua na Umasikini

MHE. HAMAD SALIM MAALIM aliuliza:-

Uvubi ni moja ya vipaumbele vinyavyosaidia kusukuma maendeleo ya wananchi wengi wa Tanzania na Taifa letu ni mionganoni mwa Mataifa maskini duniani:-

Je, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga namna gani katika kuwasaidia wavuvi wadogo ili kukuza maendeleo ya Taifa pamoja na kujikwamua na umasikini uliokithiri?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Salim Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani anawakilisha Wakojani ambao ni wavuvi maarufu wa Bahari ya Hindi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ina mikakati mbalimbali inayolenga kuleta maendeleo katika Sekta ya Uvuvi na kuwasaidia wavuvi ambayo ni pamoja na:-

(i) Kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 ili kuendana na Sera ya Uvuvi ya mwaka 2015 na mabadiliko ya sasa ili kulinda, kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

(ii) Kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu kwa kufufua Shirika la Uvuvi la *TAFICO*, kujenga bandari ya uvuvi na kununua meli mbili kubwa za uvuvi ili kuchochea ukuaji wa viwanda vya kuchakata samaki, kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, ajira na kuongeza mapato ya Serikali;

(iii) Kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu uvuvi endelevu, ukuzaji viumbe katika maji na ufugaji samaki kwenye vizimba kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki ndani ya nchi; na

(iv) Kufanya tafiti mbalimbali zitakazosaidia kuendeleza Sekta ya Uvuvi Nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha Dawati la Sekta Binafsi ili kuwasaidia wavuvi kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo kupata mikopo kutoka Taasisi za Fedha. Pia Serikali inaendelea kuwashimiza wavuvi kuijunga katika vikundi na kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Msingi, Vyama vya Akiba na Mikopo na VICOBA ili waweze kukopesheka na kuweza kununua zana na vyombo bora vya uvuvi.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kojani, swali la nyongeza.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekubali kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kujikwamua na umasikini na kuleta maendeleo ya Taifa: Je, ni kwa nini basi Serikali hii hii imeamua kuwachomea wavuvi nyavyu zao ambazo nyingine hata hazistahiki kuchomwa kama ina lengo hilo? (*Makof*)

Swali la pili; kwa kuwa uvuvi si suala la Muungano, lakini uvuvi wa Bahari Kuu ni suala la Muungano, kwa nini basi wavuvi wetu wengi wanaotoka Unguja na Pemba wanaokwenda kuvua katika mpaka wa Tanzania na Kenya wanapokamatwa Serikali yetu inashindwa kuwatetea? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvu, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega. Wavuvi wa Kojani hata kule Mkuranga wapo pia. Karibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, zoezi la uchomaji nyavyu ni zoezi liilokwenda kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Katika kutekeleza zoezi hili la uchomaji nyavyu haramu, tumetekeleza kwa kufuata Sheria ya Uvuvu Na. 22 ya mwaka 2003 lakini na sheria zingine za nchi ikiwemo Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wavuvi wote nchini kwamba Serikali iko pamoja nao katika kuhakikisha inawasaidia. Ndiyo maana yapo mambo ambayo tuliyaona kuwa yanafaa kuboreshwa, mathalan katika hili la nyavu, wavuvi wa upande wa bahari ambapo Mheshimiwa Mbunge wa Kojani anatokea, wameleta maombi yao ya kuona kuwa nyavu za milimita 10 siyo nyavu ambazo zinaweza kukamata samaki. Hivyo wametuletea maoni ya kuhakikisha kuwa tunawapelekea nyavu za milimita nane. Sisi kama Serikali tumechukua rai yao na tumeifanyia kazi.

Maboresho ya kanuni hiyo yako tayari, hivi sasa wakati wowote kuanzia sasa matumizi ya nyavu za milimita nane yatatangazwa rasmi ili wavuvi kote nchini hasa wale wa upande wa bahari waweze kunufaika na rasilimali za nchi yetu. Hivyo basi, ningewaomba waendelee kufuata sheria tulizonazo kwa muktadha mzuri wa kulinda rasilimali za Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ameuliza kuhusiana na Serikali kutokuwasaidia wavuvi wanaokamatwa upande wa kule Mkinga, mpakani na Kenya. Nataka nikuhakikishie na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote na mionganini mwa Wabunge nimashahidi, akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa kutoka hukohuko Kojani, Mheshimiwa Kai, tumekuwa tukifanya jitihada nyingi sana, kila mara, wavuvi wetu wanapokamatwa na Serikali yetu kuititia Wizara ya Mambo ya Nje, imekuwa ikifanya mawasiliano na Serikali Kenya, wakati wote, kwa ajili ya kuhakikisha kuwa, wavuvi wale wanaruhusiwa na kupewa dhamana ya kurejea nyumbani kuendelea na shughuli zao. Wakati wote sisi tumekuwa tukiwaomba wavuvi wetu wajielekeze zaidi kuvua katika maeneo ya nchi yetu kwa sababu tunazo rasilimali zakutosha na hatuna sababu ya kwenda kuvua katika maeneo ya nchi nyingine. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Mama Salma Kitwete, nilikuona, swalii la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swalo dogo la nyongeza, Jimbo la Mchingga, Jimbo la Mtama, eneo la Sudi, Jimbo la Lindi Mjini, hupitiwa na Bahari ya Hindi na vijana hutegemea uvuvi ili kujiongezea uchumi wao na vitendea kazi kwa kweli ni duni sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vijana hawa boti ili waweze kuinua uchumi wao? Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Mifugo na Uvuvi, majibu tafadhali.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salma Kikwete ameiandikia Wizara kuiomba kusaidia vijana hawa, lakini na hapa Bungeni amesimama kuuliza swalii la nyongeza. Nilienda kwenye maeneo hayo kwa vijana hao ambao wanafanya shughuli zao vizuri sana za uvuvi. Ninachotaka kusema kwa ufupi tu, najua mahitaji ya boti ni makubwa, lakini kwa kuanzia tutampa boti moja kwa ajili ya vijana hao. (*Makof!*)

SPIKA: Kwa niaba ya wananchi hao, tunakushukurusana Waziri, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. (*Makof!*)

Nilikuona Mheshimiwa Tizeba, swalii la nyongeza.

MHE.DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwakunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza. Wavuvi katika Ziwa Victoria, moja ya mambo yanayowakwaza sana ni masoko ya uhakika ya mazao ya samaki. Sasa katika Jimbo la Buchosa tulikuwa na soko mojaambalo lilihudumia karibu wavuviwote wa Jimbo hilo na Wizara ililifunga kwa maelezo kwamba halikuwa linasimamiwa vizuri, lakini tuna uhakika, suala la usimamizi wa soko hilo ni jukumu la Serikali na kwa hiyo, ilipaswa yenye we ndiyo iweke usimamizi mzuri ili wananchi waweze kuuza mazao yao. Sasa swalii langu, ni lini tu Waziri atakwenda kufungua soko hili ili wananchi wasiendelee kuhangaika? Ahsantesana. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, majibu tafadhali.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nitakwemda mwezi huu, soko hilo totalifungua. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, wafungulie Wachosa nao wafanye biashara, tunakushukuru.

Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, uliza swali lako.

Na. 161

Tozo ya Kuingia Maeneo ya Hifadhi ya Bahari

MHE. MBARAKA K. DAU Aliuliza:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana mpaka sasa kwenye tozo (*entrance fee*) ya kuingia maeneo ya Hifadhi ya Bahari (*Marine Park*) katika Kisiwa cha Mafia?

SPIKA: Majibu ya Swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994, imekipa Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu mamlaka ya kukusanyafedha zitokanazo na shughuli za utalii kwenye maeneo yaliyohifadhiwa (Hifazi za Bahari na Maeneo Tengefu) kwa ajili ya uanzishaji, usimamizi na uendelezaji wa maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2001 mpaka kufika mwaka 2017/2018, Hifadhi ya Bahari ya Mafia imekusanya jumla ya fedha Sh.6,140,843,478 za Kitanzania, zilizotokana na tozo za viingilio kwa wageni walioingia kwenye hifadhi ya bahari ya Mafia kwa kipindi hicho.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Mbunge wa Mafia, ulitaka kujua kiasi gani, umesikia, swali la nyongeza.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja namajibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza,kwa kuwa hizi bilioni sita alizozisema zimekokotolewa kutoka kwenye *net revenue*, baada ya kuondoa gharama na kwa kuwa hifadhi ya bahari wanaweka gharama za mafuta, gharama za likizo, gharama za uendeshaji wa hifadhi, mpaka kupelekea gharama zinakuwa ni kubwa lakini *net revenue* inakuwa ni ndogo ambayo halmashauri ya Mafia inatakiwa ipate asilimia 30.

Sasa swali, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni sasa umefika wakati gharama za kukusanya mapato peke yake ndiyo zitolewe, waachane na gharama za uendeshaji wa hifadhi ya bahari kwa sababu gharama zinakuwa ni kubwa na kipato kinakuwa ni kidogo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwamoja ya vikwazo vya Wilaya ya Kisiwa cha Mafia kupata watalii wachache, kwa mwakatunapata pale watalii kama elfu sita, ukilinganisha na Kisiwa cha Zanzibar, moja ya vikwazo ni hii *entrance fees* ya dola 24 kwa kila mtalii. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni sasa umefika wakati wa kuangalia uwezekano wa kupunguza kiwango hiki cha *entrance fees* ili kuweza kuvutia watalii wengi kuja katika Kisiwa cha Mafia? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri waMifugo na Uvuuvi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya kaka yangu Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Daukama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza anataka na kutushauri Serikali kuona umuhimu wa kupunguza gharama za uendeshaji ili kusudi ile faida inayopatikana na shughuli nzima za uhifadhi na utalii ziweze kwenda moja kwa moja katika jamii ya Mafia pia. Naomba nimhakikishie kuwa wazo lake hili tunalibeba na Serikalitumelichukua. Kwa kuwa ni jambo la kimchakato, tutakwenda kulitazama na kuona ni namna gani tunavyoweza kuendana na mawazo hayo ya wananchi wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni juu yakuona umuhimu wa kupunguza *fee* ya kuingilia katika maeneo haya ya hifadhi, ili kusudi kupata watalii wengi zaidi. Ni lengo la Serikali la kuhakikisha kuwa watalii wanaongezeka katika maeneo yetu ya utalii na hivyo, kama moja ya kikwazo ni *entrance fee*, nataka nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili nalo ni wazo ambalo totalichukua, tutakwenda kulikokotoa na kuona umuhimu wake ili kuweza kufikia lengo letu la kuongeza idadi ya watalii nchini.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa kwa ajili ya muda tuendelee na Wizara ya Maji. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Gimbo Dotto Masaba, uliza swali lako Gimbi kwa niaba ya Ntuzu *line* wote.

Na. 162

Mradi wa Maji Ziwa Victoria

MHE. GIMBI D. MASABA aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga Mradi mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Victoria kuanzia Nyashimo, Ngasamo, Dutwa, Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa:-

Je, ni lini mradi huo utaanza na kukamilika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali itatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Nyashimo (Busega), Bariadi na Langangabilili, Maswa na Mwanhuzi. Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni na mradi huu utatekelezwa katika awamu mbili.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza itahusisha Miji ya Nyashimo (Busega), Bariadi na Lagangabilili pamoja na vijiji vipatavyo 170 vilivyo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu kila upande. Awamu hii itagharimu *Euro* milioni 105 ambapo kati ya hizo Serikali ya Ujerumani kuititia benki yake KfW itatoa *Euro* milioni 25na *Green Climate Fund(GCF)* *Euro* milioni 80. Ujenzi waawamu ya kwanza unatarajiwा kuanza mwezi Oktoba, 2019 na kukamilika mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya mradi itahusisha Miji ya Mwanhuzi, Maswa na vijiji vipatavyo 83. Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na *Green Climate Fund* ili kupata fedha kiasi cha *Euro* milioni 208 zitakazotumika kugharimia utekelezaji wa awamu hii. Ujenzi wa awamu ya pili utaanza baada ya kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha hizo. Kukamilika kwaawamu zote kutawanufaisha wananchi wapatao 834,204.

SPIKA: Mheshimiwa majibu yako sijui kama yamegusa Itilima, muuliza swali uliza.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja namajibu ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Mradi wa Ziwa Victoria,

ulikuwa na mabomba mawili makubwa, bomba la kwanza ni bomba la maji safi na salama nabomba la pili ni bomba la maji ambayo hayana dawa kwa matumizi ya mifugo na mengineyo. Sasa naomba kufahamu kama mkataba huu umezingatia ufanisi wa mradi huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tumekuwana miradi mingi ambayo tunayo katika bajeti ambayo sasa hivi inakamilika hususan Mradi wa Nyangokulwa, Mradi wa Nyakabindi, Mradi wa Sanungu na Mradi wa Mahina. Miradi hii bado haijatekelezeka na kwenye kitabu cha Waziri nimeona kama miradi 10 ambayo wametupa. Sasa nataka kufahamu, ni kwa nini Serikali inatupa miradi ambayo haitekelezeki?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wa Simiyu akiwemo Mtemi Chenge pamoja na Mheshimiwa Mbunge Mpina, kwamba leo ni siku muhimu sana kwa Wanasiyiu kwamba ule mradi ambao umeahidiwa na Serikali kwa muda mrefu sana ninavyozungumza Katibu Mkuu yuko Dar es Salaam anasaini *financial agreement* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa huu wa maji Simiyu. (*Makof!*)

Kwa hiyo, kikubwa hii ni Serikali ya awamu ya tano inapoahidi inatekeleza. Hata hivyo, kikubwa cha msingi kuhusu suala zima la utekelezaji wa mkataba, nataka nimakikishie, *design* au mkataba jinsi ulivyotuelekeza na sisi ndivyo tutakavyotekeliza mradi ule kama tulivyoelekezwa na mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kuhusu miradi ambayo tumeahidi kwa ajili ya utekelezaji, sisi kama Wizara ya Maji zipo changamoto, moja, kulikuwa na miradi ambayo ilikuwa inahitaji kulipwa *certificate*, tumeshapokea bilioni 44 zingine na moja ya watu ambao tumewalipa ni

wakiwemo Wanasi miyu, lakini kikubwa tumewatengea tena katika bajeti hii bilioni tano na milioni 950, yote katika kuhakikisha tunatatua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwagize Mhandisi wa Maji wa Mkoa wa Simiyu, ahakikishe fedha hizi zinatumika katika kuhakikisha wanakamilisha miradi ya maji na wananchi wa Simiyu waweze kupate maji safi, salama na yenye kuwatoshleza.

SPIKA: Kabla hujaondoka Naibu Waziri, kabla hujaondoka hapo, kidogo tu, rudi hapo. Kuna ufanuzi wa Itilima, itaguswa na Kisesa kwa Mheshimiwa Mpina. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, bila shaka.

SPIKA: Wanaguswa pia, *okay* nakushukurusana.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 163

Tozo *SDL* kwenda *VETA*

MHE. ALMAS A. MAIGE aliuliza:-

Waajiri wamekuwa wakilipa Tozo ya Maendeleo ya Ujuzi kwaWafanyakazi (*SDL*) ya asilimia 4.5 ya mshahara kwa kila mfanyakazi ambayo ililengwa kupelekwa *VETA* kwa lengo la kuendeleza ujuzi:-

(a) Je, ni asilimia ngapi ya tozo hiyo inapelekwa *VETA*?

(b) Je, nilini Serikali itarejesha *VETA* katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuleta uwiano wa mantiki kuwa *VETA* inaendeleza ujuzi wa wafanyakazi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
Alijibu:-

Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige,lenge sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tozo ya Kuendeleza Ujuzi, (*Skills Development Levy-SDL*)ni kodi inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato nchini chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato na Sheria iliyoanzisha *VETA*, Sheria Na.1 ya mwaka 1994 ilyorejewa mwaka 2006. Mwajiri anayeajiri wafanyakazi wanne au zaidi anapaswa kulipa tozo hii ambayo ni asilimia 4.5 ya malipo ghafi. Kiwango cha *SDL* inayopokelewa *VETAni* theluthi moja ya pato la *SDL* ambayo ni asilimia 33 ya tozo hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi (*VETA*)ilianzishwa ili kuwezesha nguvu kazi kubwa nchini kupata stadi stahiki za ajira kulingana na mabadiliko ya mfuko wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Majukumu makuu matano (5)ya *VETAni* kusimamia, kuratibu, kugharimia, kutangaza na kutoa mafunzo ya ufundis stadi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 *VETA* ilihamishiwa katika iliyokuwa Wizara ya Elimuna Mafunzo ya Ufundis Stadi, kwa sasa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kulingana na mahitaji ya wakati huo. *VETA* hufanya shughuli zake kwa kufuata sera na mipango ya Serikali ya muda mrefu na mfupi ili kuhakikisha wakati wote kunakuwa na nguvu kazi za kutosha na yenye ujuzi stahiki kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi.Kwa mantiki hiyo, suala la *VETA* kuwa Wizara gani, itategemea mahitaji ya Serikali kulingana na wakati husika.

SPIKA: Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa vile tozo hii ya asilimia 4.5 ya mshahara wa mfanyakazi ni kubwa kuliko tozo zote duniani. Siyo Afrika tu, dunianina hapa Afrika Mashariki tozo hii inatozwa asilimia 1.2 Kenya tu, tena kwa ajili ya sekta moja ya utalii. Swali la kwanza, je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza tozo hii ili kufanya utendaji wa biashara hapa nchini uwe rahisi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hapa Tanzania tunafanya biashara au kazi kwa utatu, yaani Serikali, Wafanyakazi na Waajiri, VETA kuwa chini ya Wizara ya Elimu, imetutoa katika mfumo huo. Je, Serikali haioni sasa ni muhimukurudisha VETA chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambako kuna Kazi, Ajira na Mafunzo.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, OleNasha tafadhalii!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Almas Maige kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba *SDL* tunayotoza sisi ni kubwa kuliko zote zinazotozwa duniani, siwezi kuwa na uhakika kuhusu hilo. Hata hivyo, *concern* au hoja ya kupunguza kodi hiyo au tozo hiyo tayari imeshawasilishwa Serikalini. Hata juzi wakati wa Maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi Chama cha Waajiri Tanzania waliileta kwa msisitizo mkubwa na Mheshimiwa Rais alitolea maelekezo kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayehusika na masuala ya Kazi na Ajira ajaribu kuwakutanisha utatu ule ambaa Mheshimiwa Maige ameusema, yaani Serikali, Wafanyakazi na Waajiri ili waweze kujadiliana wapate muafaka kuhusu namna bora ya kuratibu tozo hii.

Mheshimiwa Spika, watakapokutana, itabidi sasa jambo hilolipelekwe kwenye kikosi kazi kinachohusiana na mambo ya kodi, yaani ile *Tax Reform* ili waweze kujadili na

ikiwezekana mapendekezo yaweze kutolewa na ikibidi sheria ije Bungeni irekebishwe ili sasa tuwe na tozo ambayo imekubalika na pande zote.

Kuhusiana naswali lake la pili kwamba kwa nini VETA isihamishiwe Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye hasa inahusika na masuala ya ajira. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Serikali ni ileile. Kwa hiyo, kuhusu kwamba jambo fulani linatakiwa liwe wapi wakati fulani, ni masuala ya maamuzi tu ya muda na inategemea sana kwa wakati huo, kwamba umuhimu au mahitaji yanahitaji iwekwe wapi. Kwa vyovytote vile, masuala ya ufundi stadi ni suala la elimu vilevile. Kwa hiyo, siyo kwamba kuna shida ikiwepo kwenye Wizara ya Elimu, lakini kama tunavyosema, itaendelea kubadilika kulingana na maamuzi ya Serikali kwa wakati husika.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Warufiji wote.

Na.164

**Serikali Kuchukua Maeneo Yaliyoshindwa Kuendelezwa
katika Bonde la Mto Rufiji**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (K.n.y. MHE. MOHAMED O.
MCHENGERWA) Aliuliza:-**

Bonde la Mto Rufiji lina eneo kubwa lenye rutuba ambalo lingetumika vizuri lingeweza kulisha Mji wa Dar es Salam na viwanda vyote nchini, RUBADA imechukua maeneo hayo ambayo inakadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 500,000 na kuwapa baadhi ya wawekezaji ambao wengi wao ni matapeli na madalali wa viwanja/mashamba:-

Je, lini Serikali itamua kunyang'anya maeneo yote ambayo wawekezaji wameshindwa kuwekeza kwa kadri walivyoomba ili Sera ya Serikali ya Viwanda iweze kutimia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)

Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Jimbo la Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Uendeshaji wa Bonde la Mto Rufiji (RUBADA) ilianzishwa na Sheria ya Bunge Namba 5 ya mwaka 1975 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba.146 tarehe 1 Julai 1976. Mojawapo ya majukumu ya RUBADA ilikuwa kusimamia matumizi ya ardhi ya kilimo kwenye Bonde la Mto Rufiji ikiwemo kuratibu upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumbukumbu zilizopo, RUBADA haikuwahi kuchukua eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta 500,000 na kuwapa wawekezaji. RUBADA ilikuwa inamiliiki hekta 21 katika Kituo cha Ikwiriri, hekta 12.675 katika Kambi ya Vijana Mkongo, hekta 1.15 katika Kambi ya Utete, hekta 5,128 katika Shamba la Ngalimila Kilombero, Mkoani Morogoro, hekta 5,800 katika Shamba la Mngeta, Kilombero, Mkoani Morogoro na eneo la kilometa za mraba 13,907 kwa ajili ya majengo na viwanja Jijini Dar es Salaam. Aidha, ardhi yote nyingine kwenye eneo la Bonde la Mto Rufiji ilikuwa linamiliikiwa na Halmashauri 29 za Wilaya, Vijiji na wananchi mbalimbali.

Katika kipindi chote ilipokuwepo RUBADA imewezesha upatikanaji wa Hati Miliki usio wa moja kwa moja yaani (*Derivative Right of Occupancy*) wa eneo la hekta 2,000 katika eneo la Nyumbunda, Nyambili na Bungu, Wilaya ya Kibiti kwa mwekezaji *FJS African Starch Development* kwa ajili ya kilimo na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mihogo. Aidha, Serikali haitasita kuchukua ardhi hiyo ya kilimo iwapo itathibitika kuwa mwekezaji ameshindwa kuendeleza kwa shughuli za kilimo na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

SPIKA: Mheshimiwa Kakoso kwa niaba ya Mheshimiwa Mchengerwa, tafadhali uliza swali.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa RUBADA kwa muda mrefu imeshindwa kuyaendeleza haya mashamba, je, haioni sasa ni wakati muafaka Serikali iyachie maeneo haya kwa ajili ya matumizi ya wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili Bonde la Mto Karema kuna mradi wa umwagililaji ambapo Serikali imetoea fedha nydingi lakini mradi huo haujawahi kukamilika na una muda mrefu sana. Ni lini Serikali itakamilisha mradi wa *irrigation* uliopo pale Karema?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza amependekeza kwamba kwa sababu RUBADA imeshindwa kuendeleza mabonde haya basi yarudishwe mikononi mwa wakulima. Kwanza, nataka nimueleze Mheshimiwa Mbunge RUBADA haijawahi kumiliki ardhi kama jibu langu la msingi liliyoyokuwa, muda wote wa uhai wa RUBADA ardhi hii ilikuwa inamiliikiwa na Serikali za Vijiji na vijiji husika na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ni kwamba Bunge lako hili Tukufu mwaka 2017 lilipitisha sheria hapa tulishaifuta RUBADA sasa hivi haipo, mali zote za RUBADA zimerudi Serikalini na ziko chini ya Msajili wa Hazina. Sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kuona nani apewe ardhi hiyo kwa ajili ya kuiendeleza. Hilo wazo lake tunalichukua kwamba kama

itarudishwa tena kwa wananchi kwa sababu iko kwa wananchi basi itakuwa hivyo na wataendelea kuilima.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Bonde la Mto Karema, anataka kujua lini mradi huu utakamilika. Ni kweli kwamba miradi mingi ya umwagiliaji katika nchi hii ama ilitekelezwa chini ya kiwango au ilitekelezwa pasipo ufanisi uliokusudiwa. Kama Serikali baada ya kuliona hilo wataalam wanapitia kufanya tathmini ya kina tuone athari tulioipata ili kutumia tathmini ile tuweze kuyaendeleza mabonde haya. Kutegemea na upatikanaji wa fedha tutapanga jinsi ya kwenda kumalizia mradi huu.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Amina Makilagi.

Na.165

Vitendo vya Udhaililishaji wa Wanawake

MHE. AMINA N. MAKILAGI Aliuliza:-

Baadhi ya watu katika jamii bado wanaendeleza vitendo vya kuwanyanyasa, kuwadhalilisha na kuwadhulumu wanawake:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza kabisa vitendo hivyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ukatili wa kijinsia ni pamoja na vitendo vya kuwanyanyasa, kuwadhalilisha na kuwadhulumu wanawake na watoto. Aidha ukatili wa kingono na kisaikolojia ni sehemu ya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imechukua hatua mbalimbali za kuzuia na kutokomeza ukatili huo. Moja ya hatua hizo ni pamoja na kuandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 ambaao utsaisha mwaka 2021/2022. Mpango huo unalenga kupunguza kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii yetu kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000; Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia wa mwaka 2005; na Sera ya Maendeleo ya Moto ya mwaka 2008. Kutokana na utekelezaji wa mpango huu, hadi kufikia 2018, jumla za Kamati za Ulinzi za Wanawake na Watoto 10,988 zimeanzishwa katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa. Kamati hizi zina wajibu wa kuratibu utekelezaji wa mpango kazi katika ngazi husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanzisha Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Jeshi la Polisi 420 kwa kushughulikia mashauri ya ukatili wa kijinsia. Aidha, Serikali imeanzisha huduma za *One Stop Center* kwenye Mikoa saba ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Shinyanga, Pwani, Iringa Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria Namba 1 ya mwaka 2017. Sheria hii inatoa fursa kwa wanawake waliofanyiwa unyanyasaji au kudhulumiwa kupata haki zao kuititia vyombo vya usimamizi wa sheria pasipo kujali uwezo wao wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu kwa jamii. Mfano

katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara imetoa elimu ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake kwa Wahariri na Waandishi wa Habari ili waweze kuelimisha jamii kuhusu suala hili pamoja na kufichua matukio ya ukatili wa kijinsia. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imeratibu midahalo kuhusu ukatili wa kijinsia pamoja na kuwasilisha wasanii katika kampeni za kutokomeza ukatili huo.

SPIKA: Mheshimiwa Makilagi, nimekuona.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kuhakikisha inatokomeza ukatili wa watoto na wanawake, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na jithada hizo lakini ni ukweli usiopingika masuala ya ukatili wa wanawake na watoto bado ni ya kiwango kikubwa sana. Tumeshuhudia watoto wanafanyiwa ukatili na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alikuwa anazindua tuliona hata zile takwimu wanawake wajane wananyang'anya mali zao hasa viwanja na mali nyingine lakini watoto yatima na wanawake majumbani na hata kwenye familia zao bado wanafanyiwa ukatili...

MBUNGE FULANI: Kubakwa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Ndiyo, kubakwa na halikadhalika na hata kufanyiwa ulawiti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imefanya kazi nzuri ya kutunga sheria inayotoa fursa kwa watu wanaofanyiwa ukatili kwenda kupata haki yao bila kujali anacho au hana, kazi hii imekuwa ikifanywa na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Napenda kujua Serikali imejiandaaje kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza mpango huu ili kutuachia peke yake mashirika yasiyo ya Serikali ambayo na yenyege yanategea misahada kutoka nje? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda kujua ni mkakati gani sasa umewekwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto wa kuratibu na kuona hao wanawake na watoto wanaopata msaada wa kisheria ni matokeo gani yamepatikana na changamoto zilizopo na Serikali inajiendaaje na kukabiliana na changamoto hizo? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusiana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba suala hili sisi kama Serikali tunalichukulia kwa kipaumbele kikubwa sana na ndiyo maana tumeanzisha Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Spika, kupitia mkakati wetu huu imetusaidia sana maana matukio haya yanakuwa *reported* kwa kiasi kikubwa sana, kwetu sisi kama Serikali inatupa faraja kubwa sana. Kati ya Januari na Desemba, 2017 matukio 41,000 yaliripotiwa ndani ya nchi yetu na kati ya hayo 13,000 yalikuwa ni ukatili ya kijinsia dhidi ya watoto. Kwa hiyo, mwamko katika jamii umekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba Serikali imepitisha Sheria ya Usaидizi wa Kisheria, Namba 1 ya mwaka 2017 na kwa kiasi kikubwa sasa hivi usaидizi huu wa kisheria umekuwa unapitia katika taasisi zisizo za kiserikali, Serikali imeliona hilo na iko katika hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba tunaanzisha *Legal Aid Fund* ambapo sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili sasa ya usaидizi wa kisheria pale mashauri haya yatakapokuwa yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali imeendelea na hatua mbalimbali na iko katika hatua za mwisho za kuandaa Sera ya Ardhi, umilikiwa ardhi ulikuwa ni changamoto kubwa sana kwa wanawake. Sasa hivi Sera hii ya Ardhi inaenda kuweka utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba wanawake nao wanakuwa na sauti katika masuala ya umiliki wa ardhi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi kama Wizara tunaendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera hii ya Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto. Kwa kiasi kikubwa mwamko umezidi kuwa mkubwa lakini niendelee kutoa rai tu kwa jamii kueleza kwamba masuala mengi ya ukatili wa kijinsia yanafanywa na watu ambaeo wapo karibu na familia. Tuendelee kutoa taarifa na niombe sana masuala haya tusiyamalize ndani ya familia badala yeke tuhakikisha kwamba vyombo vya dola vinapewa fursa ya kuweza kuyashughulikia badala ya familia kuyamaliza ndani ya familia. (*Makofi*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Iringa, tafadhalii uliza swali lako.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubaliana kwamba kuna unyanyasaji mkubwa sana kwa wanawake na watoto lakini upo unyanyasaji mkubwa sana kwa kina baba, wapo ambaeo wamekuwa wakipigwa na wengine kunyanyasika. Kuna maandamano ambayo tuliona katika mitandao katika nchi ya jirani ya Kenya akina baba wakiandamana kudai haki zao za msingi kwa akina mama. Je, ni lini sasa sheria pia itajengwa kuwalinda akina baba ambaeo wamekuwa wakinyanyasika kila wakati? (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, inaelekea Wanyalu wananyanyasika huko. (*Kicheko*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge Viti Maalum, Mkoaa wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapoongelea ukatili wa kijinsia haimaanishi tunaongelea ukatili wa akina mama na watoto, jinsia ina *cut-across* na akina baba. Bahati mbaya sana matukio ya ukatili wa kijinsia ya akina baba siyo mengi yanakuwa *reported*. Nitumie fursa hii kuwaomba wale akina baba ambaa nao wanapigwa, wanafanyiwa ukatili wa kingono, wanaonyanyaswa kisaikolojia nao waweze kujitokeza ili madawati yetu ya jinsia yaweze kuyafanyia kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Yussuf nilikuona.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika ripoti ya hivi karibuni ya Kituo cha Haki za Binadamu na Sheria imeonesha kwamba kuna ongezeko kubwa la unyanyasaji wa wanaume unaofanywa na wanawake hasa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani Tanga na Visiwa vya Unguja na Pemba. Nilikuwa nataka kujua ni lini sasa Serikali itaanza kuzuia ongezeko hili ili kusimama na ile kauli ya Mwenyezi Mungu ya *Arrijalu qawwamuna ala-Nnisai*.

SPIKA: Hivi hawa wanaume wananyanyaswaje mbona Spika haelewi. (*Kicheko*)

Maswali mengine nashindwa hata kuyaruhusu, labda Mheshimiwa Naibu Waziri unaelewa tafadhali, nasikia wanaume wa Dar es Salaam wanaonewaje sana, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Wanaonewaje?

SPIKA: Anataka ufanuzi wanaonewaje, Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, katika ile ripoti walisema wanaume wananyanyaswa na wake zao, wanafanyishwa kazi ndani, wanapigwa, wananyimwa haki zao na wengine mpaka wanafikia kulazwa hospitali kwa vipigo wanavyovipata kutoka kwa wanawake.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, ni ripoti ambayo imetolewa na Kituo cha Haki za Binadamu na Sheria, si ripoti yangu. (*Makofi*)

SPIKA: Kumbe jambo kubwa hili, inasemekana hata Wanyamwezi wanapata shida hiyo hiyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, yanatakiwa majibu ya uhakika hapa.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yussuf, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba yapo baadhi ya matukio ya ukatili wa kijinsia wanaofanyiwa wanaume. Hata hivyo, kwa sasa hatuna takwimu za Mikoa ambayo ameitaja zinazoonesha matukio haya ni makubwa kiasi gani. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tutaendelea kufuatilia ili kubaini suala hilo.

Mheshimiwa Spika, pia amegusia ripoti ambayo sisi hatujaiona, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki cha Bunge basi aweze kutupatia taarifa hiyo ili na sisi tuweze kufuatilia. Niendelee kusisitiza tu kwamba matukio haya ya ukatili wa kijinsia ni makubwa zaidi dhidi ya wanawake na watoto kuliko wanaume.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, inatosha, tuwaombe tu Waheshimiwa Wanawake kuititia *TWPG* sasa muanzu kutetea wanaume, inaelekea tatizo hili kwenye jamii ni kubwa maana na ninyi mna watoto wa kiume jamani, kama

wanateswa basi tuangalie hii mambo, haipendezi kwenye jamii yetu. (*Kicheko*)

Sasa matangazo, kuna wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka *Tanganyika Law Society (TLS)* ambao wamefanya uchaguzi wao majuzi hapa kule Arusha, napenda kuwatambulisha Mwenyekiti mpya wa *TLS*, Dkt. Rugemeleza Nshala. (*Makofi*)

Pia wako Wajumbe ambao ni Ndugu Angelista Nashon; Ndugu Baraka Mbwilo; Ndugu Stephen Mwakibolwa; Ndugu Paul Kaunda; Ndugu Harold Sungusia; Ndugu Mariam Othman; na Ndugu Salima Mseta. (*Makofi*)

Naona Mheshimiwa Esther Matiko anawapigia sana makofi sjui kuna nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambaye ni mpiga kura wake kutoka Muhammwe, Mkoani Kigoma, Ndugu Vicky Mkeya. Karibu sana, umetoka mbali kwelikweli. (*Makofi*)

Wageni 19 wa Mheshimiwa Felister Bura kutoka Jukwaa la Uwekezaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Jane Chitojo. Ahsanteni sana wawekezaji wanawake. (*Makofi*)

Wageni 90 wa Mheshimiwa Seif Gulamali kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Paul Haji, UDOM. Karibuni sana UDOM, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Mpwapwa wakiongozwa na Ndugu Kasanda Japhet. Ahsanteni sana, karibuni sana Chuo cha Walimu Mpwapwa na Mbunge wenu Mheshimiwa Lubeleje yuko hapa. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Mkuranga

Mkoani Pwani wakiongozwa na Ndugu Mussa Mbonde. Karibuni sana wageni kutoka Mkuranga. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba ambaao ni Diwani kutoka Sengerema Mkoani Mwanza, Mheshimiwa Joshua Kubaniza na Ndugu Silvanus Angelo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa John Kaudutu ambaye ni rafiki yake kutoka Kahama, Ndugu Ramadhani Makonda. Karibu sana Makonda. (*Makofi*)

Wageni 189 wa Mheshimiwa Marian Mzuzuri ambaao ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Zuhura Kubeta. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Gidarya ambaao ni viongozi na waamuzi wa CHANETA-Tanzania kutoka Mikoa yote wakiongozwa na Katibu Mkuu Taifa, Ndugu Judith Ilunda. Karibuni sana CHANETA, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge sijui kama mnafahamu kwamba Mheshimiwa Anna Gidarya sijui yuko wapi leo, hebu simama Bwana. Huyu ndiyo Makamu wa Mwenyekiti wa CHANETA-Taifa. Tunakushukuru sana kuendeleza michezo na kwa hiyo tunaona wanamichezo wamependeza kweli kweli, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Salum Khamis Salum ambaao ni wapiga kura wake kutoka Simiyu wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya ya Meatu, Ndugu Charles Mazuri. Karibuni sana kutoka kule Mwanduzi. (*Makofi*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambaao ni wahamaishaji wa utalii wa ndani, utalii 255 group Dar es salaam na Zanzibar wakiongozwa na Ndugu Siza Mazongela. Karibuni sana utalii group. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Rashid Ntimizi ambaye ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam

wakiongozwa na Ndugu Abdul Anania. Karibuni sana.
(Makofi)

Wageni watano wa Sonia Magogo ambao ni Ndugu zake wakiongozwa na Katibu wa CUF Wilaya ya Muheza, Ndugu Juma Nindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 40 na walimu watatu kutoka shule ya sekondari ya Shemsie iliyopo Jijini Dar es Salaam ambao wamelitembelea Bunge kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi. Wale wa Shemsie? Karibuni sana sana watoto wetu. *(Makofi)*

Wageni watatu kutoka Jijini Dodoma ambao wametembelea Bunge kujifunza. Wale wageni watatu kutoka Dodoma karibuni sana pia. *(Makofi)*

Tumemaliza matangazo. Katibu

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

SPIKA: Haya tutangulie na hoja ya kutengua Kanuni halafu tutasikiliza mwongozo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba nitoe maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2)(4), Bunge linakutana hadi Saa 7:00 mchana na kusitishwa mpaka Saa 11:00 Jioni na baada ya hapo Bunge huendelea kukaa mpaka Saa 1:45 Usiku ambapo Spika husitisha shughuli na kulahirisha hadi siku nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni ndani ya kipindi cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge unaonDELETE, waumini wa dini ya Kiislam wataanza mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Ambapo katika kipindi hicho waumini wote wa kiislam watakaofunga hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo Saa 12:30 Jioni.

Na kwa kuwa, katika Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika leo tarehe 03 Mei, 2019 Wajumbe waliohuduhuria walikubaliana na umuhimu wa kutengua Kanuni husika kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge amba ni waumini wa dini ya Kiislam waweze kuswali, kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ninaliomba Bunge liazimie kwamba Kanuni ya 28(2) na 28(4) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi Saa 7.00 Mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi Saa 11.00 Jioni itenguliwe na badala yake Bunge linapositishwa Saa 7.00 Mchana liendelee na shughuli ifikapo Saa 10.00 Jioni badala ya Saa 11.00 Jioni.

Mheshimiwa Spika, na Kanuni ya pili, Kanuni ya 28(4) ambayo inaelekeza kwamba, Bunge litaendelea kukaa hadi Saa 1.45 Usiku ambapo Mheshimiwa Spika atasitisha shughuli na kulahirisha hadi kesho yake itenguliwe na badala yake Bunge liahirishwe ifikapo Saa 12.00 Jioni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utaanza kutumika mara tu mfungo Mtukufu wa Ramadhani utakapoanza na baada ya mfungo huo kukamilika, Bunge litarejea katika utaratibu wake wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono na Bunge zima lakini kama ilivyo ada inabidi niwahoji ili kuweka recordsawa sawa na Kanuni zetu zikae sawa sawa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Kwa hiyo, mara tu mfungo utakapoanza wiki ijayo tutakuwa tunaanza session yetu ya jioni Saa 10:00 Jioni na kumaliza kwenye Saa 12.30 hivi kama pendekezo liliyotolewa na maamuzi mlivyokwishayafanya, nashukuru sana kwa hilo. Sasa nillkuona...uko peke yako hayupo na mwingine? mmoja tu? Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nimesimama kuomba idhini yako ili niweze kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 47 juu ya jambo halisi na la dharura lenye maslahi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, kuanzia siku ya jana katika Mtaa wa Kisopwa na Mtaa wa Mloganzila Mitaa ambayo inabishaniwa kati ya Manispaa ya Ubungo na Wilaya ya Kisarawe kwamba iko upande upi. Kumetokea uvamizi uliofanywa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambao wamehusisha kuchoma mamia ya nyumba za wananchi na kuvunja nyumba za wananchi na mpaka ninavyozungumza na wewe hivi sasa kuna wananchi ambao wamelala nje kutokana na tukio hilo.

Sasa jambo hili ni ladharura kwa sababu bomoa bomoa hiyo pamoja na uchomaji wa nyumba unaendelea hivi sasa na wananchi wanazidi kuathirika. Ningeomba jambo hili lijadiliwe na Bunge kama jambo la dharura ili Waziri Mkuu aweze kuagiza:-

(i) Huo uchomaji wa nyumba na bomoa bomoa inayoendelea usitishwe kwanza; na

(ii) Kuweze kutumwa team ya Mawaziri, Waziri wa Ardhi, Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Ulinzi ili wakatatue huu mgogoro baina ya Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hakukuwa na mgogoro baina ya Jeshi na wananchi. Hapo nyuma kulikuwa kuna madai tu ya wananchi kulipwa fidia kwenye mradi wa *SGR* na wakafanyiwa tathmini. Wakati Wananchi wakisubiri kulipwa fidia, mara kumetokea huu uvamizi ambao umefanywa wa kuchoma nyumba zao na kuvunja nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio naomba kuto ahoja kwamba jambo hili lijadiliwe na Bunge kwa maslahi ya Wananchi wa Mitaa ya Kisopwa na Mitaa ya Mloganzila.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Nimewaona. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali ndiyo tunalipokea suala hili sasa ndani ya Bunge na kwa kuwa ni suala ambalo linahusisha Wizara tatu kama alivyosema mtoa hoja. Ninaomba ikupendeze tuiachie Serikali tuweze kulifutililia kwa sababu mjadala hapa ndani utapelekea lazima Serikali tuweze kutoa maelezo yetu na katika jambo linalofanana na hili ni lazima tuwe tuko katoka *position* ya kulifahamu vizuri na kulitolea ufanuzi unaotakiwa. Kwa heshima kubwa ninaomba utuachie tulifutilie na tuweze kujua kiini na kinachoendelea na kama utaona inakupendeza basi tutarudisha taarifa kwenye Ofisi yako.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika tumesikia hoja yako na pia tumesikia rai ya *Chief Whip* wa upande wa Serikali kwamba kwenye eneo la Ubungo, eneo la Kisokwa na Mloganzila kuna matatizo kidogo ya wananchi na Jeshi letu lakini wote ndiyo tunasikia hivi sasa kutoka kwako kwahiyio kwa hakika ni jambo ambalo ni vizuri tuwaachie wenzetu kwa mapendekezo uliyoyatoa ili walifanyie kazi halafu kwa wakati muafaka

tutaona way *forward* ya jambo hili namna gani twende nalo lakini tumelipokea kama meza. Ahsante sana.

Katibu ulikwishatamka nini kinafuata?

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano yanaendelea, tunaanza na Mheshimiwa Lucy Magereli atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge. Mheshimiwa Lucy. Wachangiaji wote muwepo kwa sababu mtapata nafasi, anayekuwa nje kwa sababu *list* yangu ni ndefu basi atakuwa amepitwa na Treni. Mheshimiwa Lucy.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata nafasi hii kuchangia hoja ya Wizara ya Maji, lakini kabla sijaendelea nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uzima na uhai na kuwezesha kuwepo ndani ya Bunge hili leo kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, neno "Maji" lina herufi nne tu; (M), (A), (J), (I) lakini nadhani ndiyo Msamati mgumu sana ndani ya Bunge hili tangu nimeingia mwaka 2015 mwishoni ndilo jambo ambalo limekuwa likileta mjadala mkubwa, mgumu na ambao hauna majibu. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika kueleza masikitiko yangu kwamba suala la maji tufike mahali labda Serikali iseme imeshindwa halafu tuwape *private sector* huenda tukapata jibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina vipambale. Tunatekeleza miradi mingi, mikubwa kwa wakati mmoja

wakati tunafahamu ya kwamba *resources* ziko so limited, tunatekeleza miradi midogo midogo mingi sana wakati tunafahamu kabisa kwamba *resources* zetu ziko limited badala yake tumekuwa na vipande vingi sana vya miradi ya maji ambavyo havikamiliki, havitoi matokeo, visima vinachimbwa haina maji, pamekuwa na Misamiati tu mizuri ya usanifu wa kina, sijui Bodi, hakuna jibu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 148 nimeona ametaja suala la mradi wa fedha za India ule wa Miji 29, tunashukuru. Bajeti iliyopita mradi huu ulizungumzwa na kiasi hiki cha fedha kilitajwa na kwamba kingeanza kufanya kazi tangu Bajeti ya 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, ni kwa bahati mbaya sana kwamba mpaka sasa bado fedha hizo hazijaanza kufanyakazi katika miradi ya hiyo Miji 29 illyotajwa. Lakini naamini bado nia na dhamira ipo kwa sababu ni fedha za mkopo ambazo tutakwenda kuzilipa kwa kodi zetu. Niwasih Serikali katika utekelezaji wa mradi huu wa Miji 29, naamini walifanya utafiti wa kina kabla ya kuamua ya kwamba ni Mji gani na Mji gani fedha hizo zielekezwe. Basi uwiano wa ugawanyaji wa fedha hizo upelekwe kwa utaratibu kadri ya utafiti ili hatimaye basi angalau kwa mara ya kwanza tupate Miji 29 ambayo inasema sisi sasa hatuna tatizo la maji, limekwisha ili watu wengine wafikiriwe baada ya kuwa mradi huu umekwishakukamilika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika mradi huu wa Miji 29 nashukuru nimeuona Mji wa Mugumu nao umetajwa kwa Mama yangu. Umetengwa shilingi milioni 200 kwa ajili ya kutibu maji katika Bwawa la Manchira. Bwawa la Manchira Mheshimiwa Waziri ni changamoto ya muda mrefu, nimezaliwa pale nimelikuta, nalisikia watoto wanaishai kuogela tu lakini hatimaye miaka mitatu, minne nyuma likaanza kufanyakazi lakini halina ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maji yanayotoka pale yanafanana na ile aina ya Togwa tunayokunywa inayoitwa *Obhosara*. Huwezi kufananisha ya kwamba haya ni maji au

hii no Togwa. Kwa hiyo nikushukuru na nitajisikia vizuri ikiwa hizi milioni 200 zitapelekwa na utaratibu wa kutibu maji yale ukafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera; suala hili nimelifuatilia kwa karibu sana kwa kipindi kirefu, nimezungumza na Waziri, nashukuru amekuwa akinipa mrejesho kila nilipofika kuzungumza naye. Leo sikupanga kulizungumzia lakini nilipokwenda kwenye hotuba ya Waziri nikakuta ametaja ya kwamba pale Kimbiji kwenye visima 20, tayari wamekamilisha visima 19 kwenye ukurasa wa 80, hili linanifanya niongee.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa Kimbiji na Mpera, visima vilivyokamilika ni tisa tu. Waziri anaposema kumekamilika visima 19 kwenye hotuba yake anamaanisha kutoa Ujumbe gani? Bajeti ya 2016/2017 tulijadili suala hili, 2017/2018, 2018/2019 na leo ni 2019/2020 bado hoja ya visima vya Kimbiji na Mpera iko kwneye hotuba ya Waziri. Mradi huu umekuwa ukitengewa fedha lakini ufanisi wake umekuwa mdogo na umekwenda pole pole sana sijafahamu ambacho kimetokea.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nakumbuka Mwaka 2017 wakati huo Waziri wa Maji akiwa Mheshimiwa Eng. Lwenge alikuja mpaka pale kwenye mradi wetu wa Kimbiji na *deadline* ya mradi huu mkataba ulikuwa unakwisa Oktoba, 2017. Mradi haukwisha wakapewa *extension* mpaka Disemba na wakaambiwa baada ya hapo watalipa *penalty* za kuchelewesha mradi lakini ninapozungumza mpaka Disemba, 2017 ule mradi haukwisha leo tunazungumza ni Mei, 2019 bado mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera haujatupa hata kilometra moja ya mtandao wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliuliza swalii hili hili wakati huo ni Mheshimiwa Eng. Kamwele nadhani ndiyo alikuwa Waziri. Na yeze alijibu ya kwamba tayari utaratibu wa distribution unaanza lakini bado hata *distribution* yenewe hajaanza na kwa maelezo ya Waziri anasema ndiyo kwanza wametangaza tenda za ujenzi wa Matenki kwa ajili ya kuanza

distribution. Kwa hiyo mradi huu umemeza fedha nyingi, umechukua muda mrefu kama ilivyo miradi mingine mingi nchi hii ambayo unajikuta kwamba mkataba umetajwa miezi 36, miezi 48 lakini mikata mingi inakwenda ina-*extend* mpaka miezi 60 mpaka 90.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la gharama za juu za uchimbaji wa visima; sijafahamu serikali ina mpango gani baada sasa ya kusuasua kwa uwezo wake wa kuwapatia wananchi maji kuwezesha watu binafsi wanaotaka kuchimba viisma vyao kwa maana ya ku-*subsidies* aidha ile mitambo au hao watoa huduma wapewe aina fulani ya *leave* kusaidia kushusha gharama za uchimbaji visima ili watu binafsi nao ambao hawawezi kufikiwa na hii huduma ya Serikali waweze kujipatia huduma za maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mfano halisi ni Mji wa Kigamboni; Mji wa Kigamboni tangu ulipoumbwa haujawahi kuapata mtandao hata wa mita 600 za maji kwa maana ya maji ya Serikali maji ya DUWASA ama nyininge yoyote. Tumeishi miaka yote tukichimba visima wenyewe virefu na vifupi lakini kwenye mkakati ambao niliusikia kwenye ile Sheria ya usimamizi wa rasilimali za maji namba 11 ya Mwaka 2009 ambayo tulikuwa tumeomba irudishwe Bungeni kwa ajili ya mapitio kwa sababu ina mkanganyiko wa kiutekelezaji ndipo ambapo kuna ile hoja iliyoletwa ya kwamba tutatakiwa kuja kilipia gharama za kumiliki visima binafsi ikiwa tumefanya *initiatives* ya sisi wenyewe kuchimba vile visima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba sana mnapokuja kutekeleza suala hili, Mji wa Kigamboni muuangalie kwa sura ya peke yake. Mwenye kisima chake kama mtataka kuanza kum-*charge* tozo yoyote ya kulipia basi uanze leo usim-*charge* gharama za nyuma kwa sababau ndiye aliyefanya ubunifu wa kuhakikisha kwamba anajipatia huduma ya maji ambayo Serikali haikuweza kumpa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ucheleweshwaji wa kukamilika kwa miradi ya maji; ni kwa bahari mbaya sana

miradi mingi imekuwa na *extensions* za utekelezaji wa mikataba kwa hiyo hata thamani za miradi zinakuwa zinabadi lika badilika kila mara wakati ambapo fedha za Wananchi zinaendelea kutumika kwa wingi na matokeo hayaonekani.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la usanifu unafanyika kabla ya kupata fedha; miradi mingi ya maji imekuwa ikifanyiwa usanifu sijui na upembuzi n.k wakati Serikali bado haina fedha. Kwa hiyo jukumu lile la usanifu linakamilika halafu Serikali haina fedha, badala yake inapofika ule muda sasa kwamba Serikali imepata fedha, ule mradi unakuwa hauna thamani ile ile na kwa jinsi hiyo kukuta kama miradi inakuwa inafanyiwa mipango ambayo inashindwa kutekelezeka kwa utaratibu ambao unakubalika kwa sababu ya kuwa muda umekwishakupita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Taasisi za Serikali ambazo hazili pi ankara za maji. Sifahamu tatafanya nini, kwa sababu kama Serikali kama Wizara ya Maji inasimama leo Bungeni inalalamika katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba kuna taasisi za Serikali; siyo kuna, mimi nahisi taasisi za Serikali zote hazili pi ankara za maji. Kama ndivyo, je, kuna haja ya kuleta hoja Bungeni ya kwamba taasisi hizi zifutiwe kabisa basi utaratibu wa kulipa ankara za maji ili tujue kwamba sio wadeni, hata tunapopanga bajeti zetu, tusifikirie zile fedha za ankara zinazotokana na Taasisi za Serikali?

Mheshimiwa Spika, naomba kwa utaratibu maalum, kama Serikali ingeweza kuangalia shule zetu, wakahakikisha shule zote zinapatiwa huduma ya maji, ingekuwa vizuri. Kwa sababu fikiria watoto wa kike wanapotumia vyoo vya kawaida vya shimo katika mazingira ambayo hakuna maji wala hakuna *toilet paper*, suala la *hygiene* yao limebakii kuwa kitendawili. Labda hawa wangeweza kupewa maji na wakawa *exempted*, tungeweza kuliunga mkono vizuri suala hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mabwawa ya kimkakati. Nasikitika kuona kwamba bwawa la Kidunda

Morogoro limetajwa tena leo na likiitwa bwawa la kimkakati.
(*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Magereli, muda hauko upande wako.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, *one minutes*. Dakika moja ya kwako Mheshimiwa.

SPIKA: Unga mkono hoja. (*Kicheko*)

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muda huu. Mungu akubariki. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Chenge na atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kusema machache kuhusiana na hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kusema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Profesa Mheshimiwa Mbarawa, Naibu wake Mheshimiwa Aweso, timu nzima ya Wizara ya Wataalam ikiongozwa na Profesa Mkumbo na msaidizi wake *Engineer Kalobeloo*, viongozi wote, watendaji na wataalam. Ni miongoni mwa Wizara ambazo kusema kweli zinafanya kazi nzuri, ni kwa sababu tu ya rasilimali fedha zinakuwa zinatuangusha. Tuwatie moyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitaanza na ya nyumbani kidogo, maana mcheza kwao hutunzwa. Nina miradi ya siku nydingi sana ambayo haijapata fedha. Nikianza na Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, kuna visima vilichimbwa tangu mwaka wa fedha 2012/2013, mpaka leo maji yapo lakini wananchi

hawajanufaika na jitihada za kodi zao kupitia miradi hii. Miradi hii ipo Masewa, Igaganulwa, Sengerema, Nkololo na Igegu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Nkololo ni kichekesho kusema kweli, kwa sababu tumepata msaada kutoka Serikali ya Misri na Waziri wa Ujenzi sasa hivi Mheshimiwa *Engineer Kamwele* alipokuwa Naibu Waziri wa Maji alienda akatembelea mradi huu. Ni mradi ambao umetoa maji mengi sana, tunataka tuwasambazie wananchi wa *center* hiyo kubwa ya Nkololo. Amemaliza kuwa Naibu Waziri, akawa Waziri (*full minister*) wa Maji, maji hayajasambazwa. Mheshimiwa Prof. Mbarawa, rafiki yangu, naomba mtusaidie kwa upande wa miradi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi ambao ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu, tuna miradi ambayo tumeleta Wizarani, imesimama miezi sita sasa. Mradi wa Sanungu, Mahina, Nyangokolwa; nilimsikia Mheshimiwa Gimbi asubuhi akiuliza swali la nyongeza, lakini ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Spika, pia Nyakabindi, Bupandagila, kunahitaji kuunganishiwa na kusambaziwa maji kwa ajili ya wananchi hawa na sekondari yetu kongwe ya Bupandagila, wananchi hawapati maji. Kuna Giriku, Kidali Mandam na Mbiti. Kote huko maji yapo, tunataka tu tupate fedha tuwapatie huduma wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Izunya hivyo hivyo. Kisima hiki kina maji mengi sana, tunaweza tukatoa kwa Mitaa yote ya karibu pale Nyamhimbi, Ntuzu na Chenge Sekondari. Yote haya ni mambo ambayo tungependa tuyaone. Ni ombi langu kwa Serikali tuwaone wananchi wa Bariadi kwa jicho la huruma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali hili asubuhi alipoulizwa na Mheshimiwa Gimbi Masaba, naipongeza Serikali yetu kwa

hatua ya msingi ya kuanza kutekeleza mradi wa kutoa maji haya Ziwa Victoria na kuyafikisha katika Miji ya Nyashimo, Bariadi, Lakangabilili, Itilima Pale, Maswa na hatimaye Meatu, Kisesa na Mwanhuzi. Huu ndiyo ukombozi kwetu. Hii ndiyo huwa naita kwa ukanda wetu kama Simiyu. Kwetu hii ndiyo *royalty*, ndiyo mrahaba kwetu wananchi wa Tanzania. Ahsante sana Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli. Sasa tunapata matumaini kwamba mradi huu utaanza kutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye nyongeza ya saba, zipo pesa shilingi bilioni 19.5 zimetengwa kwa shughuli hiyo. Naamini tutaanza vizuri. Najua muda wangu siyo rafiki, hayo ambayo yamo humu ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo wanatarajia kuyatekeleza katika mwaka ujao wa fedha iwapo pesa itapatikana kwa wakati yatatekelezwa. Ni imani yangu kwa Serikali kwamba fedha ikipatikana yatatekelezwa na ninaomba iwe hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili nami niseme tu kwa upande wa shida ya maji nawe unajua, ni kubwa. Lazima tufanye kila linalowezekana kuunga mkono jitihada za kuwapatia huduma ya maji wananchi wetu. Wazo la kuondoa kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji ni moja njia ya kusaidia. Tulianza vizuri huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma tulikuwa tumeondoa kodi kwenye mitambo. Hapa katikati tukajichanganya tena kwa sababu ya ombi letu, misamaha ya kodi imekuwa mingi sana na kadhalika, ndiyo ikatufikisha hapa. Naiomba Serikali tualiangalie tena suala hili. Wenzetu hapa katika *East Africa*, wote wameshaondoa kodi kwenye mitambo ya maji, ni sisi tu hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Fedha, Wizara ya Maji na Serikali kwa ujumla, tumalize biashara hii na *private sector* isaidie katika kutoa huduma hizi. Tutaona viwango vitashuka sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nije kwa hili la hoja ya Kamati. Mimi kama Mbunge, wewe kama Kiongozi wetu, naomba sana, Waheshimiwa Wabunge mnisikilize, naomba sana...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hebu tusikilizane. Kuna *lots of talking, please.*

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, sisi tusimamie maamuzi yetu. Tuna Azimio la Bunge ambalo lilitaka tuongeze shilingi 50 kwa mafuta. Huu ni mwaka wa tatu mfululizo Kamati inasema; sio mimi, Kamati na ni Azimio la Bunge. Sasa sisi Bunge tusipoheshimu maamuzi yetu, nani atayaheshimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba maamuzi yetu tuyalinde kwa wivu wa hali ya juu sana. Mojawapo ni hili. Napenda sana, maana tunajenga nyumba moja, tusigombanie fito na Serikali. Sisi tumetoa pendekexo hili la kuongeza shilingi 50/= kwa kila lita ya mafuta ya *petrol* /na *diesel* /na tunaona *figures* tunazozitaka. Tunataka tufikie kiwango cha kupata shilingi bilioni 300 karibu na 20 na kitu kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itakuja na *alternative* ambayo inatupeleka huko, sisi tutakuwa tayari baadaye kuja kuondoa Azimio letu kwa utaratibu wa Kibunge. Kwa sasa hivi inakuwa ni *very awkward* kwamba sisi wenyewe Wabunge tulipitisha Azimio hapa na Serikali ilikuwepo, haikufanya mabadiliko kwenye Azimio hilo na lipo. Sasa tunataka twende kwenye *force* nyingine, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, sisi tung'ang'anie kwenye shilingi 50/= kwa lita. Halafu tutaisilikiza Serikali kama ina *alternative* ambayo ni *sustainable*, endelevu ya kutufanya tuhangaike na suala zima la maji. Hizi ndiyo kura za uhakika. Unaona, ingekuwa siyo Mfuko huu wa Maji, tungkuwa mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuiunge mkono Serikali, lakini na Serikali ituelewe

sisi kama wawakilishi wa wananchi kwamba tuna hoja ya kujenga na siyo ya kubomoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chenge. Nilishakutaja Mhesimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Naomba nianze kwa kuipongeza sana Wizara. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine kwa kazi nzuri kwa kweli ambayo tunaona mnaifanya. Hata ukiangalia michango ya Waheshimiwa Wabunge toka nimekuwa Mbunge kwenye Wizara ya Maji kipindi cha bajeti, kidogo hii bajeti ya 2019/2020 imejikita kushauri Wizara iweze kuboresha yale ambayo hayakukaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Wizara kwa kutusaidia mradi mkubwa wa maji pale Geita Mjini. Nilichokuwa naiomba tu Wizara, ijaribu kuangalia, kwa sababu huu mradi sehemu unapowe kwa, lile tanki kubwa likiwekwa vizuri linaweza kumaliza kabisa matatizo ya maji Geita Vijiji na Geita Mjini. Kwa hiyo, ni vizuri upembuzi yakinifu ukafanyika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine, huwa napata taabu sana, naijiliza sijui watu wengine huwa wanafanyaje; nimejaribu kuona Wizara ya TAMISEMI kwa Mheshimiwa Jafo, imeanzisha *TARURA*; pamoa na changamoto ilizonazo, lakini kiukweli tunaanza kuona mabadiliko yanayofanyika kule vijiji. Najaribu kuangalia hata Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ummu amefanya vizuri sana. Tumejenga hospitali, zahanati, vituo vya afya, magari, kila mtu kiukweli tunaona kazi zinafanyika. Tatizo, naijiliza huku kwenye Wizara ya Maji kuna mchawi gani?

Mheshimiwa Waziri, lazima tukueleze ukweli. Mheshimiwa Rais anapozunguka kila siku anakueleza kuna wezi, hushughuliki nao; anakueleza, Wizara imeoza, hushughuliki nao; Waheshimiwa Wabunge humu, nimemsikia ndugu yangu Mheshimiwa Keissy jana amesema kuna mwizi kaiba, haushughuliki nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu naomba nitoe ushauri wangu, hata kama tungeongeza shilingi 200/=, hii Wizara ina wezi, zitaenda kuliwa. Ukimsimamisha kila Mbunge humu ndani, kila atakayesimama ana mradi wa maji lakini umepigwa; kila anayesimama humu, atasema mimi nina mradi, lakini umepigwa.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na mradi wa Chankolongo kwa dada yangu Mheshimiwa Lolesia toka mwaka 1978, umekamilika mwaka huu. Tuna mradi kwa Mheshimiwa Hussein Nassor Nyang'hwale, umepigwa mabilioni, umekamilika *term* hii. Kila Mbunge atakayesimama hapa ana mradi lakini umeibiwa. Sasa ninachouliza Waheshimiwa Wabunge tunataka kubebesha mzigo wananchi wetu mara kwenye simu, mara kwenye mafuta, tukaongeze hela kwa watu wanaotubia hela, haiwezekani. Hayo ni mawazo yangu, haiwezekani. Tutafute kwanza mchawi wa hii Wizara. Profesa fukuza wezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli tuseme tu wazi, alifumua Mainjinia nchi nzima. Leo *TANROADS* imesimama, ilikuwa na wapigaji. Sasa wewe kila siku Mheshimiwa Rais akienda huko, kisima; jana nilikuwa naangalia kwenye *TV*, Mheshimiwa Rais kasimamishwa huko aliko Mbeya watu wanalamika kisima kimechimbwa kwa shilingi milioni 475. Kuna Mkurugenzi, kuna *engineer* na ziara mnaenda.

Mheshimiwa Spika, nashauri Waheshimiwa Wabunge, tusijaribu kuongeza hela, hizi hela ni nyingi sana. Tusijaribu kabisa. Kama tumetumia leo shilingi bilioni 300 na kitu, hii kitu haiwezekani kuwaongeza wezi hela, tutafute kwanza mchawi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kule vijijini mimi huwa najiuliza, Maprofesa wetu na Mainjinia, ukitoka hapa kwenda Mwanza utaona madaraja zaidi ya 1,000. Madaraja kazi yake ni kupitisha maji; maji yanaachwa tu yanasaambaa yanaenda kupotea maporini. Ikija hela ya utafiti, watafiti wanaenda *ku-drill* kwenye milima ambako hakuna maji. Tunakosa maji na hela zimelipwa, haiwezekani. Naomba kabisa, suala la kuongeza hela shilingi 50/=, kama Waheshimiwa Wabunge tutajaa kingi hii ya kukubaliana naye, anayebeba mzigo ni wanyonge walioko kwetu. Kuna watu wanaishi kwa kipato cha shilingi 5,000/=, analima mchicha, ukamwambie akatwe shilingi 50/= anampigia mtu njoo ununue mchicha wangu shambani, hiki kitu hakiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba, Profesa anafanya kazi vizuri sana, Profesa Mkumbo anafanya kazi vizuri, Naibu Katibu Mkuu *Engineer* jamani, mkishindwa *term* hili labda tufute tu hii Wizara. Kwa sababu mimi najiuliza, hili suala kuanzia Profesa Mwandosya alishindwa maji, akaja Prof. Lwenge akashindwa, akaja Profesa Maghembe akashindwa, hebu jaribuni basi na darasa la saba. Mimi nitaziba mitaro tu, yatajaa maji kwa watu wote humu ndani. Hiki kitu hakiwezekani. Serikali mjiulize mara mbili. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana jana nilikuwa nasikia ndugu yangu Mheshimiwa Mboni hapa analia, ooh, Mheshimiwa Mbarawa tupe maji, Mheshimiwa Aweso tupe maji, Mkumbo tupe maji. Huyu atatoa maji wapi? Angekuwa Mheshimiwa Mwijage na Mbunge wa Bukoba wangetoa maji. Hawa watu wa hapa Singida utatoa maji, hayo maji yana chumvi, haiwezekani. Nilichokuwa naomba, tuangalie kwanza tatizo tulilonalo ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hakuna sehemu ambayo Mheshimiwa Rais anapata shida kubwa ya maswali na Waheshimiwa Wabunge tunadhalilika kwa sababu ya maji.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano, kwenye Wilaya yangu nilikuwa na mradi huo niliosema wa Chankorongo, tumejenga miaka 20 na kitu hauishi; mara tanki linapasuka,

mara linafanya hivi. Akaja Mheshimiwa Jafo, nikamwambia mimi ni mkandarasi wa darasa la saba, lakini nina wasiwasi na huyu *engineer*, hebu tukague cheti chake. Huyu *engineer* gani anatengeneza bwawa linafumuka? Tulipokagua tukakuta ana cheti cha *environmental*. Tukafukuza, maji yameanza kutoka. Hivi Profesa unataka ufundishwe *design* gani?

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tusijaribu kuingia kingi ya kutoa shilingi 50/=, hakuna 50 inayotoka, wananchi wetu ndio tutakaowapa mzigo. Kama tunataka kuongeza shilingi 50/=, lazima tuangalie anayeongezewa mzigo ni nani? Sisi Waheshimiwa Wabunge tunavaa suti, tuna mshahara mzuri. Kuna watu kule wanaauza mchicha, wanaauza dagaa, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wako watu wazuri sana, sipigli debe, mimi natoka Kanda ya Ziwa. Kuna *engineer* anaitwa Sanga kule, miradi yote inayoshindikana kutoka Halmashauri anapewa, anakesha vijiji kule, kamaliza mradi wa Lolesia, kamaliza Chato, kamaliza mpaka Musoma. *Engineer* Sanga, kwa nini watu wazuri kama hawa wasipandishwe vyeo ili uzuri wake ukaonekana nchi nzima? Kuna watu wabovu kabisa wamekalia madaraka, hela zinatumwa Halmashauri halafu tena zinakuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameenda Lindi amekuta Mhindi ameshalipwa hela mradi hautoi maji. Alivyosema nyang'anya *Passport*, watu wameanza kushughulika na hela zililipwa. Chalinze hivyo hivyo hela zimeliwa; Morogoro, kila mahali, halafu tukaongeze tena hela ndugu zangu. Ukienda kwa Mheshimiwa Keissy hela zimeliwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hili suala la kuongeza hela, tuondoeni hayo mawazo Waheshimiwa Wabunge, tushughulike na hela tulizonazo. Hizi shilingi bilioni 600 zikienda zote; na ushauri wangu kwenye Serikali, ili kuondoa hii kesi, toeni hela kwa muda muafaka. Hizi shilingi bilioni 600 zikitolewa kwa muda muafaka, watu wote watajaa maji.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ushauri wangu. Nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Haya, ushauri huo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante. Nilishakutaja Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, na mimi nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja muhimu sana ambayo ipo mbele yetu. Hoja ya maji ni hoja ya uhai na kiukweli mtu unaweza ukaishi bila chochote, lakini huwezi kuishi bila kupata maji. Kitendo cha Serikali kuendelea kutoa fedha kwenye kidogo kwenye Wizara ya Maji kwa asilimia 51 zilizotolewa kwa bajeti iliyopita, kwa mwendo huu hatuwezi kutatua tatizo la maji na ile *spirit* ya kumtua mama wa Tanzania ndoo kichwani haitafikiwa na *spirit* ya kutaka mtoto wa kike wa Kitanzania asome, apate *full education*, awe mtu wa maana haitafikiwa. Vile vile pia *spirit* ya kuona kwamba kila Mtanzania au wananchi wote wanaenda kwenye shughuli za maendeleo na kuachana na shughuli za kusaka maji haitakaa iishe.

Kwa hiyo kwanza ni lazima kwenye Sekta ya Maji fedha inapotengwa kwenda kufanya kazi ya kuleta maji itoke kikamilifu ikafanye kazi ya kuleta maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono Wabunge wote waliosimama kusema kwamba Mfuko wa Maji uongezewe; Mfuko wa Maji lazima uongezwe. Hatuna namna nyingine zaidi ya kuhakikisha kwamba kuna fedha ya kutosha kupeleka maji kwa wananchi wetu. Tumeona mfano mdogo wa *REA*, sasa hivi kila Mbunge akisimama anagusia *REA* japo sio vijiji vyote angalau kuna kazi imefanyika imeonekana. Kwa hiyo, naiomba Serikali na naomba niungane na wale wote waliosema patachimbika Jumatatu hapa kama fedha ya Mfuko haitaongezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kaliua tuna shida kubwa sana ya maji; mwanamke wa Kaliua anateseka sana, mtoto wa Kaliua hata shulen i wanakwenda kuvamia kwenye nyumba za watu kutafuta maji ya kunywa; nyumba za walimu na wananchi waliopo jirani. Wilaya ya Kaliua tunaomba kipaumbele cha hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kaliua kwanza kabisa jiografia yake na Mkoa wa Tabora hatuna maji ardhini, kwa hiyo Miradi yote ya Maji ya *World Bank* na visima hatunufaiki navyo kwa sababu hatuna maji ardhini. Kingine jiografia ya maeneo yetu hakuna mito kama ambayo inatamkwa Morogoro, Kaliua, Tabora hatuna mito hiyo, tuna Mito ya Igala na Malagarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na mpango wa kutoa maji Malagarasi kuleta Kaliua na Wilaya ya Urambo, lakini pia mradi mwininge ni kutoa maji Victoria kuja mpaka Igunga, Nzega, Tabora na Uyui. Ule mradi wa Malagarasi ambao sasa hivi ni mwaka wa nne ulikuwa umetengewa fedha kidogo kidogo ya kuanza kufanya usanifu yakinifu.... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Sakaya...

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: mpaka leo hakuna chochote ambacho kimefanyika...

SPIKA: Mheshimiwa Sakaya kidogo...

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: mwaka huu Serikali imekuja na mpango kwamba...

SPIKA: Mheshimiwa Sakaya kidogo tu, Waheshimiwa Wabunge hebu tupunguze sauti, hata sisi wenyewe tunaweza kusikia hasa upande huu wa CCM, kwa nini CCM hatusikilizi? Tutulie kidogo hata kama unaongea na mtu, ili mjadala uwe na maana, lakini sasa maeneo haya, ni kama mikutano ya hadhara kabisa. Endelea Mheshimiwa.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona kwamba mradi ule wa Malagarasi utakuwa na gharama kubwa, umekuja na mpango mwингine wa kuweka Kaliua na Urambo kwenye mradi wa miji 29. Nashukuru kwa kuwa tumewekwa kwenye huu mradi wa miji 29 ila kwa hamu kubwa ya maji ambayo tunayo, tunaomba huu mradi uende haraka tuweze kufanikiwa kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nimeangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Kaliua imewekwa kama ni sehemu ya Urambo, nakubaliana kweli Wilaya ya Kaliua tulizaliwa kutoka Urambo lakini ni Wilaya inayojitegemea, inayosimama, tuandikwe kama Wilaya na sio mtoto wa Urambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa tumepata mradi huu ambaao ni wa miji 29, lakini bado kwa mradi alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba, utoalisha kilomita 12 kutoka barabarani kuja Wilaya ya Kaliua. Jiografia ya Wilaya ya Kaliua ni kubwa sana, kutoka Makao Makuu ya Wilaya kuna mwananchi anayeishi kilomita 120, kilomita 90, kilomita 60, kilomita 30 mpaka unafika. Kwa hiyo, mwananchi huyo ambaye anaishi kilomita 60 atapata wapi maji? Huyu wa kilomita 90 na kilomita 120 watakunywa wapi maji? Naomba waifahamu jiografia ya Kaliua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachoomba pamoja na mradi huu ambaao wa miji 29, lazima uwepo mradi mwингine wa kuweza kutoa angalau maji kutoka Mto Ugala ambaao ni mto pekee ambaao tunao Kaliua uweze kulisha wananchi ambaao wapo mbali ambaao hawatanufaika na mradi wowote, aidha ni Malagarasi hautawafikia au ni huo wa kutoka Mjini Tabora hautawafikia. Kwa hiyo, ni lazima kuwepo na mpango wa kuhakikisha wale ambaao hawanufaiki na mradi huu uliopo wanapataje maji kwa sababu na wenyewe ni Wanakaliua na ni Watanzania, wana haki ya kupata maji na kupata maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia kuna mradi mdogo ambao unaendelea pale Kaliua Mjini ambao ni wa Kata ya Kaliua na Kata ya Shokora, naomba pia Serikali itoe fedha kwa wakati mradi huo ambao ni mradi wa Kata mbili tu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mradi mwingine ambao tunaomba Serikali itusaidie, tumeppata kisima kimoja kimechimbwa na *G7*/pale Kijiji cha Usindi, Kata ya Ushokola. Maji yale ni mengi sana, tunaomba Serikali isaidie kuyasambaza yaweze kulisha eneo kubwa, kwa sasa hivi yamelisha kijiji kizima cha Usindi. Tunaomba iwekwe nguvu ya kutosha na *G7*/wapo tayari kusaidiana na Serikali uweze kusambazwa, uweze kulisha angalau kata nzima, inawezekana na ni kisima cha kwanza katika Wilaya ya Kaliua kuweza kuchimbwa kikawa kina maji ya kulisha angalau kata nzima. Kwa hiyo, naomba Serikali iweke nguvu zake pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Wakala wa Uchimbaji; mwaka 2016/2017, Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa walikuja Kaliua wakafanya utafiti katika maeneo mengi, wakaainisha maeneo tisa ya kuchimba mabwawa na wakasema kutokana na jiografia yetu, watafanya haraka kuweza kuja kutusaidia kuchimba mabwawa ili tukusanye maji ya mvua, lakini mpaka leo ni mwaka wa tatu hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, naomba Serikali wale Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa waje Kaliua, tayari walishakuwa na mpango ule, waweze kuhakikisha kwamba maeneo yale yaliyoainishwa yanachimbwa mabwawa tuweze kukusanya maji ya mvua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni uvunaji wa maji. Bajeti ya mwaka 2017/2018, Serikali ilikuja na mipango mizuri sana hapa Bungeni kwamba ilikuwa imetoa maagizo kwenye Halmashauri zote nchi nzima na kutunga sheria ndogo kuzitaka taasisi za kijamii, asasi na watu binafsi kujenga miundombinu ya kuvuna maji. Pia wakati huo huo ikatuambia kwamba Serikali ilikuwa imetoa mafunzo kwa wananchi

karibu 795 kwa ajili ya kutumia mbinu sahihi na nyepesi kuvuna maji.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ikasema ilikuwa imejenga matenki makubwa 29 na 59 na ukubwa tofauti kukusanya maji katika Wilaya mbalimbali. Sasa nategemea Waziri akija ku-*wind up* atuambie huu mpango umefikia wapi? Wananchi wangapi wameendelea kupewa elimu na matenki mangapi yameendelea kujengwa? Pia tujue kwamba maagizo yaliyotolewa kwenye Halmashauri mbalimbali yametekelawa kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa mtu anayetoka nje kuiona Tanzania, akiona mvua zinaponyesha maji yanavyosambaa yanavyoharibu miundombinu akisikia tunalia maji hapa Bungeni, atatuona kama tumechanganyikiwa kiasi fulani kwa sababu hakuna juhudhi ya kukusanya maji haya, hatuyakusanyi kabisa, yanakwenda kuharibu barabara, nyumba na kila kitu lakini kilio cha maji kipo pale pale. Kwa hiyo, kwa maana nyingine lazima Serikali ijpange kikamilifu kukusanya maji ya mvua, hii ni neema wakati mwingine, tuitumie kuhakikisha kwamba tunapunguza tatizo la maji. (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye sekta hii muhimu. Pia naomba niungane na

wewe kuipa pole familia na watoto wa Mzee Mengi kwa kuondokewa na baba yao. Nilivyokuwa Waziri wa Uwekezaji, Uwezeshaji na Sekta Binafsi ndiye alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pole hiyo, sasa naomba nichangie kwenye sekta hii muhimu na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa sababu kila anapoongea na anapokuwa kwenye mikutano ya hadhara, jambo kuu analoliiongelea ni kumtua mama ndoo kichwani, jambo ambalo kila mmoja wetu hapa nina hakika analipenda kwa sababu bila maji hakuna uhai, uchumi na maendeleo. Kwa hivyo, analolifanya Rais ni jambo muhimu na nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote ili waweze kuona kwamba azma hii ya Mheshimiwa Rais na wananchi wa Tanzania inafikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo; Wilaya yetu ya Hanang ni Wilaya ambayo ni kavu, kwanza ipo kwenye *lift valley* na kwenye *lift valley* kule chini maji yanapatikana kwa shida sana. Ningependa kuanza na kuwapongeza sana Serikali kwa sababu walitoa shilingi bilioni 2.5 ili kuiletea Makao Makuu ya Wilaya maji na tulitegemea mwaka jana mwezi wa Tisa maji ya Katesh yawe yamefika lakini mpaka hivi nasimama hapa, mradi umetekelizwa kwa asilimia 66 tu. Naomba sana yafuatayo yafanywe; kwamba kuna wakandarasi ambao wanadai hela zao na *certificates* zimefika, naomba jamani tuweze kulipia *certificate* hizo ili maji ya Katesh yapatikane, siyo jambo zuri kwa Makao Makuu ya Wilaya kutokuwa na maji ya uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika,vilevile, nafurahi sana na kuipongeza Serikali kuchimba visima ambavyo vinatumia *solar* katika Kijiji cha Gehandu, Kijiji Garbapi, Kijiji cha Gidika, Kijiji cha Hirbadaw, Kijiji cha Gawlolo, Kijiji Murumba, Kijiji cha Dawar, Kijiji cha Ginirish na Kijiji cha Laghanga. Naishukuru Serikali kwa nini si rahisi kuwa na visima vingi kwa wakati mmoja, lakini naomba mradi huu uwe wa maana kwa wananchi kwa sababu kutokana na kuwa kwenye Kamati hii ya Maji nimetembelea sehemu nyingi, visima vingi vina

solar ambazo zina betri lakini visima visima vyote nilivyovitaja na najiuliza kwa nini. Naomba Mheshimiwa Waziri ajue kwa nini visima vile vinaendeshwa na solar ambazo hazina betri na wanajua Hanang ni eneo moja ambalo lina baridi kwa hiyo maji hayatapatikana kwa ufanisi kama tunavyotaka.

Mheshimiwa Spika, lingine ni lile alilloongelea Mheshimiwa Musukuma kwamba tunatoa mradi na hela zinatolewa, tuna mradi wa Kijiji cha Gehandu ambaao tayari ulishapokea shilingi milioni 183 lakini mpaka leo kisima hakijatoa maji na ni muda mrefu sio mwaka mmoja ni miaka zaidi ya miwili. Naomba Waziri aweze kuona ni kwa nini jamani inachukua muda mrefu kupita kiasi kwa miradi kuwa tayari na wananchi waweze kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile niongelee suala la Mfuko wa Maji; Mfuko huu ndiyo utakuwa ni namna ya kuondokana na tatizo hili kubwa la huduma nyeti ya maji. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuheshimu azimio letu, nami nasema kwamba Mfuko huu wa Maji ndiyo uliofanya tutekeleze miradi mingijamani. Kwa hiyo, sasa tukirudi nyuma tutarudisha bidii iliyoukwepo nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ile Sh.50 ya kutokana na mafuta iongezwe lakini na vyanzo vingine navyo viongezeke kwa sababu hata hiyo Sh.50 haitaondoa tatizo linalotukabili kutokana na ukosefu wa maji. Naomba sana ndugu zangu vyanzo vingine kama simu *Vodacom*, *Airtel*/na vyanzo vingine vingi vije tu kwenye maji, tukiondokana na tatizo la maji, matatizo mengine kwenye sekta zingine yataondoka vilevile. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Musukuma asikubali kwamba wale wenye petroli wamtumetume humu ndani waseme kwamba hii isitokane na petroli. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Kwa hiyo naomba sana kama ata...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: ataona kwamba hilo...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mama nakuhestimu sana, eeeeeh aisee.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma hujaruhusiwa kusema tafadhalii, Mheshimiwa Mary Nagu endelea.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Anisamehe kwa jambo lolote kwa sababu na yeeye namheshimu, lakini naomba kwa kweli suala la Mfuko wa Maji kama alivyo sema Mheshimiwa Chenge na walivyosema wengine, wote tulismamie kidete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba jambo moja ninamshukuru Mwenyezi Mungu na nawashukuru na Marais walioniteua kuwa Waziri, Waziri wetu naye akajenge hoja kule Serikalini ili Serikali ione umuhimu wa kuongeza Mfuko huu ambaao tayari kama si Wizara hii kujenga hoja, haitoshi kuongea hapa Bungeni peke yake bali kwenye *Cabinet* na Waziri na wenzake wengine wasaidiane kuona na Serikali inaona umuhimu huo, nina hakika ukosefu wa maji... (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kuhusu utaratibu

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Inaongeza...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kuhusu utaratibu

SPIKA: Nipe kanuni

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64(1).

SPIKA: Isome.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Sasa namwomba mama athibitishe kama mimi nimetumwa na watu wa petroli, vinginevyo atoe kauli yake.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji ya wanawake na wananchi wa Tanzania ni makubwa. Kutokana na kuona umuhimu huo, kama nilisema jambo ambalo halimpendezi yeye basi avumilie na anisamehe. Naomba sana ndugu zangu suala la maji ni muhimu, ni kweli kwamba kuna watu ambao siyo waaminifu kwenye sekta hii, lakini kuna watu ambao wanafanya kazi kwa nguvu. Naomba Mheshimiwa Waziri kama Wabunge walivyosema, aunde hata tume kuona ma-engineer ambao siyo waaminifu waondolewe ili suala la maji lioneokane kama linapewa nguvu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na sitaki hata kuitisha muda wangu, kama umebakia wengine waongee kuona kwamba hoja ya kuongezea fedha Mfuko wa Maji inaendelezwa vizuri na Mheshimiwa Musukuma akiondoka ananiheshimu, namheshimu, tutaongea naye hapo nje. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Waarabu Wapemba hao, wameshamaliza.

Mheshimiwa Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Charles Kitwanga ajiandae. (*Kicheko*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii ya Wizara ya Maji. Kwanza kabisa, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya kwa ajili ya kuhudumia Watanzania hasa miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni tatizo la maji katika Mji wa Mpwapwa. Mji wa Mpwapwa maji tunayo lakini

hayatoshi. Idadi ya watu inaongezeka sasa ni zaidi ya laki moja na bado vyanzo vya maji vinavyotumika ni vile vile vya zamani na usambazaji wa maji Mji wa Mpwapwa kuna maeneo mengi sana maji hayafiki. Kwa mfano, maeneo ya Ving'hawe, Namba 30, Mang'hangu, Ilolo, Kwamshangoo, Behelo pamoja na Majumba Sita na Mbuyuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile maji ni shida sana hasa kwenye taasisi kwa mfano Shule ya Sekondari ya Mpwapwa na Chuo cha Ualimu Mpwapwa wanafunzi wanapata matatizo makubwa, wakati fulani wanabeba ndo kwenda kutafuta maji maeneo mengine. Mheshimiwa Waziri, maji yetu ni ya chumvi lakini sina maana kwamba ayabadilishe yawe baridi (*soft water*), hapana, lakini Wizara mwaka 2008 mimi nikiwa Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Serikali iliahidi kuchimba visima sita vya maji baridi maeneo ya Ilolo na Kwamshangoo, mpaka sasa hakuna kilichofanyika. Walishafanya *survey* na wakagundua kwamba kuna maji baridi eneo la Ilolo na Kwamshangoo. Sasa naomba kwa Mheshimiwa Waziri, Wizara yake ilitekeleze, visima sita vichimbwe ili kuongeza wingi wa maji katika Mji wa Mpwapwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni miradi ya maji katika Jimbo langu. Kuna miradi minne ambayo inaendelea mpaka sasa, Kijiji cha Bumila, Iyoma, Mzase na Mima. Sasa ni mwaka wa tatu miradi haikamiliki, wakandarasi wapo *site*, sasa kama hawawalipi hawa wakandarasi hii miradi itakamilikaje? Wananchi wa vijiji hivyo wanaendelea kupata shida ya maji, hiyo miradi itakamilika lini; wawalipe wakandarasi ili miradi hiyo ikamilike, namwomba sana sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri afike katika vijiji hivi na yeye mwenyewe awaeleze kwa nini miradi haikamiliki. Nimeeleza sasa nimechoka na siwezi kukosa kura katika vijiji hivyo kwa sababu miradi haikamiliki, afike yeye mwenyewe kuwaeleza wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, katika bajeti ya mwaka 2018, Wizara ya Maji iliahidi kuchimba visima katika vijiji vifuatavyo:-

Kijiji cha Kisima, Kijiji cha Mgoma, Gulwe, Lupeta, Chitemo, Igoji I, Iwondo, Kazania, Kiegea na Ng'hambi lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika na tayari Mhandishi wa Maji wa Wilaya ya Mpwapwa alishatoa orodha kwamba mpango wa kuchimba visima upo na mpaka sasa hata kisima kimoja hakijachimbwa. Sasa nielezwe hizo hela ambazo zilitengwa zimekwenda wapi, naomba anieleze Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, maji ni uhai, maji ni uchumi na maji ni maendeleo. Kwa hiyo, naomba sana miradi inayopangwa na fedha ambazo zinapitishwa na Bunge ziende kwenye miradi husika. Jambo la kushangaza, Bunge kama Bunge tunapitisha fedha katika Bunge lako Tukufu lakini fedha hizo nyingi hazifiki kwenye maeneo husika. Kwa hiyo, inakuwa Bunge hapa tunafanya kazi ya bure na miradi mingi sana siyo maji tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tupo hapa miezi mitatu kuitisha bajeti ya Serikali kwa ajili ya miradi na matumizi mengine lakini fedha zinazotolewa hata asilimia 50 hazifiki, sasa hizo fedha zinakwenda wapi na kuna miradi mingi sana viporo, kwa mfano, miradi ya maji ni mingi sana hajikamilika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii miradi inayopangwa itekelezwe. Maji ni siasa, ukishasema kwamba Serikali imeahidi kuchimba kisima cha maji katika kijiji na mradi haujatekelezwa, hii ni siasa na uchaguzi ni mwaka kesho tutapata shida sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nikushukuru, nirudie tena kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maji lakini naomba sana miradi hii itekelezwe ili wananchi wetu waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Seneta Lubeleje. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala ajandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu lakini zaidi kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye *page* yake ya 2, Waziri anakiri kwamba maji yana mchango mkubwa kwa maisha ya watu, kwa maendeleo ya uchumi na jamii. Kinachoshangaza Serikali haioneshi kuipa kipaumbele Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata bajeti ambazo tunapitisha hapa, bajeti ya mwaka 2018/2019 tulipitisha shilingi bilioni 673 lakini kwenye hotuba Waziri anasema mpaka Aprili zimeenda shilingi bilioni 344 ambayo ni sawasawa na asilimia 51 tu na hizi zote ukiangalia sanasana zimetoka kwenye Mfuko wa Maji. Watanzania tumekuwa tukihangaika na maji, wengine wanapoteza maisha wakienda kutafuta maji wanaliwa na mamba, akina mama wengine wanabakwa na ndoa zinaharibika lakini haya yote Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kuweza kuwekeza kwenye Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya watu. Waziri ameendelea kukiri kwamba kiasi cha mtu anachotumia maji kimepungua kutoka zaidi ya 7,600 mpaka 2300 lakini hamna mkakati ambao unawekwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi niombe Wabunge, pamoja na kusema kwamba tupitishe hili Azimio la shilingi 50, sasa tuitake Serikali kama vile ambavyo inafanya kwenye Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, inapeleka hela hata ambazo zingine hatujapitisha hapa Bungeni iweze kuipa kipaumbele Wizara ya Maji ili *once and for all* tuwekeze kwenye miundombinu ya maji vijiji na mijini, tu-*solve* hili tatizo ili sasa huu Mfuko

ambao tunaupigania ubaki kufanya *maintenance* ya ile miundombinu ambayo tumeweka vinginevyo hatuwezi kufikia hata uchumi wa viwanda bila maji. Naomba kabisa kama Bunge tuitake Serikali sasa ije kwanza na bajeti yenye uhalisia ambayo imesheheni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine nataka kuzungumzia kuhusu takwimu ambazo Waziri anatoa za Watanzania wanaopata maji. Vijiji mnatuambia asilimia 64 na wanasema wanazi-drive hizi kwa kuangalia zile *center* za kuchota maji, sijui ni vijiji vipi hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi vijiji ambavyo nimepitia Tanzania hata kama mnafanya kwa *average*, suaona vijiji ambavyo unaweza uka-*generalize* ukasema Watanzania kwa sasa wanapata maji kwa asilimia 64 na *target* mwaka 2020 mnataka muwe mmefikisha maji vijiji kwa asiimia 95. Tunavyoongea kufikia mwaka 2020 tuna mwaka mmoja tu lakini mnaweza mkaona uhalisia Wabunge wakisimama adha za maji wanazosema Majimboni kwao. Sasa hii asilimia 95 vijiji tutaifikia kweli au tumekuja hapa tunaongea *tuna-document* inapita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mijini mnasema kwenye miji ni asilimia 64, mimi kwangu pale Tarime na nimekuwa nikisimama nalalamika pamoja na kwamba ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Tarime lakini ni kata mbili tu ambazo zina maji kati ya kata nane na hizo kata mbili sio wananchi wote ambao wameunganishiwa. Tunataka Serikali ituambie mikakati ambayo ina dhamira ya dhati ya kutekeleza Sera ya Maji ya Mtanzania kupata maji ndani ya mita 400. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, narudia kusema tukiamua kuwekeza kwenye maendeleo ya watu inawezekana. Kama vile ambavyo Serikali ya Magufuli/CCM mmeamua kuwekeza kwenye miundombinu ambayo ni maendeleo ya vitu na tunaona kweli mmewekeza kwa zaidi ya asilimia ambayo tumepitisha hapa hivyo hivyo tupeleke kwenye maji ili tutatue na tutekeleze Sera ya Maji kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa kuhusiana na Jimbo langu la Tarime. Tuna miradi mingi ya maji; kuna mradi wa Gamasala ambao umekwama ungeweza kusaidia kule Nyandoto. Waziri, Mheshimiwa Kamwelwe alienda akaona na nimeuliza swali hapa ukasema sasa fedha zimepatikana lakini mpaka sasa hivi navyoongea mkandarasi bado hajapelekewa fedha. Mheshimiwa Waziri unapokuja ku-*windup* naomba mtuambie ule Mradi wa Gamasala unaenda kukamilika lini na ni lini mkandarasi atarudi *site?*

Mheshimiwa Spika, kingine ni kuhusu Bwawa la Nyanduma. Mmekuwa mkitenga shilingi milioni 300 na nashukuru na hapa mmetenga tena lakini mnatenga shilingi milioni 300 kwanza hazikidhi haja lakini tutashukuru zikija zitaweza kufanya ukarabati wa kuhakikisha kwamba wananchi wa Tarime hawapati yale maji ambayo wanayapata sasa hivi ambayo ni mchafu, unaweza ukafikiri ni ubuyu, chai ya maziwa imewekwa pale. Kwa hiyo, hizi shilingi milioni 300 ambazo mmezitenga hapa tungependa kujua sasa hivi mtazileta au itakuwa kama kila mwaka zinavyotokea kwenye kitabu lakini haziji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru, nimeona mmetenga zaidi ya shilingi bilioni 600 ingawa hazijanyambulishwa ambazo zitakuja Tarime, napenda kujua hizi zinaenda kwenye nyanja zipi, nimejaribu kutafuta sijaona. Maana najua tunawadai visima 23 ambavyo viro tangu mwaka 2017/2018 na 2018/2019 lakini hazijaenda mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, pia niliuliza swali hapa ukanihakikishia kwamba umewaambia *DDCA* waende maana wanasubiria fedha, ukasema umeagiza waende mara moja, imepita takribani sasa hivi mwezi sijawaona kule Tarime. Napenda nihakikishiwe hawa *DDCA* wanaenda lini maana ulisema fedha zimeshapatikana ili sasa zile kata za pembezoni za Nyandoto, Nkende, Kenyemanyori na Kitale waweze kupata maji wakati huo sasa tukisubiria Mradi wa Ziwa Victoria ambao nao pia nashukuru mmeuweka hapa kwa zile fedha za India.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati tunasubiria huo mradi mkubwa kutoka Ziwa Victoria ambao utapeleka maji Rarya na Tarime, nitake kujua hivi visima 23 ni lini vinaenda kuchimbwa maana vipo tangu mwaka uliopita na uliniahidi. Kwa hiyo, mkitufanya hayo walau zile taasisi mbalimbali ambazo zipo ndani ya Mji wa Tarime kuna magereza, hospitali na biashara nyingi maana Tarime ni mji ambao unakua wataweza kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, samahani, nataka kujua maana tusije tukasahafulishwa, Wabunge wote tunajua msisimko ambao tulikuwa nao Bunge la bajeti lilllopita la mwaka 2018/2019. Kulionekana kuna ujisadi mkubwa sana, hata mimi mwenyewe nilisimama nikataja ujisadi ule wa mkandarasi kule Geita. Hata siku zile Mheshimiwa Eng. Kamwelwe akasema kwa kweli mimi naogopa hata msinipe tena hela mpaka tuhakkishe huu ujisadi ambao mmeutaja hapo umefanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tujue sasa kabla hatujawapa hizi hela ambazo Mheshimiwa Kamwelwe aliogopa kuzipokea, ule ujisadi wote ambao tuliutaja kwenye miradi mbalimbali ya maji hapa nchini mmechukua hatua zippi ili sasa muweze kutuaminisha sisi kwamba tunaweza kuweka fedha nyingi kwenye hii Wizara na zisipate ubadhirifu wowote ule. Kinyume na hapo hatuwezi kuja tu tunakaa hapa tunapitisha fedha zinaenda, zinatumika vibaya, leo ukikagua miradi mingi maji hayatoki, lakini fedha zinaenda tu, hii itakuwa siyo ufanisi wa Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusisitiza kabisa na kwa nia ya dhati kabisa kwamba kama nchi maji ni mojawapo ya kichocheo cha maendeleo. Bila maji wananchi watakuwa wanapoteza muda mwangi kuliko kufanya kazi zao za shughuli za maendeleo. Bila maji safi na salama, tunakunywa maji watoto wetu wanapata vichocho. Ukipatapata kichocho ina maana unaipelekea Serikali gharama kubwa ya kuweza kumtibu huyu mwananchi, kwanza anaacha kufanya kazi lakini pia inakuwa ni gharama kwenye hospitali zetu ambazo pia tunajua hazina madawa

ya kukidhi mahitaji. Kwa hiyo, mwananchi asipopata tiba mbadala pia ina maana tunampumzisha kwa amani. Tukiwekeza kwenye maji tutaenda kuondoa haya yote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuishia hapo lakini naunga mkono hoja ya upinzani, yale yote ambayo yamewekwa mle tuyachukue na tuyafanyie kazi na michango yote ya Wabunge ambayo ina tija tufanyie kazi kwa maendeleo ya taifa letu, ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kitwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai. Kwa sababu leo ndio nasimama kwa mara ya kwanza kuzungumza Bungeni hapa baada ya kupata matatizo ya kuugua, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Wanamisungwi ambao waliacha kufanya kazi zao wakaamua kuwaomba Mapadre na Wachungaji kwa siku mbalimbali kuweza kuniombea niweze kupona. Siyo Wanamisungwi tu, nimshukuru sana Mheshimwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa *support* na kwa jinsi walivyoweza kufika kuniona wakati nikiwa naumwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mheshimiwa Karume aliyefika kuniona. Namshukuru sana Makamu wa Rais wa Zanzibar, wao wanamuita Makamu wa Pili, mimi sitambui hilo kwa sababu hakuna wa kwanza, kuna Makamu wa Rais tu Zanzibar. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kuniombea. Wewe mwenyewe ulifika zaidi ya mara moja kuja kuniona, nakushukuru sana pamoja na timu yako. Nawashukuru sana Wabunge wote kwa jinsi ambavyo mlifika na mliniombea na leo hii nazungumza nikiwa najidai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Watanzania wote kwa sala na maombi yao. Jamani niseme hivi, kabla hujafa hujaumbika na hapa ulipo kwa sababu unatembea mshukuru Mwenyezi Mungu na utumie dini yako uendelee kumuomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, niseme tu kwamba ni watu wengi sana walifika kuniona na kunitakia kheri, siwezi kuwataja wote lakini kwa sababu ya muda mfupi na nadhani huu hutauweka kwenye zile dakika zangu kumi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kujikita kwenye hoja, leo sitaondoka hapa kwenda lhelele kuwashawishi wananchi wa Misungwi kwenda kufunga ule mtambo unaotoa maji sehemu mbalimbali kwa sababu leo nitatoa shukrani kwamba ombi langu liliSikilizwa na wananchi wa pale lhelele ambapo mradi mkubwa wa maji unatoka, sasa hivi kuna mradi lakini nitazungumzia matatizo yanayojitokeza. Hilo litakuwa zaidi katika kutoa ushauri wangu kwa Serikali yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa katika miradi hii ni muundo. Ukiangalia muundo wa namna miradi inavyoendeshwa ni *finance based*, pesa zikipatikana wanaanza kusema tutapeleka kijiji hiki, wilaya hii na wilaya hii, kitu ambacho kinasababisha sasa utekelezaji wa muda mrefu unakuwa tatizo. Nitatoa mfano mdogo tu katika Mkoa wa Mwanza na *particularly* katika Wilaya yangu ya Misungwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingi ambayo utakuta meneja wa mradi, *engineer* wa mradi na vitu kama hivyo, yote haya yapo katika utawala wakati ambapo miradi hii ingekuwa *consolidated* halafu kukawa na *individuals* ambao wanasi mamia miradi *in particular*, mambo ya Afisa Utumishi na Meneja wa Mradi yote yasingekuwepo. Kungekuwa na Meneja wa Mradi ambaye ni mkubwa kiwilaya au kimkoa lakini waone namna ambavyo kutakuwa na muundo mzuri.

Mheshimiwa Spika, nichukulie mfano wa Mkoa wa Mwanza. Kuna mradi wa Ukerewe, kuna mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Kwimba kupitia kwa ndugu yangu Mheshimiwa Ndassa na kuna mradi wa maji wa Misungwi; Misungwi tuna miradi minne na kila mradi una meneja, hii yote ni gherama matokeo yake sasa wakishaondoka pale uendeshaji unakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, nichukulie mfano pale Wilayani Misungwi kuna mashine nzuri sana zinazopeleka maji Ukiliguru lakini *customer base* ya Ukiliguru ni watu wachache. Waki-pump maji kwa wiki mbili, bili ya umeme kwa mwezi inakuja shilingi milioni 10, shilingi milioni 10 zitalipwa na watu 200 wanaokaa Ukiliguru?

Mheshimiwa Spika, halafu siyo tu hapo katika Wilaya yangu, kuna mradi sasa wa Wilaya unaotoa maji Nyahiti kupeleka Misungwi, huo nao ni mradi. Kuna mradi huu ambao sasa hivi unaitwa mradi wa kupiga kelele Kitwanga Bungeni unaotoa maji lhelele kuja Mbalika mpaka kufika Misasi, huo nao ni mradi unajitegemea. Sasa hivi mradi huo una matatizo, baadhi ya wakandarasi hawajalipwa na naomba tukishatoka hapa tuweze kuzungumza na wenzangu wa Wizara waweze kuniambia wamefikia wapi kuwalipa wakandarasi. Mheshimiwa Waziri nakushukuru ulifika katika Wilaya yetu ukaweza kuahidi kwamba pesa zitatolewa lakini mpaka sasa hivi hazijafika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, tujaribu kuona katika Wilaya tuweke mfumo unaoeleweka, mfumo wa Dar es Salaam na maeneo yanayoizunguka ulivyowekwa, huo ndio *the best*. Sijui ni *DAWASA* sijui nini ile ya Dar es Salaam inahudumia Dar es Salaam, Bagamoyo na sehemu kubwa zinazoeleweka na kuna mpangilio. Je, kuna tatizo gani kwa Mkoa wa Mwanza kuwa na *institution* moja na hizi zingine zilizopo kwenye Wilaya zikawa *subsidiary* za *institution* hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunamsifia sana Mheshimiwa Eng. Sanga kwa Mkoa wetu wa Mwanza kweli anafanya kazisana.

Ukienda pale Misungwi ukiuliza hamna jibu, ukienda Ukiliguru hamna jibu, unakwenda kwa Sanga ndiyo anaanza kukuelezea, aah, mimi pale sina mamlaka jaribu kumuomba Waziri kama naweza kupewa nguvu, kwa nini asiwe na nguvu siku zote? Kwa sababu kama tungekuwa na *institution* moja kwa Mkoa wa Mwanza zile za Misungwi, Sengerema na Ukerewe zikawa *subsidiary* ya hiyo *MWAUWASA* tungeweza kuwa na sehemu moja inayosimamia miradi yote na hii mipangilio yote ingekuwa mizuri zaidi. Sasa nyie mkipata pesa mnaanzisha mradi na unakuwa unajitegemea, mkishaondoka kwenye mradi hamna mwendeshaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa imefikia mpaka kwenye kata, Kata ya Fera wana mashine pale wana-*pump* maji lakini *customer base* ya Kata ya Fera ni wanakijiji. Sasa wanakijiji wataweza kweli kulipia bili ya umeme waweze ku-*pump* maji kila siku? Mimi nadhani hapa kidogo tuna tatizo, miradi hili isiwe *finance based*, iwe na *organization* zinazojitegemea na pesa zinazofika mnasema kwamba leo hii tunaweka pesa eneo hili na inasimamiwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Muda umeisha?

SPIKA: Ndiyo, umeisha.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Eeh, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana. Muda *washiraga*.

Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Muda umeisha?

SPIKA: Ndiyo, umeisha.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Heehee! Naunga mkono hoja. (Kicheko)

SPIKA: Ahsante sana. Muda washiraga.

Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia Wizara ya Maji. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja nyingi ambazo zinaendelea kutolewa, lakini leo ntajikita kwenye hoja mbili, hoja ya kwanza ntatoa sababu za kuwaondolea wasiwasi wale wanaofikiri kwamba tukiongeza shilingi 50 kwenye mafuta petroli na dizeli kwamba inaweza ikasababisha mfumuko wa bei kuongezeka. Na jambo la pili ntakalozungumzia kwa ufupi, ntazungumzia hoja inayohusiana na *Stiegler's Gorge*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na hoja ya kwanza; wale ambao wanafikiri tukiongeza shilingi 50 kwenye lita ya mafuta ya dezeli au ya petroli itaongeza mfumuko wa bei, nataka nitoe sababu zifuatazo kuwaondolea wasiwasi kwamba hilo halitatokea. Sababu ya kwanza hii shilingi 100 au shilingi 50 ambayo tunataka iwe shilingi 100 sasa, hii kodi kitaalam tunaita *specific* sio *Ad valorem*, na mchumi yejote duniani ukimuuliza atakwambia kama ni *specific* maana yake haibadilikibadiliki, kama thamani ya kitu fulani inapanda au kushuka kodi yenyehe haibadiliki.

Mheshimiwa Spika, sasa hii tunasema shilingi 100, hii shilingi 100 bei ya dunia huko ya mafuta ipande ishuke, bei

ya mafuta hapa Tanzania ipande ishuke, hiyo haibadilishi hiyo shilingi mia. Kwa hiyo, ntapenda yule atakayekuja kusema itabadiili ka anieleze yeye uchumi anaousema alisomea wapi na anatumia *reference* ya wataalam gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, mfumuko wetu tunaouzungumza saa hizi ni wastani wa asilimia 3.1 mpaka Machi kwa takwimu za *BOT*, lakini *BOT* lengo lake ambalo wameliweka ni kwamba mfumuko wa bei usizidi asilimia tano, hilo ndilo lengo la *BOT*. Sasa kama lengo la *BOT* ambalo ndiyo lengo la Serikali pia ni asilimia tano tusivuke lakini saa hizi mfumuko wa bei ni asilimia 3.1, huu wasiwasi unatoka wapi wa kusema huu mfumuko wa bei utapanda. Ukipanda acha upande tu, sana sana ukipanda utaenda mpaka asilimia 3.5, itakwenda nne, hata ukifika tano uache tu ufike tano, kwani tatizo ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu ni kwamba ndani ya Afrika Mashariki tumekubaliana kitu kinaitwa *convergence rate*, tumlichokubaliana ndani ya Afrika Mashariki ni kwamba nchi zote za Afrika Mashariki zihakikishe mifumuko yao ya bei haizidi asilimia nane. Sasa kama hiyo ndiyo ya Afrika Mashariki tuliyokubaliana tusizidi asilimia nane, sisi tuko asilimia 3.1, huu wasiwasi unatoka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi kwa nini mfumuko wa bei unaweza ukapanda, unaweza ukapanda ama kwa sababu ya kuongezeka sana kwa *aggregate demand* au unaweza ukapanda kwa sababu ya *cost push*, gharama zinaongezeka, lakini hivi kama unasema unaweza ukapanda kwa *aggregate demand* ikapanda maana yake ni nini; maana yake ni kwamba watu wanakuwa na *disposable income* kubwa, watu wakiwa na *disposable income* kubwa kipato kikipanda sana wanaweza wakawa na nia ya kutumia sana.

Sasa unapoongeza kodi kwenye mafuta hauongezi *disposable income* bali unalenga kupunguza *disposable income*, sasa wasiwasi huu unatoa wapi kama uchumi hivyo ndivyo unavyotueleza na ndivyo ulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine, *EWURA* ni chombo ambacho kinafanya kazi nzuri. Mara kwa mara wamekuwa wakitoa takwimu na wanachapisha kwenye magazeti yote, na tunasoma tunaona, na mara nyingi saa nyingine kulingana na mwenendo wa bei duniani wanasesma sasa *cape itapanda* wanaweka *cape inapanda* kidogo; saa nyingine shilingi 50, saa nyingine 100 saa nyingine inashuka, lakini siku zote *EWURA* walipopandisha hiyo mfumuko wa bei haukupanda kwa sababu mafuta yamepanda kwa shilingi 50 au shilingi 100. Hata waliposhusha mfumuko wa bei haukushuka kwa sababu wameshusha, kwa maana hiyo kuna vitu vingine vya kuangalia vinavyoweza kusababisha mfumuko wa bei upande au usishuke. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine kwa nini nina uhakika haitatokea kama tunavyofikiri; mfumuko wetu wa bei takwimu zinaonesha unachangiwa zaidi na chakula. Sehemu kubwa tunayoangalia ni chakula, sasa kama takwimu tulizonazo kila siku tunaambiwa tuna *surplus* ya uzalishaji wa chakula ndani ya nchi, wasiwasi huo unatoka wapi tena ya kwamba gharama hizi zitapanda tukiongeza? Kwa sababu sehemu ya kuangalia kwa makini na kwa wasiwasi ni sehemu tu ya ule mfumuko wa chakula usije ukapanda.

Mheshimiwa Spika, wachumi huwa wanaangalia mambo kwa macho mengi, lakini naomba niwaambie sio siku zote kwamba mfumuko wa bei ni jambo baya, hata mfumuko wa bei ukipanda kidogo si jambo baya, na mfumuko wa bei kupanda kwenye uchumi unatakiwa. Tatizo ni watu waliosoma vitabu vile vinavyowafundisha tu kwamba mfumuko wa bei ni mbaya, si kweli, mfumuko wa bei na wenyewe unatakiwa kwenye uchumi kwa sababu ukiporomoka zaidi, ukiwa *negative*, ni tatizo pia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niliseme la mwisho; mfumuko wa bei pia unaangalia na *interest rates*. Kinachotakiwa siku zote mfumuko wa bei usiwe juu ya *interest rates*. *Average* ya *interest* Tanzania ni asilimia 8.3; sasa huu wasiwasi wa mfumuko wa bei unatoka wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nichangie tu kwa ufupi kuhusu *Stiegler's Gorge*; ni mradi mzuri sana, lakini mnakumbuka tulikuwa tuna Sheria Na. 5 ya mwaka 1975 ambayo tulifuta nadhani humu Bungeni kwa sababu tulifuta ile Sheria ya RUBADA, sasa *Stiegler's Gorge* ni mradi mzuri na pale tutaweka trilioni 6.3.

Mheshimiwa Spika, ningeomba itungwe sheria ya kulinda mradi ule kwa sababu bila kuwa na sheria maalum ya kulinda ile *Stiegler's Gorge* kwa maana ya kulinda chanzo cha maji, tusipokuwa makini tutawekeza hela nydingi halafu baada ya muda maji hayatakuwepo. Kuna sababu ya kuja na sheria maalum ya kulinda ule mradi, ya kulinda vyanzo vya maji. Hili jambo tunaweza tukafikiri si muhimu lakini nadhani lazima tuanze kufikiria sasa na lazima tuchunge sheria hiyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala kwa kuamua kutushushia sasa *theories* za uchumi. Haya anayepinga aje sasa na yeye na *theories* zake.

Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia kwenye hotuba hii muhimu sana ya jambo muhimu sana la maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuipongeza Wizara; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu na wataalam wote wa Wizara kwamba pamoja na kwamba bado changamoto ya maji ni kubwa, lakini kuna kazi kubwa ambayo inaonekana inafanyika kwa hiyo nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha uliopita kwa maana ya 2017/2018, Halmashauri yangu ya Nzega DC

kupitia Mpango wa *Water Sector Development Programme (WSDP)* ilipata karibu *one billion* ya kutekeleza miradi ya maji. Kwa hiyo, pale halmashauri sisi tulifanya usanifu tuka-*engage* wakandarasi wa miradi mikubwa mitatu ya visima virefu, lakini tangu wakati huo tulikuwa hatujapata *go ahead* ya Wizara ya kuwaruhusu wakandarasi wale waanze sasa kufanya kazi. Tulifuatilia, niliwasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri na naipongeza Wizara kwamba sasa hivi, muda mfupi tu, kama mwezi mmoja uliopita, Wizara imetoa *go-ahead* ili wakandarasi wale sasa waanze kutekeleza ile miradi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kilichotokea hapa ni kwamba wakandarasi wale tuliwa-*engage* mwaka wa fedha uliopita mwezi Juni, 2018 na karibu mwaka sasa umekaribia kuisha, kwa hiyo wakandarasi wale sasa hivi wanaomba *review* ya mikataba kwa sababu wanadai kwamba bei za vitu zitakuwa zimebadilika na vitu kama hivyo. Sasa rai yangu kwa Wizara ni kwamba kwa sababu Wizara wamechelewesha huo mchakato, kwamba badiliko lolote ambalo litatokea kwa maana ya bei basi Wizara iwe tayari kuli-*accommodate* ili fedha ziweze kutosha na miradi ile ifanyike. Kwa sababu ni kweli tuliwa-*engage* mwaka sasa umepita na huenda kweli baadhi ya bei zimebadilika.

Mheshimiwa Spika, angalizo lingine ni kwamba kwenye kitabu cha Wizara ya Maji mwaka huu halmashauri yangu imepangiwa shilingi milioni 620 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya maji. Kwa hiyo, hofu yangu ni kwamba isije ikawa hizi milioni 620 za mwaka huu zikatumika kulipia ujenzi wa miundombinu ya hii miradi ya mwaka wa fedha uliopita. Ninaomba Wizara wawe makini kwamba hizi milioni 620 zilizopangwa zilizo kwenye kitabu hiki zitumike kwa ajili ya miradi mipya, miundombinu mipya itakayojengwa na wala zisije zikatumika tena kwa miradi hii ya mwaka wa fedha uliopita kwa sababu hii ilikuwa na fedha zake na hizo fedha zake ndiyo zitumike.

Mheshimiwa Spika, kama ni kuchelewesha ni Wizara ilichelewesha na ninaamini kwa sababu fedha ziliwuwa zinatoka Wizarani basi wanazo kule na zilezile ndiyo zitekeleze

hii miradi ya nyuma na hizi milioni 620 zitekeleze miradi mipyä ambayo tutaisanifu kwa ajili ya mwaka huu wa fedha unoaoanza mwezi Julai unaokuja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu mradi wa Ziwa Victoria; nimeona kwenye kitabu cha bajeti zimetengwa milioni 500 za ndani lakini na bilioni 23 za nje kwa ajili ya kutekeleza mradi huu wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyafikisha Tabora Mjini na Igunga kupitia Nzega. Tulilalamika kwamba usanifu wa mwanzo wa mradi huu uliruka baadhi vijiji lakini naipongeza Wizara kwa sababu imelizingatia hili, vile vijiji vilivyorukwa vimeingizwa kwenye usanifu lakini tatizo ni kwamba baada ya kuingizwa vijiji hivi vingi vimepewa gati moja tu au magati mawili.

Mheshimiwa Spika, vile vijiji nya zamani vilivyokuwemo kwenye usanifu wa zamani unakuta kijiji kama kina vitongoji saba kimepewa magati saba, kama kijiji kina vitongoji nane kimepewa magati nane, lakini hivi vilivyorukwa ambavyo sasa vimeingizwa unakuta kijiji kimepewa gati moja, sasa unakuta kijiji kina vitongoji nane lakini kimepewa gati moja tu, maana yake ni kitongoji kimoja tu ndiyo kitapata maji. Kwa hiyo hofu yangu ni kwamba tukiacha hivi ilivyo badala ya kuona kwamba wananchi wamepelekewa maji kitakachotokea ni malalamiko makubwa kwa sababu vile vitongoji vingine vyote vitakuwa havijapata maji na tutakuwa hatujafikia lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ushauri au ombi langu hapa ni kwamba hivi vijiji ambavyo vilikuwa vimerukwa na sasa vimeingizwa na vyenyewe vipatiwe idadi ya magati kama vile vijiji nya mwanzo kulingana na vitongoji ambavyo viko kwenye vijiji husika. Vijiji ambavyo vilikuwa vimerukwa ni Ilagaja, Bulambuka, Isalalo, Mizibaziba, Mwamalulu, Mabisilo, Mihami, Ilela Mhina, Kiloleni na Kipugala. Vijiji hivi vipatiwe magati ya kutosha ili kwa kweli waweze kufurahia na wao maji ya kutoka Ziwa Victoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, tulifanya ziara na katika

ziara yetu tulifanya ukaguzi wa miradi ya maji, miradi mingi ilikuwa ni ya maji, hasa ya vijijini. Nashauri maeneo ya vijijini Wizara jie na mwongozo kwamba usanifu wa miradi ya maji ya vijijini basi usanifiwe kwa namna ambayo utaendeshwa kwa pampu zitakazotumia umeme wa juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vijijini hizi pampu za dizeli zina gharama kubwa na unakuta watumia maji wa vijijini wameshindwa kabisa kuendesha miradi hii na hata kunufaika na hayo maji kwa sababu maji yamewafikia, wameyapata, lakini gharama zinakuwa kubwa na kuna vijiji vingine mradi hautumiki kabisa kwa sababu wananchi wameshindwa. Mimi kwangu kule nina Miradi wa Mahene, Nawa, Buhondo, Sojo, Ikindwa, ni miradi mikubwa, mirefu, inafanya kazi lakini hata bei ya shilingi 100, 200 kwa ndoo wananchi kule vijijini bado wanausuasua kuweza kuimudu. Kwa hiyo napendekeza kwamba usanifu wa miradi ya maji ya vijijini usanifiwe kwa namna ambavyo itaendeshwa kwa pampu za umeme wa juu badala ya dizeli, dizeli bado ni gharama na wananchi wanashindwa kuimudu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine ni kwamba maeneo mengi ya vijijini tu-focus kwenye visima vifupi badala ya virefu kwa sababu kisima kirefu kimoja ambacho kinagharimu milioni 300, 400 unaweza ukapata visima zaidi ya kumi, 15 vifupi. Kwa hiyo katika maeneo mengi ya vijijini, kwa mfano kule kwangu nime-experience, ukijenga kisima kirefu unanufaisha kijiji kimoja unatumia milioni 400, milioni 400 hizo hizo ukisanifu visima vifupi vya pampu ya mkono unapata visima kumi mpaka 15 na eneo ambalo unahudumia linakuwa pana kwa maana ya vitongoji na vijiji vingi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile gharama ya kuendesha pampu ya mkono kwa wananchi wetu wa vijijini ni nafuu haihitaji fedha kulikoni kisima kirefu ambacho kinahitaji fedha za dizeli na kuendesha. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba visima vya vijijini visanifiwe kwa...

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Zedi. Mheshimiwa Chikota, atafuata na Mheshimiwa Mussa Ntimizi na Mheshimiwa Kiza Mayeye ajiandae.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ilio mbele yetu, hotuba ya Wizara ya Maji, hoja ambayo ni muhimu na ni yeti kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nianze kuwapongeza viongozi wa Wizara hii; nianze kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Mbarawa; nimpongeze Naibu wake, Mheshimiwa Aweso; nimpongeze Katibu Mkuu, Prof. Kitila Mkumbo na Naibu Katibu Mkuu *Eng. Kalobeloo*; wakurugenzi wa Wizara pamoja na watendaji wa maji katika ngazi mbalimbali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na mikoa. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na kazi wanazozifanya zinaonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ulikuja kukagua mradi wetu wa Chawi, ulifanya kazi kubwa ulizunguka mpaka Nanyamba, Mheshimiwa Aweso ultatua changamoto kubwa ya mradi ambaa ulikuwa unatekelezwa Nanyamba, unasimamiwa na Mtwara Vijijini, baada ya kikao chako kifupi ulitoa suluhisho la changamoto ile.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru kwa miaka miwili mfululizo mlikuwa mnatenga fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya maji ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, nawashukuru sana. Lakini kipekee niwashukuru hivi karibuni mmetoa kibali kwa ajili ya ujenzi wa visima kumi. Kwa hiyo. nichukue nafasi hii Mheshimiwa Waziri nikushukuru kwa jinsi unavyotoa jicho la kipekee kwa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa kuhusu Mradi wa Maji wa Makonde; mradi huu ni wa siku nyingi na upo katika

ile miji 28, na mradi huu katika eneo letu utahudumia Mamlaka za Serikali za Mitaa zisizopungua nne na majimbo kama matano. Mradi huu ni wa siku nyingi na unahitaji kujengwa upya. Sasa Mheshimiwa Waziri nikukumbushe tu kwamba tulishawasilisha andiko Wizarani kwako na ulipofika pale Chawi uliahidi kwamba hakuna Mtanzania atakayekosa maji kwa sababu ya gharama.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni wa siku nyingi na unahitajika kujengwa upya. Sasa Mheshimiwa Waziri nikukumbushe tu kwamba tulishawasilisha andiko Wizarani kwako na ulipofika pale Chawi, uliahidi kwamba hakuna Mtanzania atakayekosa maji kwa sababu ya gharama. Nanyamba andiko letu ni kutoa maji Mitema na kupeleka Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, mradi ambao unahuishisha kata tisa, mitaa tisa na vijiji 34. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watendaji waliniyahidi kwamba tutaingiza kwenye utekelezaji wa fedha za mkopo wa Serikali ya India hata kama hawajatoa maandishi kwa Mkurugenzi wetu, lakini kauli ya Waziri, kauli ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu tunaiamini. Rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba Serikali inafanya kazi kwa maandishi. Naomba mtoe andiko mumpelekee

Meneja wa Mradi wa Makonde ili wakati wa utekelezaji asione kwamba ni *annex* aone kwamba ni *component* muhimu katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu kama nilivyosema unahuishisha vijiji 34 na mitaa tisa; kwangu wananchi wanaopata maji ni asilimia 45, lakini mradi huu ukitekelezwa, tutafikia asilimia 85. Kwa hiyo, naomba *component* hii ya kutoa maji Mitema kupeleka Nanyamba isisahauliwe na aandikiwe barua Meneja wa Mradi ili wakati wa utekelezaji basi isiwe *annex* iwe ni sehemu ya mradi wa Makonde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichangie mradi wa maji wa kutoa Mto Ruvuma na kupeleka Mtwara Manispaa. Wachangiaji waliopita wamezungumzia mradi huu lakini naamini kwa

sababu chanzo cha maji kipo Jimboni kwangu Mahembe Chini, naomba sasa mradi huu utekelezwe, ni mradi wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kuna kauli mbili Wizarani, kuna kauli ya kutekeleza mradi huu, lakini kuna maneno ya chini chini kwamba mradi huu siyo *viable* kwa hiyo, hautatekelezeka. Kwa hiyo, naomba wawe wazi tuambibiwe kama mradi unatekelezwa au autekelezwi. Wananchi wa Mtwara wanataka maji *whetherwanatoa* Ziwa Victoria kupeleka Mtwara au Mto Ruvuma, tunachotaka ni maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama mradi unatekelezwa tuambibiwe kwamba mradi unatekelezwa; na kama kuna mabadiliko ambayo yameonekana kwamba kwa Wizara kutekeleza mradi huu kuna ghamama ambazo siyo za lazima, basi mtuambie. Wanachohitaji wananchi wa Mtwara, Nanyamba na sehemu ya Mtwara Vijiji ambapo linapita bomba hili, wajulishwe ili na wao wawewe kufahamu na pia ili miradi inayotayarishwa na Mamlaka ya Serikali ya za Mitaa iweze kujumuisha maeneo haya ambayo hapo awali tuliacha kwa sababu kuna mradi mkubwa wa kutoa maji Mahembe Chini, yaani Mto Ruvuma na kupeleka Manispaa ya Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 106 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri unazungumzia changamoto za utekelezaji wa miradi ya maji. Hapa changamoto ya kwanza amesema upatikanaji mdogo wa fedha za kutekeleza miradi. Naungana na wale wanaosema tuongeze shilingi 50/= ili tupate fedha za kutosha za kutekeleza miradi yetu ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna haja ya kuwa na wasiwasi. Professor amesema kwenye kitabu chake kwamba kuna changamoto ya fedha na isije tukawalaumu baadaye kwamba Mheshimiwa Prof. Mbarawa alishindwa, kumbe siyo kwamba alishindwa, hakuvezeshwa, hakupewa fedha za kutosha. Kwa hiyo, tuwape fedha za kutosha ili Waziri, Naibu

Waziri, Katibu Mkuu na watendaji waweze kutekeleza miradi ya maji kama walivyojipangia. Tusipofanya hivyo, tutawalaamu kwa makosa ambayo siyo ya kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa Mheshimiwa Waziri ameweuka wazi kwamba fedha za maendeleo hadi Aprili amepata asilimia silimia 53, fedha za uhakika ni za Mfuko wa Maji, wenyewe kufanya maamuzi ni sisi. Mheshimiwa Chenge amesema vizuri kwamba kuna Azimio la Bunge. Kwa hiyo, tuliunge mkono Azimio la Bunge, Wizara hii ipate fedha ili itekeleze miradi ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye llani ya Chama chetu cha Mapinduzi inasema tutatekeleza miradi ya maji kwa asilimia 85 ifikapo 2020. Bila kuwaongeza fedha tutakuwa na maswali magumu sana mwakani. Hii ni Mei sasa hivi, 2020 siyo mbali. Tuwape fedha ili wakatekeleze miradi ya maji ili 2020 tusipate kazi ya kuzungumza maneno marefu majukwaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho unahusu mabadiliko ambayo tumeyafanya hivi karibuni kuhusu sheria Na. 5 ya 2019 kuhusu Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira. tunaazisha *RUWASA*, ushauri wangu kwa Wizara, hebu tufanye matayarisho ya kutosha ili chombo hiki kipyta tunachokianzisha kianze kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina hadhi tofauti. Tumeona pale tulipoanzisha *TARURA*, tuliwaambia kwamba Mhandisi wa Maji aende kule na gari yake. Ukitamka hivyo, Meneja wa *RUWASA* wa Nanyamba hatakuwa na gari, kwa sababu *so far* Nanyamba haina gari ya maji. Kwa hiyo, ukisema atumie gari ambayo alikuwa anatumia Halmashauri, Meneja yule ameanza kazi kwa kufeli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba matayarisho ya kutosha yafanywe ili *RUWASA* atakapoanza, Meneja wa *RUWASA* wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa awe na rasilimali za kutosha. Kwanza apate ofisi, awe na rasilimali za kutosha,

awe na vitendea kazi na aanze kwa kujiamini na siyo kuwa omba omba wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, rai yangu kwa Wizara, tufanye maandalizi ya kutosha. Sheria tumeitunga vizuri, lakini tusipofanya maandalizi ya kutosha tutaanza kuilaumu *RUWASA* wakati hatujawapa rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Abdallah Chikota kwa mchango wako mzuri. Nilishamtaja Mheshimiwa Mussa Ntimizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kiza Mayeye na Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae.

MHE. MUSSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Maji, Wizara Muhimu sana katika maisha ya wananchi wenzenetu na sisi wenyewe hapa tulipo. Nianze kwa kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Profesa. Mbarawa, mdogo wangu Mheshimiwa Aweso na Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara pamoja na changamoto nyingi zilizopo za upatikanaji wa maji nchini, ikiwemo pia na changamoto ya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kushukuru kwa mradi wa maji wa Kijiji cha Igala, nimeona imetengwa shilingi milioni 76 hapa za kwenda kumalizia kumlipa mkandarasi aliyefanya kazi katika Kijiji cha Igala. Kwa kweli nashukuru sana Wizara kwa kazi kubwa iliyo fanyika pale.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko, lakini mwishoni nitachangia. La kwanza, mradi wa Ziwa Victoria unakuja katika Mkoa wa Tabora, unakwenda katika Majimbo yote ya Mkoa wa Tabora kasoro Jimbo la Igala. Hili nimekuwa nalisema sana na nimekuwa nikahidiwa kwamba kuna miradi mingine mbadala itakuja lakini pia nimeahidiwa kwamba Jimbo la Igala itaingizwa katika awamu ya pili ya mradi wa maji wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na subira hiyo, lakini pia Mheshimiwa Rais amekuja Igalula katika Kata ya Kigwa akaahidi kwamba maji ya Ziwa Victoria yatakuja. Nasikitika kwamba nimeona pia kuna mradi tena wa miji 29 na bado Jimbo la Igalula halijaangaliwa. Miji ambayo tayari inapelekewa maji ya Ziwa Victoria tena karibu na Jimbo langu imewekwa tena katika miji 29 kwenda kuwekewa miradi mingine ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Igalula nimejaribu kupitia sijaona mradi hata mmoja ambao unakuja kusaidia kutatua kero ya maji katika Jimbo la Igalula. Bado katika mgao wa fedha za Halmashauri kwenda kusaidia utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo yetu, ukiangalia Wilaya yetu ya Uyui, tuna Majimbo mawili; Tabora Kaskazini kwa Mheshimiwa Almasi Maige na Jimboni kwangu; tumepata fedha takribani shilingi millioni 500 tu, lakini kuna Majimbo ambayo yanapita maji ya Ziwa Victoria, yana Jimbo moja, wanapata zaidi ya shilingi milioni 800. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba yamefanyika makosa, lakini tuangalie, Jimbo la Igalula maji hayaendi, fedha tunazotengewa ni ndogo, miradi hii itatekelezwa namna gani? Mheshimiwa Nailbu Waziri alikuja Tabora, Igalula tukamweleza, kuna vyanzo vya maji viwili vimepatikana katika Kata ya Loya na Tura. Usanifu umefanyika, namshukuru Katibu Mkuu alinisaidia; katika Kata ya Loya usanifu ulishafanyika, *documents* ziko Wizarani kwenu, lakini hakuna chochote kilichoandikwa katika kitabu cha bajeti kuhusiana na mradi wa maji wa Loya na kuhusiana na mradi wa maji wa Tura.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie, tanki kubwa la maji linalopeleka maji Manispaa, linalopeleka maji Sikonge na Urambo linajengwa kilomita 15 toka Jimboni kwangu Igalula. Wananchi wanaona tenki linatengenezwa pale, maji Igalula hayaji, *this is not fair at all*. Wananchi wanasikitika lakini kabisa hatutendewi haki. Kilomita chini ya 15 tenki kubwa linajengwa lakini wananchi hawapati maji. Mheshimiwa Waziri, naomba hili tuliangalie sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka pia nizungumzie mgawanyo wa fedha hizi ndogo ambazo nimejaribu kusema hapa; ukiangalia ukurasa wa 129, ukurasa wa 148, tazama na ukurasa wa 147, kuna maeneo wanafaidika na maji ya Ziwa Victoria yanakwenda. Miradi zaidi ya mitatu inazungumzwa katika kitabu hiki inakwenda Jimbo jirani na kwangu, wananchi wangu wanapata taarifa hizi. Inaonekana sisi hatufanyi kazi. Inaonekana wananchi wangu wamesahaulika kwenye suala la maji. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tuangalie maeneo ambayo yana matatizo ya maji tuweze kupeleka hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, nami nizungumzie suala la kuongeza fedha katika Mfuko wa Maji ili miradi hii iende. Nimeanza kuzungumzia changamoto za Igalula kwa kifupi tu; lakini miaka yote mitatu tuko hapa, nimekuwa nazungumzia uwezekano wa Serikali kuongeza shillingi 50/= ili ziende kwenye Mfuko wa Maji ziweze kutusaidia sisi wenye matatizo ya maji katika maeneo yetu. Utamu wa ngoma uingie ucheze. Kwa sisi tunaotoka vijijini, unapozungumzia suala la maji, ukamwambia mwananchi eti tukiongeza shillingi 50/= kutakuwa kuna *inflation*, hawezi kukuelewa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hivi *effect* za *inflation* kwa wananchi wetu wa Igalula na *effect* za kukosa maji, zipo tatizo ni kubwa sana kwa wananchi wetu? Kukosa maji ni tatizo kubwa sana. Ikiiongezwa shillingi 50/= shida yake watakayopata wananchi wetu ni ndogo kuliko wananchi kuendelea kukosa maji kwa sababu eti ya shillingi 50/=. Kama alivyosema Mheshimiwa Chenge, nami nataka nimuunge mkono Mheshimiwa Chenge. Alichosema ndugu yetu Musukuma ni cha msingi, Mheshimiwa Waziri safisha Wizara yako, miradi inaonekana ina thamani kubwa haiishi, lakini haina manufaa kwa wananchi wetu. Kisima kimoja kinachimbwa kwa shillingi milioni 45, lakini utafiti tuliofanya kisima kinachimbwa kwa shillingi milioni 20 na wananchi wanaweza kupata maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo katika Wizara, tunaomba Mheshimiwa Waziri asafishe Wizara yake ili hizi

fedha tunazomwidhinishia hapa, ziende zikalete matokeo kwa wananchi wetu ambao wana matatizo makubwa sana. Pamoja na matatizo yaliyopo katika Wizara yake, sisi Wabunge kazi yetu ni kumpitishia fedha, kumpatia fedha ili miradi iende. Hatuwezi kuacha kumwongezea fedha eti kwa sababu kuna ubadhirifu katika Wizara yake. Wizara yake ikisafishwa, hizi fedha zikienda wananchi wetu watanufaika kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, hili suala la kusafisha Wizara halihitaji kuchukua miezi miwili au mitatu. Tunajua Mheshimiwa Waziri amezianza juhudhi, lakini zifanyike haraka sana ili mwisho wa siku hizi fedha tunazozipitisha hapa zikalete matokeo chanya kwa wananchi wetu na siyo kingine ni kupata maji kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unaweza kuona hapa Wabunge wote watakaosimama, wanachokihitaji wao ni maji. Suala la kwamba unapata wapi fedha, tuachie sisi. Tutasimamia Azimio letu la shilingi 50/= ili uweze kuongezewa fedha za Mfuko wa Maji. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, shida ya maji inatukuta sisi sote, kwa hili tusimamie Azimio letu, ule upungufu tumwachie Mheshimiwa Waziri akayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, hapa Jumatatu hakitaeleweka mpaka shilingi 50/= iongezwe. Wananchi wa Igalula wanataka maji, tunajua hatuwezi kuzungumza kupata maji bila kupata rasilimali fedha. Hii fedha tutasimamia aipate, lakini tukiipata maji yasipopatikana, sasa Mheshimiwa Waziri huo mzigo utakuwa ni wa kwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo nilitaka niseme hayo, lakini naomba Mheshimiwa Waziri aangalie mgao wa fedha unaokuja katika mikoa yetu, aangalie changamoto zilizopo. Kwa sababu Igalula tuna changamoto tofauti na Sikonge na maeneo mengine. Mgao wa fedha uje, miradi ambayo tumeshaifanya usanifu iletewe fedha ili iweze kutusaidia kutekeleza miradi tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini Jumatatu hakieleweki hapa mpaka shilingi 50/= iweze kupitishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Ntimizi. Sasa nakuita Mheshimiwa Kiza Mayeye na Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya maji. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya na kuweza kusimama mchana huu wa leo. Kipekee kabisa niungane na wewe katika kuwapa pole Watanzania na wanafamilia wote kwa kuondokewa na mzee wetu, Mzee Mengi na Mungu amlaze mahali pema Peponi, amen.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri, na jopo lote la maji kwa kazi ambayo wamekuwa wakiifanya katika kuwasaidia wananchi suala la maji. Ni ukweli usiopingika kwamba changamoto ya maji bado ni kubwa katika maeneo mengi ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nzungumzie suala la Kigoma, kwa sababu tunasema *charity begins at home*. Sasa nami nianze kuwapigania wananchi wa Kigoma ingawa changamoto ya maji ni Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ambayo natokea ya Kigoma *DC*, tuna miradi miwili ya maji; tuna Mkongolo I, tuna Mkongolo II. Miradi hii imeachwa, imetelekezwu, miundombinu ni mibovu. Pia miradi hii inahudumia zaidi ya watu 50,000 Vijiji vya Mwandiga, Bitale, Mkongolo, Nkungwe, Kiganza na maeneo mengine ya Kigoma *DC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kigoma tunateseka, hatuna maji. Leo nimefikisha miaka 30, lakini mama zangu

wanabeba maji kuanzia sijazaliwa mpaka sasa. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri wasaidieni wamama wa Kigoma. Kama kweli tunasema ni Serikali ya wanyonge, kama kweli tunataka kumtua mama ndoo kichwani, tuwasaidie akina mama ambao nywele zimeisha katikati kwa sababu ya kubeba ya ndoo ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Kijiji cha Mwandiga. Hapo Mwandiga kuna Mzee mmoja anaitwa Mzee Sheni, ni Mhindi. Huyu amechimba kisima, anawasaidia watu hawa wa hapo, ndoo shilingi 100/=. Sasa leo tunaposema kwamba mtu kama huyu atoe tozo kwa sababu ya kuchimba kisima, sidhani kama tunamtendea haki. Kwanza amewasaidia wananchi, ambao kwa miaka zaidi ya 30 tunatumia maji ambayo siyo safi na salama. Mwandiga tumekuwa ni kinara wa ugongwa wa kipindupindu kwa sababu hatuna maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba tozo hii kwa sababu ya kuchimba visima, iweze kuondolewa. Kaka yangu, Mheshimiwa Nape alielezea vizuri kwamba hawa ambao wanaiza maji labda haya ya kunywa ambayo wanafunga kwenye makatoni, sawa; lakini hawa ambao wanachimba visima kwa sababu ya kuwasaidia wananchi, kama tutawatoza tozo, kiukweli hatuwatendei haki. Kwanza wanawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, yuko mwengine amechimba nyumbani kwake kwa sababu ya matumizi yake binafsi. Hailengii akilini tunapomwambia atoe shilingi 700,000/=, atoe kiasi cha fedha kwa sababu ya kuchimba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongezee suala lingine katika Mkoa wa Kigoma. Nashukuru katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri amesema kuna mradi wa Ziwa Tanganyika Naomba sana huu mradi utekelezwe na ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuna maji ambayo yako katika Manispaa ya Kigoma

Mjini kwa kaka yangu Mheshimiwa Zitto, lakini haya maji yanakuja yanaishia katika mpaka wa Mwandiga na Kigoma Mjini ambako panaitwa Ntovye. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, haya maji ambayo yanaishia pale yasiweze kupotea yapande katika Kijiji cha Mwandiga, yapande katika Kijiji cha Bitale na Kijiji cha Kiganza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mwaka 2018 nakumbuka niliuliza swali kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuleta maji ya Kigoma Mjini yapande mpaka Vijiji vya Mwandiga na kuendelea? Kaka yangu Mheshimiwa Aweso alinijibu akaniambia kwamba wapo kwenye mkakati. Nafahamu juhudhi ambazo zinafanywa, sasa nawaomba sana wasichelewe, tusaidieni wamama wa Mwandiga na maeneo mengine tuweze kuondokana na changamoto hii (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Nzungumzie suala lingine. Ndani ya Halmashauri ya Kigoma *DC* kuna vijiji ambavyo mpaka sasa kwenye miradi tunatumia dizeli na mafuta, kitu ambacho tunasababisha hasara kwa Serikali yetu kutokana na gharama ambayo tunatumia. Sasa katika Vijiji kwa mfano, mradi katika Kijiji Nkungwe, Kalinzi kule kwetu na Kandanga tunatumia dizeli na umeme, ni gharama kubwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kama tungepata *solar* naamini ingeweza kutusaidia na wakafanya kazi kwa ufanisi mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nisisitize, mbali na kwamba nimeongelea Kigoma, lakini bado kuna maeneo mengine hata Dar es Salaam, suala la maji ni changamoto, kwa mfano, Goba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Goba, wamekuwa wakiteseka, hakuna maji ya uhakika na ninatambua kuna mradi pale unaendelea. Sasa huu mradi ambao umekuja umeishia Kinzudi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri huu mradi uweze kusambaa katika eneo lote la Goba, wakazi wa Goba waweze kupata maji safi na salama, lakini tuondokane na kero ambayo wakazi wa Goba wamekuwa wakiipata kwa kukosa maji kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine nizungumzie changamoto ya watumishi; Kigoma suala la maji katika Idara ya Maji bado tuna changamoto ya watumishi. Niombe sanawatusaidie watumishi waongeze nguvu katika halmashauri zetu tupate Wahandisi wakutosha. Kipekee kabisa Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni na kama mtu anafanyakazi apongezwe, nampongeza Mheshimiwa Waziri, baba yangu Mbarawa anafanyakazi.

Sasa naomba Mhandisi Mkoa wa Kigoma nikijana kama mimi, anafanyakazi kwa kujituma, naomba tumuunge mkono mpaka sasa bado anakaimu, lakini amekuwa ni kinara katika kushirikiana na wananchi wa Kigoma kutatua kero mbalimbali za maji. Sasa kama anatusaidia wananchi wa Kigoma na anafanya kazi vizuri, basi Mheshimiwa Spika kipekee kabisa naomba huyu kijana aweze kupewa haki yake na asibaki kukaimu kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuongea nafikiri nitakuwa narudia ambayo wenzangu wameshaongea, naomba sana Mheshimiwa Waziri haya ambayo nimemwomba Mji wa Mwandiga tupate maji, lakini vijiji vingine ambavyo havijawahi kuona maji kabisa kwa mfano Kiziba, Kalalangabo na Matyazo hawajawahi kuona maji kwenye mabomba wala maji safi na salama. Naomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kuwasaidia watu hao wapate maji na waone faida ya kuwa na Ziwa Tanganyika katika mkoa wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kiza Mayeye, kumbe na wewe unatoka kule kule mwisho wa reli. Haya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mwandiga, Manyovu kule Kalinzi na kadhalika.

Nilishakutaja Mheshimiwa Frank na atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsantekwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Maji ni uhai na nitaanza kwanza na bajeti ambayo tulidhinisha kwaajili ya kuwapatia wananchi maji mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018/2019 tulidhinisha...

SPIKA: Mheshimiwa Kiza Mayeye unatakiwa urudi ulipokaa, rudi tena, hutakiwi ukatize kati ya anayeongea na mimi. Endelea Mheshimiwa Frank.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, tulipitisha bajeti ya shilingi bilioni 672 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata maji, lakini mpaka sasa fedha ambayo imekwenda kufanyakazi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji, imetolewa shillingi billioni 343.4.

Mheshimiwa Spika, tunajiuliza sana kama Wabunge kwa kazi ambayo tunailfanya ndani ya Bunge ya kupanga/kutengeneza bajeti lakini pia kuhakikisha kwamba tunaidhinisha bajeti hii ili wananchi wetu waweze kupata maji, lakini cha kushangaza fedha haziendi kabisa kwenda kutekeleza shughuli za maji. Nataka nitoe mfano tu katika bajeti hii ya bilioni 672, kuna fedha karibuni shilingi billioni 185, hizi fedha zilikuwa zinatokana na fedha za mchango wa wananchi kwenye mafuta ya petroli na dizeli, lakini pia kulikuwa na fedha karibuni shilingi billioni 229.9, hii ni fedha ambayo ilikuwa inatoka kwa Washirika wa Maendeleo ambayo tulikuwa tunategemea zitaingia ili kuhakikisha kwamba zinatusaidia. Pia kulikuwa na ruzuku ya Serikali karibu shilingi billioni 285 ambayo ilitakiwa pia kuchangia ili kutimiza hiyo fedha bilioni 672 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi fedha iliyotoka ni kama nilivyosema ni bilioni 343 tu ndiyo iliyotoka. Sasa ni nusu ya bajeti yote ambayo tulikuwa tumeipitisha kwenye mwaka 2018/2019. Fedha hii ambayo tunaitenga kila wakati na tunaipitisha inakuwa ni ndogo na kila siku Wabunge tukiwepo

humu tunalalamika kwamba fedha ni ndogo sana, iongezwe lakini cha kushangaza hata hii fedha ndogo ambayo inakuwa imeshapitishwa ndani ya Bunge, inashindwa kutolewa na Serikali ili kwenda kutekeleza miradi ya wananchi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote hicho fedha ya mchango wa wananchi kwenye mafuta ya dizeli na petroli ambayo ilikuwa imetengwa shilingi bilioni 185, imetoka shilingi bilioni 155 imekwenda kutekeleza miradi ya maji. Pia fedha ya wafadhilli, kati ya bilioni 229.9, fedha iliyotoka ni shilingi bilioni 188, ukizijumlisha fedha hizi inakupa hesabu ya shilingi bilioni 343.4. Tafsiri yake ni kwamba Serikali upande wa Hazina kama ruzuku ya Serikali bilioni 285 haijaonekana katika hesabu inayoonekana sasa hivi hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa napitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa kwenye ukurasa wa 104 na 105, Mheshimiwa Waziri amejaribu kuongea kuhusiana na changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza na ni kwanini wameshindwa kutekeleza miradi mbalimbali ambayo ilikuwa imepangwa. Tatizo kubwa wanadolizungumzia kama Wizara wanalalamika kwamba fedha hazitoki kwa muda na fedha hazlendi ili kutekeleza miradi na hii imesababisha kukwamisha miradi mingi isiweze kutekeleza. Sasa kama Wizara Serikali imeanza kulalamika kiasi hiki, ni wajibu Wabunge sasa kuchukua hatua kujaribu kuiambia Serikali itoe fedha ili Wizara ikaweze kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio lazima tusimame tuangalie Waziri wa Fedha pamoja na Hazina waangalie ni namna gani wanawenza kuwa wanatoa fedha ambazo tunakuwa tunazipitisha ndani ya Bunge hili ili ziende kufanya kazi na Watanzania waweze kupata maji. Hatuwezi kuwa kila siku tunatengafedha halafu baadaye hizo fedha haziendi kufanyakazi. Hili ni jambo ambalo linatushangaza sana na ni wajibu wetu kama Wabunge, ni wajibu wako kama kiongozi wa Bunge kuhakikisha kwamba unalismamia hili jambo na fedha zinatoka, maana yake nakumbuka mwaka uliopita ulijaribu kumweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba

kwanini hupeleki fedha katika miradi ya maendeleo kama ambavyo tumepitisha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ningeomba Bunge lako hili lihakikishe kwamba Serikali wakati wote tunapokuwa tumetenga bajeti yetu, ni lazima bajeti hii ikatekeleze miradi kama tulivyokuwa tumpanga. Sasa miradi iliyotekelizwa mwaka 2018/2019 ni nusu ya fedha ambazo tulikuwa tumechezitenga. Tafsiri yake ni kwamba mwaka 2019/2020 tunakwenda kutekeleza viforo ambavyo tulitakiwa kutekeleza katika mwaka uliopita. Kwahiyo, naomba sana jambo hili lazima tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, nilimsikiliza Mheshimiwa Musukuma pale amesema kwamba hataki Sh.50 iweze kuongezwa. Watu wengi wanaweza kuona hii ni hoja dhaifu, lakini si hoja dhaifu, ni hoja nzuri na inaendeleza kutukumbusha kwamba tunavyozidi kuongeza tozo kwenye mafuta kwa ajili ya maji tafsiri yake ni kwamba tunawaongeza wananchi mizigo, tunaendelea kuongeza gharama wananchi badala ya kuwapunguzia gharama wananchi. Hawa Watanzania ambao tunawazungumza leo kuwaongeza kila siku mafuta hawa wananchi wanalipa kodi, hawa wananchi kila siku tunaosema kwamba tuwaongeza ni wananchi ambao tayari wanalipa kodi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo lazima tuangalie tunachokizungumza tunamaanisha namna gani, je, kodi wanazozitoa wananchi na ambazo tunatenga kwenye bajeti hii kwanini Serikali inashindwa kutoa fedha hizi na kwenda kufanyakazi. Nimeshasema kuna fedha bilioni 285 zilitengwa mwaka jana ambazo Hazina walitakiwa wazitoe mpaka sasa hivi tukisema kwenye mahesabu ambayo tumeypiga hapa kufikia bilioni 343 hutajiona fedha iliyotoka Hazina. Sasa tunataka fedha za wananchi ziweze kutumika kama ambavyo tunapitisha bajeti katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kutokuwa na maji safi na salama kwa wananchi ni makubwa sana katika Taifa kwasababu wananchi wengi sasa wanaumwa matumbo na

matumbo haya yanababishwa sana na kupata maji ambayo ni machafu. Sasa Serikali inaingia gharama kubwa sana ya kununua madawa na tumekuwa tunajinasibu ndani ya Bunge hili kwamba Serikali inatenga fedha nyingi kwaajili ya kununua madawa. Kununua madawa kwa fedha nyingi sio sifa ni kwamba Watanzania wengi ni wagonjwa, Watanzania wengi wanaumwa na ndio maana tunatenga fedha hizi, lakini fedha hizi tunasababisha kuzitumia vibaya kwenye madawa kwasababu hatutaki kutengeneza mazingira mazuri ya kupata maji safi na salama. Ni lazima tujikite kuhalikisha kwamba tunawapatia wananchi wetu maji safi na salama na bajeti zingine hizi zitakwenda kufanya kazi zingine ambazo zinahitajika zaidi, lakini hiki tunakihitaji wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia kuna kiasi cha maji kwa mtu kwa mwaka, ukiangalia katika takwimu mwaka 1961 kiasi cha matumizi ya maji kwa mtu mmoja mmoja kwa mwaka ilikuwa ni ujazo wa mita za ujazo 7,862, lakini mpaka mwaka 2018, sasa hivi zimeshuka mpaka 2,300. Hii inatoa picha gani? Ni kwamba Serikali haijaweka uwekezaji mzuri ili kuweka uwiano mkubwa kulingana na ongezeko la Watanzania katika Taifa hili. Ni lazima tuone na ndio maana mjambe mmoja jana amesema tunakoelekea Tanzania sasa hivi tuko kwenye mstari ambao uko kwenye hatari ya kukosa maji kabisa kwasababu wananchi wanazidi kuongezeka, lakini uwekezaji unazidi kushuka. Angalia katika bajeti ya mwaka huu, bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri anahitaji bilioni 610 ili kutekeleza miradi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:...lakini kila mwaka bajeti inazidi kushuka. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Frank hujaunga mkono hoja.
(*Kicheko*)

Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji na pia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya. Nianze kwa kuipongeza Wizara nikianza kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji kwa kazi ambayo wanaifanya. Ninaimani kabisa kwamba wakiwezesha pesa za kutosha wataweza kufanyakazi nzuri zaidi kuliko ambavyo sasa hivi wanafanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu hizo, ningependa kuchangia maeneo mbalimbali yanayogusa katika eneo langu. Kwanza nianze na ule Mradi wa Maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mtwara Mjini. Mradi ule ukitekelezwa utapeleka maji katika vijiji vya Mtwara Vijijini zaidi ya 30, lakini mpaka sasa hivi mradi huu umekuwa ukisusua. Ukikutana na watendaji wanakwambia mradi upo, wakati mwingine ukikutana na Waziri anasema huu mradi haupo. Kwahiylo ningependa Waziri atakapokuja kutoa majibu atuambie Mradi huu waKutoa Maji Mto Ruvuma upo au haupo na kama haupo sisi wa Mtwara Vijijini vile vijiji ambavyo vilipangiwa kupata maji kutoka katika mradi huu vitapelekewa maji kwa mradi gani?

Mheshimiwa Spika, katika kuptitia bajeti nimekuta sehemu imeandikwa kwamba mradi wa kutoa maji mto Ruvuma kupeleka Mtwara kwa gharama ya shilingi bilioni moja. Kwa kweli imenitia wasiwasi hivi kweli unaweza ukatoa maji Mto Ruvuma ukafikisha Mtwara Mjini kwa shilingi bilioni moja au hii ni *tokentu* kama mradi utakuwepo wataongezea pesa au bado wako katika kusuasua uwepo au usiwepo. Kwahiylo Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo pia nataka ufanuzi ni suala la mradi wa maji katika Mji wa Mtwara na Babati, yenyewe imetengewa Sh.2,500,000,000 kwa kweli kwa miji miwili na Mheshimiwa Waziri ametembelea katika Mradi wa Mtwara nilikuwepo, ameona changamoto zilizopo, maji

yanayokwenda katika Mji wa Mtwara zaidi ya kuyatibu hayachunjwi, yanakwenda na rangi yake ileile. Mheshimiwa Waziri kazi ni kubwa inayotakiwa kufanyaika pale.

Mheshimiwa Spika,tunayomiradi ya maji ambayo ni mibovu, tunao Mradi wa Kitere, ambao unatakiwa upeleke maji katika Vijiji vya Chemchem,Nakada, Chekelenina Lilido, lakini mradi huu ulijengwa muda mrefu na sasa hivi unahitaji ukarabati mkubwa, lakini nimeangalia kwenye hii bajeti sijaona. Tunao Mradi wa Mbuo – Mkunwa,Mradi huu unaithwa Mbuo- Mkunwa lakini Mkunwa hata hayo maji hawajayaona, upanuzi kila siku utafanyika, utafanyika. Mradi huu tumewapa *MTUWASA* lakini pamoja na kuwapa *MTUWASA* hatuoni kasi wala manufaa ya kuwapa wao, tulitegemea baada ya wao kupewa huu mradi, basi vijiji vyote vinavyotakiwa kuhudumiwa na mradi huu wangkuwa wameshafikiwa.

Mheshimiwa Spika,nimpongeze na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa Mradi wa Lyowa kwasababu amenihakikishia kwamba pesa zimeingia, nami nitafuatilia kujiridhisha kama pesa ya kununua *pumpimekwenda* ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika,tunayo changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika katika Mradi wa Mbawala Chini, ambao wenyewe unatakiwa kuwashudumia wananchi wa Manispaa ya Mtwara, Mbawala lakini na Kata ya Nanguruwe na wenyewe mara nydingi umekuwa unapata uharibifu wa mitambo, lakini hata usambazaji wake na wenyewe haujafikia kiwango ambacho kinahitajika.

Mheshimiwa Spika,tunazo kata ambazo kwa kweli zinachangamoto ya upatikanaji wa maji kwa kiasi kikubwa, Kata ya Lipwidi, Kata ya Mangopachanne, Kata ya Madimba na Kata ya Tangazo tunao mradi, lakini kuna vijiji ambavyo bado havijafikiwa na mradi huu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri nimeangalia kwenye bajeti kuna miji kuna miradi, nimesoma, nimeangalia katika mkoa wangu, naona Mradi wa Makonde, nimeuona Mradi wa Mangaka nimeiona miradi mingi, lakini mradi haswa wa kuhudumia Halmashauri ya

Wilaya ya Mtwara nimejaribu kuutafuta mradi hasa wa kusema huu ndiyo utasaidia kuondosha kero ya maji katika Halmashauri ya Mtwara Vijiji ni sijauona.

Mheshimiwa Spika,Mheshimiwa Waziri alipotembelea Mkoa wa Mtwara aliouona Mradi wa Maji wa Msanga Mkuu, aliona changamoto ya maji kubadilika rangi, ambapo hata wananchi wanaogopa kunywa maji yale kutohana na rangi na alituahidi kwamba angeleta pesa za kuwezesha mradi ule ili ijengwe chujio dogo la kuweza kusafisha yale maji. Nimejaribu kuangalia humu sioni chochote.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumza, inaonesha Wizara baadhi ya Halmashauri au Mikoa hawajui ilivyokaa au ikoje. Nimeangalia ukurasa wa 163, nikaangalia pesa ambazo zimeenda kwenye mikoa kwenye miradi mbalimbali, nimesikitika kuona kwamba wilaya yangu kwa Wizara ya Maji inaonesha kwamba wamenitengea pesa nyingi, lakini kiuhalisia hizo pesa haziji kwenye wilaya yangu. Inaonesha wilaya yangu nimetengewa shilingi milioni 943 ambapo shilingi milioni 20 zinaenda Kilambo, milioni 70 zinakwenda Msanga Mkuu, milioni 93 zinaenda Nanyamba - Malanje na milioni 630 zinaenda Mradi wa Maji wa Ujenzi wa Chipango, Namyomyo, Manyuli,Mnavirana Mkaliwata. Hivi vijiji huu mradi ni wa Wilaya ya Masasi *DC*, zaidi ya shilingi milioni 630.

Mheshimiwa Spika, sasa huko wakikaa wanaonesha kwamba milioni 600 imeenda Mtwara *DC*, kuna milioni 128 ambazo ni za maji Nanyamba - Mbembaleo. Kwahiyo kiuhalisia Mtwara Vijiji imepata milioni 90 peke yake, lakini hapa inaonesha zaidi ya milioni 900 imeenda Mtwara Vijiji. Hii si haki na naomba hizo pesa ambazo zinaonesha milioni 600 zimekwenda Mtwara Vijiji wakati zimeenda Wilaya ya Masasi, basi watafute popote zinapopatikana ziweze kuja Mtwara vijiji ili tuweze kuondoa changamoto. Kwa sababu Masasi kama Masasi wamewatengea pesa zao, tena nyingi bilioni 1.8, halafu wakachukua milioni 600 badala ya kupeleka Masasi ikaonesha wamewapa bilioni 200 na nukta zake kule wamekuja kuziweka Mtwara Vijiji, kama ziliikuwa zinafichwa

sijui, lakini sidhani kama ni kwa bahati mbaya. Naomba hizo milioni 600 nilizokuwa nimetengewa zije zote Mtwara Vijiji na Masasi wawawekee kwamba wamewapelekea bilioni 200.

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie tena kuwaomba, wakati wa kuandaa hizi bajeti na takwimu zetu na vijiji tujiridhishe, kwasababu nitaonekana mlalamishi, nimeletewa milioni 900, wakati kiuhalisia nimeletewa milioni 90. Nisikitike sana kwa hilo na nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majibu anijibu pesa hizo ambazo zilistahili kwenda Mtwara Vijiji zitapelekwa lini na miradi ya Mtwara Vijiji itatekelezwa pipi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Mheshimiwa Azza Hilary Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa William Ngeleja ajiandae.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliye nijalia afya na uzima na hatimaye nimeweza kusimama kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa pongezi katika Wizara ya Maji. Nisipolisema hili, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao watanishangaa sana, kwa sababu nimezunguka sana, katika Ofisi za Wizara ya maji na hatimaye kile nilichokuwa nakifuata kimekamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii, kuwashukuru sana, Wizara ya Maji na Watendaji wote, Kata ya Tinde na vijiji vyake vyote vilikuwa vimesahaulika kwenye Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Nilisimama humu ndani nikasema, namshukuru sana Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, alilipokea, tukaa kikao Ofisini kwake na Watendaji wake na hatimaye

mradi ule sasa unakwenda kuanza kutekelezwa mwezi huu wa Mei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya, vijiji vyote vilivyopo Kata ya Tinde, vinakwenda kupata maji ya Ziwa Victoria. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa, yale yaliyofanywa na Mheshimiwa Eng. Kamwelwe uyaendeleze na mradi ule uende kukamilika. Mradi ule unaenda kutekelezwa kuanzia mwezi huu wa Mei na utafanya kazi ndani ya miezi saba, nikuombe sana, uende ukasimamie na mradi huu uweze kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nisiishie mradi huo, nilisimama ndani ya Bunge hili lakini nimezunguka sana Ofisi za Wizara ya Maji kwa ajili ya mradi wa maji Kata ya Masengwa. Mradi huu umeanza kufanya kazi na unaendelea vizuri. Niwashukuru sana Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lilitopo, fedha kwa Timu iliyoundwa kwa ajili ya kufuatilia mradi huo wa maji hazijapelekwa hata senti tano. Hivyo, tunaipa kazi kubwa Timu ya ufuatiliaji kufanya kazi kwa kutumia pikipiki kwa sababu hawajawezeshwa kwenda kusimamia mradi huu. Niwaombe sana Wizara ya Maji wapeni Halmashauri fedha hizo ili waweze kuusimamia Mradi wa Masengwa kama ambavyo ilikuwa imepangwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, akini Mradi wa Masengwa wameleta hati ya madai ya shilingi milioni 94 kwa ajili ya mradi huu, malipo hayo bado hayajafanyika. Niwaombe mtoe malipo hayo ili kazi hii iweze kuendelea na kuweza kukamilika mapema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu katika Mradi wa Maji wa Masengwa. Mradi huu una zaidi ya shilingi billioni nne, ni mradi mkubwa sana na kuna tenki kubwa ambalo linakwenda kujengwa. Kulikuwa na mradi awamu ya kwanza, awamu ya pili na awamu ya tatu. Awamu ya kwanza, ndiyo huu ambaa unatekelezwa. Niwaombe sana Wizara ya Maji,

toeni pesa kwa ajili ya usanifu kwa awamu ya pili ya Mradi wa Maji wa Masengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya Mradi wa Masengwa utakwenda kutekeleza Vijiji vya Ishinaburandi, Isela, Idodoma na Ibingo. Hawa watu vijiji vyote hivi watanufaika kupata maji katika mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia Mradi wa Maji wa Masengwa, naomba nijikite katika vijiji ambavyo vipo nje na Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Vijiji hivi ambavyo haviko ndani ya kilomita 12, haviguswi popote na Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria lakini hakuna namna yoyote ya vijiji hivi kuvipatia maji. Vijiji hivi viko 23, naomba nivitaje baadhi. Vijiji vya Mwasenge, Nyang'ombe, Nyaligongo, Bushoma, Kilimawe, Mwamala, Bugogo, Masonula, Igalamya, Singita, Chabuluba, Mwamkanga, Msalala, Supigu na Masokelo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi 23, vina idadi ya watu 59,241. Wizara ya Maji mmejjipangaje kuhakikisha kwamba vijiji hivi 23 tunaleta mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba watu hawa na wao wanakwenda kupata maji. Akina mama wanahangaika, hawawezi kufanya shughuli zozote za kiuchumi kwa kutafuta maji, ukiangalia Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria uko mbali nao, je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha vijiji hivi na wao sasa wanakwenda kupata maji ya uhakika ili na akina mama hawa waweze kufanya kazi zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, niingie katika vijiji ambavyo viko ndani ya kilomita 12 lakini havijapata maji mpaka leo. Toka awamu ya kwanza ya Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria vijiji hivi havijapata maji na viko ndani ya kilomita 12. Kila nikisimama ndani ya Bunge hili huwa nasema, naomba pia nivitaje tu. Vijiji hivi viko 22 toka awamu ya kwanza ya Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Vijiji hivi vina idadi ya watu 58,465 ambao wako ndani ya kilomita 12 lakini hawapati maji ya Ziwa Victoria wanayaona yanakwenda kwa wenzao. Vijiji hivi ni Mawemilu, Buduhe, Azimio,

Mwandtu, Ibibu, Mapingiri, Mwashagi, Mwamala, Mwabagehu, Mwashilugura, Mwambasha, Mwalukwa, Bulambila na Shatimba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haipendezi toka awamu ya kwanza ya Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, hawa watu wanapewa matumaini kwamba watapewa maji, wako ndani ya kilomita 12, lakini mpaka tunakwenda awamu nyingine sasa hawajapata maji.

Je, Wizara mna mpango gani kuhakikisha vijiji hivi 22 vinakwenda kupata maji kwa sababu wanaishi kwa matumaini wakitegemea kwamba siku moja na wao watapata maji kwa sababu utaratibu unawaruhusu wako ndani ya kilomita 12. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusemea hilo, naomba niingie katika Manispaa ya Shinyanga, Mradi wa Maji wa Galamba. Mradi huu umeanza kutekelezwa ndani ya Manispaa ya Shinyanga lakini kwa masikitiko makubwa, toka Agosti, 2018, Halmashauri imeleta hati ya malipo ya shilingi milioni 131 mpaka sasa hivi fedha zile hazijalipwa na mradi ule umesimama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunaposema Wizara ya Maji kuna tatizo huko chini angalieni. Inawezekana huku juu mko vizuri sana lakini Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kuangalia Ofisini kwako kuna shida gani kwa sababu Wabunge wengi pia wanalamika hati hizi zikiletwa fedha hazitolewi kwa wakati. Fikiria toka Agosti, 2018, fedha hizi hazijalipwa mpaka leo, kuna tatizo gani katika Mradi wa Maji wa Kijiji cha Galamba katika Manispaa ya Shinyanga? Nimuombe sana Waziri alifanyie kazi suala hili na nitafurahi kama nitapata majibu kabla hujahitimisha mjadala wako kujua Mradi wa Maji ya Galamba mmewapelekea pesa au unanipa majibu gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Tunazunguka kukagua miradi mingi katika Halmashauri hapa nchini lakini katika miradi

mibovu ambayo tunakutana nayo ni miradi ya maji. Sijui kuna tatizo gani, miradi mingi unakuta ama maji yanatoka lakini tenki linavuja. Serikali imewekeza fedha nyngi lakini unakuta mradi ule hauna tija kwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi najiuliza miradi ile inasimamiwa na Wahandisi haya matatizo yanatokea wapi? Mheshimiwa Waziri jaribu kuangalia, fedha nyngi ya Serikali inakwenda kule lakini miradi mingi ina matatizo.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Azza, muda wako umekwisha.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Ujumbe umefika, Wasukuma wana kiu kwelikweli huko Mheshimiwa Waziri. Wakizidiwa sana wahamie Dodoma tuna afadhali kidogo. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae. Mheshimiwa Ester dakika tano.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kama Bunge, nafikiri hatuwi wakali vya kutosha. Nadhani mnakumbuka miaka mitatu mfululizo Wizara hii imekuwa ikitengewa pesa kidogo sana, asilimia 18, 19. Bajeti iliyopita tumetenga shilingi bilioni 700 wamepata shilingi bilioni 300, hivi hizi zilizobaki zinafidiwa lini? Leo anakuja tena kuomba shilingi bilioni 600. Lazima Bunge tutimize wajibu wetu wa kuibana Serikali, *unless otherwise tutakuwa tunamshambulia* Mheshimiwa Prof. Mbarawa wakati Serikali haitimizi wajibu wake wa kupeleka pesa za kutosha katika Wizara ya Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maji hayana mbadala, umeme ukikatika leo, unaweza ukawasha kibatari, lakini ukikosa maji huwezi ukatumia maziwa kuoga, huo ndiyo ukweli. Huwezi ukatumia maziwa kunywa, kiu ya maji na kiu ya maziwa ni vitu viwili tofauti. Operesheni hospitalini zinakwama kwa sababu maji hakuna na ukiuliza sababu ni nini, Serikali haipeleki fedha za kutosha katika Wizara ya Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tutakuja tutawasulubu hawa Mawaziri lakini pesahaziendi, Bunge sasa tutimize wajibu wetu, tuwe wakali, tuhakikishe pesa zinaenda na hiyo dhamira ya kumtua mama ndoo kichwani iwe kweli. Sisi tunaotoka majimbo ya mikoani, tunajua akina mama wan-a-suffer kiasi gani kwa kukosa maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo ninapozungumzia Jimbo la Bunda Mjini, *shame*. Kuna mradi wa maji pale una miaka kumi na moja haujakamilika yaani mradi wa maji na mwanangu Brighton wamepishana miaka mitatu. Mradi una miaka kumi na moja haujakamilika, Brighton yuko *form one* ana miaka kumi na nne, ni aibu. Kila siku unakuja kuzungumza kitu hicho hicho, ukiuliza tanki, chujio, chujio gani miaka kumi na moja inashindwa kukamilika watu wapate maji safi na salama? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni aibu, tunatesa wanawake, tunatesa akina mama vijiji huko. Wanatembea umbali mrefu wanakosa maji safi na salama. Mheshimiwa Waziri umeenda, naomba sasa usifike mwaka wa kumi na mbili, wananchi wa Bunda wamechoka kupata maji machafu. Hatuna mbadala, hatuwezi kunywa maziwa wakati tuna kiu ya maji, hatuwezi kuoga maziwa wakati tunataka kuoga maji, *please*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine kwenye Kijiji cha Chakung'ombe, Mamlaka ya Mji wa Bunda ni *Grade C* haipati ruzuku Serikalini, kuna mradi wa shilingi milioni 800 umekamilika. Hata hivyo, kwa sababu Serikali haiwapi pesa mradi umeshindwa kuijendesha, umefungwa na gharama za maji zimepanda, kila siku wananchi wanalamamika. Haya mmeshindwa kukamilisha miradi iwezesheni basi Mamlaka

hii iweze kutimiza majukumu yake. Gari haina, hamuipelekei ruzuku, mnategemea nini? Tunawapa *stress* tu watumishi, *stress* ya kuongezewa mishahara wanayo sasa wana-*stress* ya kupelekewa vitendea kazi ili watimize majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaombeni sana Serikali hebu tutimize wajibu wetu na sisi Wabunge tutatimiza wajibu wetu kuisimamia hiyo miradi iwe na tija kwa sababu tunahitaji kumtua mwanamke ndoo kichwani. Tunamtuaje ndoo mwanamke kichwani kama hatupeleki pesa za kutosha? Nawaomba sana Halmashauri yangu ya Mji, Mamlaka ile ya Maji ipewe ruzuku iweze kutimiza majukumu yake, watu wana morali lakini Serikali haipeleki hela, *please*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya. Tunaendelea na Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kushiriki kwenye mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia zote. Mchango wangu utakuwa na sehemu mbili, kwanza ni shukrani na pongezi kwa yale ambayo yamefanyika Jimboni Sengerema, lakini la pili nitakuwa na ushauri kwa yale mambo ambayo naona ni kazi zinazoendelea kwa sababu hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika pongezi, naomba niungane na wenzangu kusema kwamba Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa pamoja na wenzake Mheshimiwa Naibu Waziri Jumaa Aweso, Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu, Eng. Kalobelio pamoja na Wakurugenzi na wataalamu wenginge wanaopambana kadri inavyowezekana, wanajitahidi sana. Tumeona na

inawezekana kukawa na udhaifu katika baadhi ya maeneo lakini dhamira yao naiona kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa mashahidi kwa namna ambavyo wanajitahidi kutatua kero katika nchi yetu. Mheshimiwa Waziri ameshafika Jimboni Sengerema, Mheshimiwa Naibu Waziri anaendelea kutembelea maeneo mbalimbali nchini, pia Katibu Mkuu mwenyewe alishafika Sengerema, Naibu Katibu Mkuu ameshafika na Wakurugenzi wanaendelea kufanya ziara mbalimbali kutatua kero za maji. Kwa hiyo nachosema ni kwamba wanapambana na sisi Mkoa wa Mwanza Mamlaka ya Maji *MWAUWASA* inaendelea kufanya kazi nzuri, ingawaje ziko changamoto.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Sengerema wamenituma niipongeze Serikali kwa haya yafuatayo. Tumekuwa na killio cha muda mrefu cha upatikanaji fedha lakini hivi karibuni Sengerema tumepata shilingi milioni 502 kwenye mradi wa maji unaohusu Kijiji cha Buyagu, Kalangalala hadi Bitoto. Pia tumepata shilingi milioni 58 kuhusu uchimbaji wa visima katika Vijiji vya Illekanilo, Kasomeko na Igulumuki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 121 kwenye kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri, unaona katika mgao wa fedha za miradi ya maji vijijini. Sisi Halmashauri ya Sengerema tumetengewa shilingi milioni 886, asiyeshukuru kwa kidogo hawezikushukuru hata kwa kikubwa. Tunasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 63, ambao unahusu miradi ya maji katika vijiji vilivromo pembezoni mwa Maziwa Makuu, ukisogea kidogo chini ukurasa wa 64(iii), kuna mradi mkubwa umebuniwa na Serikali, unahusu kutoa maji Ziwa Victoria na kuwafikia walengwa katika Vijiji 301. Hapa nazungumzia Mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara pamoja na Mkoa wa Simiyu. Sisi kwenye Halmashauri ya Sengerema tuna zaidi ya vijiji 26, tunasema ahsanteni sana kwa kuiweka Sengerema katika ramani ya huo mradi mkubwa na tunaamini fedha zikipatikana za kutosha mradi

huu utatekelezwa. Serikali imetoa *commitment* hapa, kwamba baada tu ya kukamilisha zoezi ambalo linaendelea sasa hivi la usanifu, ujenzi wa mradi huo, utaanza, ni jambo jema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo kuna kazi zinazoendelea, naikumbusha Serikali, nimekuwa na mawasiliano mazuri, nashukuru tumepata hizi fedha ambazo nimesema zaidi ya shilingi milioni 500 lakini kuna fedha zingine tunazisubiria kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya kufikisha maji kwenye kijiji cha Ibondo kwa Mwarabu, Mwabalugji kule na hasa eneo la Zanzibar, kule Sengerema pia kuna Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia tuna miradi ambayo tunasubiri fedha kama mradi unaohusu Vijiji vya Mwaliga, Kang'washi na Sima, pale kuna ujenzi wa kisima pamoja na kisima cha Kijiji cha Nyamahona. Haya ni maeneo ambayo tunasubiri tu fedha, Serikali ilitoa fedha hivi karibuni *roundya* kwanza, lakini itatoa tena fedha nadhani labda kufikia mwishoni mwa mwezi huu ili tukaikalimishe miradi hii. Tunasema ahsanteni sana Serikali kwa kazi kubwa mnayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kazi zinazoendelea na hapa naikumbusha Serikali kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Nyasigru, Bungo na Ngoma. Mradi huu unahu kutoa maji Ziwa Victoria umebuniwa zaidi ya miaka miwili iliyopita na utaratibu wa kumpata mkandarasi, atakayeshughulikia mradi huu ulikamilika Mei, 2018, leo ni mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, naelewa sana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaposema ziko changamoto katika Wizara hii. *Imagine* tumempata mkandarasi kwa utaratibu wa kawaida wa Serikali Mei, 2018 na hapa katikati mimi sijalala, nimekuwa nina mawasiliano na Serikali mazuri tu lakini mpaka leo mkandarasi hajaingia *site*. Bado kuna *reservation, technically* wanasema kuna hili na lile lakini kwa nini ichukue mwaka mzima? Haya ndiyo mambo ambayo tunasema yanahitaji kuongezewa kasi ya utatuzi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikumbushe *MWAUWASA* wako hapa wanasiliza, pale kwenye mradi mkubwa Mjini Sengerema pale na vijiji vingine ambavyo vinapitiwa na mradi ule kuna eneo la Kizugwangoma, Misheni pamoja na Bujora kuna ahadi ya kujenga booster ili kufikisha maji maeneo hayo. *MWAUWASA* waliahidi kwamba ujenzi ungekuwa umeshaanza toka Aprili, 2019, mpaka ninavyozungumza bado na mimi nafuatilia kila siku. Kwa hivyo, unaweza kuona hizi changamoto zilizopo, tunaamini kwamba fedha zipo lakini katika kasi ya utekelezaji kuna mahali hatuendi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuna Mradi wa Nyampanda ambaao tayari taratibu zote za kumpata mkandarasi zimeshakamilika, tarehe 25 Aprili, ilikuwa tushuhudie kusainiwa kwa mkataba kwa mkandarasi aliyepatikana. Hivi karibuni Serikali ilahirisha tuisaini tarehe 25 Aprili hadi tarehe nyingine itakapopangwa.

Mheshimiwa Spika, najua nina wito wa kukutana na Watendaji wa Wizara hii baada ya hapa tukayajadili haya tupeane *update* lakini nawaomba wajiandae kunipa majibu kwamba ni nini mkandarasi wa Nyasigru, Bungo, Ngoma yeye hajapatikana? Ujenzi wa hii *booster* niliyosema ili kuyafikisha maji kwenye maeneo ya Misheni, Kizugwangoma, Bujora lakini lini mtasaini mkataba wa kuyafikisha maji katika Kijiji cha Nyampande? Pia tuna Kijiji cha Sima ambako kinaingia kwenye programu ya kuanzia mwezi Julai lakini kuyafikisha maji katika Kijiji cha Tunyeng'e.

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu ya ushauri nina jambo la kusema ukisoma ukurasa wa kumi wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu alivyokuwa anaelezea hali halisi ya upatikanji wa maji katika nchi yetu na nijielekeze hata katika maeneo ya vijijini. Kwenye ukurasa huu wa kumi wa hotuba hii anasema kufikia mwezi wa nne mwaka huu upatikanaji wa maji katika vijiji ulikuwa ni asilimia 64.8 lakini lengo ni kufikia asilimia 85 ili tufikie lengo lile kuu la kuhakikisha kwamba wannachi hasa vijijini wanapata maji ndani ya mita 400.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo ukisoma ukurasa wa 106 hadi 108 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri anakubali kwamba kinachotukwamisha kufikia malengo yetu ni changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati na fedha za kutosha. Pia hotuba ya kamati inayoshughulikia wizara hii Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ukurasa wa tano wamezungumzia changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, katika hili nimeshindwa kuelewa sitaki kuwa vuguvugu ama baridi ninashindwa kuelewa tunakwama wapi kwa sababu hapa tumezungumza na katika hili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema ninasimama na wote wale wanaouna mkoно tuongeze shilingi 50 katika ule mfuko ili tuongeze kasi ya kuwafikishia maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninafahamu wasilwasi uliopo lakini nataka *ni-share* uzoevu kidogo nilionao. Baada ya m dororo wa uchumi kuikumba dunia mwaka 2007 hadi mwaka 2009 mwaka mmoja au miwili baadaye sisi kama Taifa tulikumbwa na tatizo kubwa sana la uchakachuaji katika mafuta hasa bidhaa ya petrol kwa maana ya *diesel* na petroli. Na tatizo liliokuwa limesababisha kutufikisha hapo ni kwa sababu katika bidhaa zile tatu, mafuta ya taa, *diesel* na petrol kwenye ushuru sisi tulikuwa tumetoa *exemption* kwenye mafuta ya taa, kwa hivyo uchakachuaji ukawa ni mkubwa sanan zaidi ya asilimia 87. Lakini tukajadiliana sana na jambo likawa gumu

Mheshimiwa Spika, wakati huo nikiwa Waziri wa Nishati na Madini na-*share* huu uzoevu tulinganishe hofu iliyokuwepo. Tulikwenda mara ya kwanza tukapa ushauri na Mheshimiwa Shabiby sijui yuko wapi alikuwa hapa alishauri kwamba ondoeni tufanye *harmonization* ya ushuru katika bidhaa zote hizi petrol, *diesel* na mafuta ya taa. Tulivyorekebisha tulivyunganisha ule ushuru hapakuwepo na uchakachuaji na tukasonga mbele na hofu kubwa ilikuwa kwamba zaidi ya asilimia 90 ya watanzania kwa maana ya Nishati ya Mwanga wanatumia mafuta ya taa lakini...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, hapakuwa na shida hiyo ndio maana nasema, nashukuru sana kwa nafasi hii naunga mkono hoja lakini Serikali tu itafakari tu ushauri wa Wabunge naamini kwamba tutaelewana tutafika mahali pazuri na sio lazima tuongeze mafuta tunawenza kuongeza kwenye maeneo mengine pia kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge, asante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mary Pius Chatanda

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ambayo ameiwasilisha Waziri ma Maji.

Kwanza niunge mkono hoja na kwamba nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo pamoja na kwamba kuna changamoto za hapa na pale hizo tunatarajia kwamba kutokana na haya ambayo yanayozungumzwa na waheshimiwa Wabunge yatashughulikiwa ili kusudi kazi ya kuwapelekea maji wananchi wetu kwenye majimbo yetu na kwenye halmashauri zetu yanafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nishukuru Serikali kwamba Korogwe mji nimeona wanasma kwamba nimo kwenye orodha ya miji ambayo itapewa maji kutoka fedha za mkopo wa India. Nikiangalia kwenye kitabu ukurasa wa 148 kwenye ile orodha waliyoiweka pale hiyo Korogwe Mji yenewe hajawekwa imewekwa HTM lakini miji iko 29 ni namba saba na HTM nachofahamu ni mradi ambao unapelekea maji Handeni.

Mheshimiwa Spika, sasa nisije nikawa vile napewa kama hisani niombe tu waniambie watakapokuwa wanasma hapa ili wananchi wangu nitakapokuwa naenda kuongea nao ninapowaonyesha kitabu hiki kwamba tupo kwenye mradi ule wa India lakini kwenye kitabu humu hatumo imeandikwa HTM na kule wanajua HTM ni Handeni basi ni

vizuri atakapokuwa ana-*wind up* hapo atamke kwamba huu mradi na Korogwe Mji ambako ndio kwenye chanzo cha maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa HTM unatoka Tabora kwenye chanzo cha maji ni Tabora kwenye kata yangu ya Korogwe. Sasa kama sionekani humu naonekana tu kwamba nipo kwa kueleza tu maneno na kuambiwa humo humu sijui nawaambia nini wananchi wangu wa Korogwe. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utakapokuwa una-*wind up* hapo ni vizuri basi ukawaeleza wananchi wa Korogwe wajue kwamba hicho chanzo cha maji cha Tabora ambacho kitapeleka maji kule Handeni basi na Korogwe mtapatiwa maji kutoka kwenye hichi chanzo cha maji, nashukuru sana endapo waziri atalisemea hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikupongeze na nikushukuru sana sana ulikuwa umepita umeenda ulifanya ziara kule Lushoto nilikupigia simu nikakuomba nikakwambia ndugu yangu naomba unipitie hapa kwenye ratiba yako haikuwemo uliweza kupita. Nikawa nimekueleza suala la mradi wa maji wa ule vijiji 10 nikushukuru sana sana kwa hatua ambazo umezichukua kwamba mradi ule wa vijiji kumi vile viwili tayari kwa maana ya kwamba Msambiazi tayari wanapata maji lakini sasa hivi wanaendelea yule mkandarasi anaendelea na ujenzi wa ule mradi wa Luengela relini na darajani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na bahati nzuri sana nakushukuru vilevile baada ya ku-*raise* ile *certificate* umeweza kumlipa yule mkandarasi hili nakushukuru sana Mwenyezi Mungu akubariki na kwamba kazi inaendelea vizuri kwenye ule mradi na bahati nzuri tena wameshatuma ile *certificate* nyingine ili kusudi muweze kuwalipa. Nimeona ni vizuri nikakushukuru kwa sababu nisipokushukuru kwa hili nalo nitakuwa sijakutendea haki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri nina mradi wa maji ambao tulipewa milioni 500 uko pale pale mjini, shida ya Korogwe Mji tuna

mto unapita pale, Mto Pangani. Lakini tuna tatizo la maji pale mjini kana kwamba hatuna chanzo cha maji, Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo wakati ule ndugu yangu Mheshimiwa Kamwele alitembelea Korogwe akazunguka akakuta kwamba tuna mto unapita pale akaamua kwamba tuutumie ule mto ndipo akatuletea fedha milioni 500 imeshajengwa *intake* imekwisha imejengwa tayari chujio limemalizika. Kilichobaki sasa ni miundombinu ya kuwapelekea wananchi maji.

Mheshimiwa Spika, hivi navyokwambia Korogwe kila siku kuna kipindupindu kuanzia mwezi wa tatu wananchi wangu ni kipindupindu, mwezi wa nne, mwezi huu hivi navyozungumza watu wako vitandani ni kipindupindu wanakwenda kuchota maji kwenye mto, lakini mkitumalizia mradi huu tutapunguza hili tatizo la kipindupindu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri alitembelea mradi huu aliuona na Mheshimiwa Rais alipokuwa amekuja kufungua ile *stand yetu* mpya alituahidi kutupa fedha za kumalizia hiyo miundombinu bilioni 2 ili kusudi mradi ule ukamilike. Sasa wananchi wa Korogwe kila siku wanashubiri na kuniuliza Mheshimiwa Mbunge kwamba Rais alituahidi mbona huu mradi haukamiliki.

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara naomba basi muutembelee ule mradi Naibu Waziri aliuona upo mradi ule pamoja na kwamba mnasema mmeniweka kwenye huu mradi wa fedha za India lakini zile milioni 500 ambazo zimeshajenga *intake* zimemaliza na *intake* nzuri zimejengwa chujio imekamilika, tutaufanya nini huu mradi? Hivi tuendelee kusubiri mtoto anasema nataka nguo, unasema subiri na mwenzako mama yako ana mimba subiri kwamba atakapoifungua ndio niwanunulie wote nguo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, nakuomba utembelee mradi ule Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji nakuomba utembelee mradi ule uone jinsi

ulivyojengwa na hatimaye wananchi wa Korogwe Mjini waweze kupatiwa maji yaliyo safi na salama waondokane na tatizo la kipindupindu, ni aibu kusikia kila siku tuna kipindupindu Korogwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji wanafanya kazi nzuri sana lakini kuna tatizo, tatizo liko kwa wasaidizi wao. Fedha zinazopelekwa kwenye miradi huko zinaweza zikapelekwa fedha zinaende kutengeneza mradi fulani unakuta ule mradi unaweza ukawa umekamilika lakini maji hayatoki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika niko kwenye Kamati ya *LAAC* tumepita kukagua miradi tumekuta matatizo ya aina hiyo, unaweza ukawa umejengwa mradi haujakamilika lakini amemaliziwa fedha zote amelipwa mkandarasi lakini mradi haujakamilika. Matatizo haya yanatokana na wasaidizi walionao huko chini wanaonekana ma-engineer wanakula pamoja na hawa wakandarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mkandarasi akalipwa fedha zote lakini mradi haujakamilika kwa nini alipwe fedha zote na hali mradi haujakamilika? Ushahidi ni pamoja na ninyi wenyewe tumewaona kabisa mnavoyzunguka mnavyofanya ziara kwenye kukagua miradi ya maji mmeenda kuyakuta matatizo haya. Kwa hiyo, tukuombe sana tunakutakia kila heri Mheshimiwa Waziri tuajua unapambana unapata shida.

Mheshimiwa Spika, wapo ma-engineer wako sugu huku chini huko nyuma inaonekana walishazoea kuona kwamba miradi ya maji ni shamba la bibi, ndugu yangu jikaze funga mkanda, Katibu mkuu jikaze mfunge mkanda haya majitu yaliyokaa huku yaliyokuwa yamezoea huko nyuma yashughulikieni ili kusudi muweze kufanikiwa, msipofanya hivyo tutasema fedha hazitoshi tutatafuta fedha zitakwenda lakini zitakwenda kuliwa hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana Mhehimiwa Waziri na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu atakusaidia tu utafanikiwa, mkifanikiwa kuwashughulikia hawa huko chini

basi nadhania hata hizi fedha tunazosema ziongezeke zitawenza kwenda kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kuunga mkono suala la kutumia *force account*. Fedha za maji kama tutatumia *force account* inawezekana kabisa tukafanikisha kama tulivyofanikisha kwenye miradi ya afya, kwenye miradi ya shule. Kuna ubaya gani? Ma-engineer hawa si wapo na tukitumia hii *force account* kwa sababu tuna watu ambao tayari kule kwenye wilaya zetu wastaaafu waliostaafu kwenye masuala ya maji watafanya hizi kazi kwa kutumia hii *force account*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutashuhudia tunafanya kazi ya miradi ya maji kwa gharama nafuu kuliko sasa, sasa hivi haya mambo ya wakandarasi mradi mdogo tu kwa mfano kisima cha maji mtu anakwambia kisima cha maji ni milioni 350 kitu ambacho mradi huo unaweza ukakamilika kwa milioni 20 tu wananchi wakapata maji kwa sababu mkipeleka kwa *force account* hata wananchi watashirikishwa na kwa sababu wanashida watafanya kazi zile ambazo wananchi wanahitajika kusaidia kuhakikisha Serikali inawapatia maji pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naunga mkono suala la kutumia *force account*. Lakini naunga mkono vilevile suala la kuongezea ile shilingi 50,000 hebu tuzingatieve kusimamia maazimio tuliyoyapitisha humu ndani. Tulyapitisha wenyewe haya maazimio tukisaidia kuongeza hii shilingi 50,000 utatuna huu mfuko na hatimaye angalau hata tunayoshauri haya yanaweza yakatekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri ni vizuri basi katika hili wenzetu watusikie na wasikilize ili kuona kwamba tunaweza tukafanikisha katika kuwapatia maji wananchi wetu huko kwenye miji yetu na kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mary Pius Chatanda kamishna kwa mchango wako tunakushukuru sana. Waheshimiwa wabunge jioni tutaendelea na wachangiaji wote wenye majina yaliyoorodhesawa hapa watapata nafasi hakuna ambaye hatapata nafasi hata kidogo.

Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Prudensiana Kikwembe, Mheshimiwa Dastan Kitandula na wengine wote mtapata nafasi. Na mimi nipongeze sana Waziri wa Maji Profesa na Naibu wako Mheshimiwa Aweso mmefanya kazi bwana yaani ninyi mnazunguka nchi hii kama tiara utawaona Kigoma, ujaka sawa wameshafika Mtwara duh! Huyu bwana kafika Mtwara lini tena? Mara Tanga mara wapi Profesa Kitambi hakiwezi kuota hata kidogo yuko barabarani kila siku, Mheshimiwa Aweso anajitwisha ndoo huko na nini kazi kubwa sana mnahangalkia kweli.

Lakini mvumulie tunapowalaumu Wabunge kwa sababu shida bado ni kubwa sana. Unajua mahali popote ambapo *expectation* ni kubwa kuliko unachoweza kukifanya hata sisi Wabunge wananchi wana matarajio makubwa mno kwetu kuliko labda tunavyoweza kutekeleza mambo yao na sasa bado mwaka mmoja, sasa hapo mwakani tukikutana hapa kindumbwendumbwe hapa. Kwa hiyo, tunawapongezeni, tunawapeni pole lakini tunajua kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tunapaswa kuwabana Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba angalau basi kile ambacho tumekibajeti mnakipata.

Waheshimiwa Wabunge, hili la visima vya watu binafsi vijijini ndio ukombozi tukifikiria kwamba eti tutatatua tatizo la maji vijijini kwa visima vya Serikali za Vijiji hatuwezi. Visima vya Serikali za Vijiji vile vya ujamaa vile uendeshaji tatizo, watakaa watatengeneza kamati za wajomba, binamu nani ndio demokrasi yenewe, wanakula hela kwenye mifuko ile hela hamna. Leo mtajitahidi mtabanabana inafika milioni 30, 40, 50 ukiangalia huku kidogo hata shilingi hakuna ilikoenda haeleweki miradi ya maji ina matatizo kweli na ndio yenye vyanzo vya fedha vya uhakika vijijini.

Baada ya vijiji vya ujamaa hivi kuwa havina mapato tena mengine mengine havina mapato vijiji, mapato yake ni mradi wa maji, kila mtu anaangalia kwenye mradi wa maji, shida. Kwa hiyo, angalau wale mwalimu kastaafu kachimba kisima chake, sijui nani kuna tajiri ng'ombe naye kachimba kisima anywesha mifugo na majirani wanachota pale, kuwaambia hawa waanze kutoa tena malaki, malaki hiyo ni *disincentive*. (*Makofi*)

Sasa tunakoelekea ni kuzuri kwamba sasa watu wanawenza wakamiliki visima vya maji hizi *bore holes* hizi zitasaidia sana. Tena watu wetu wakihamasihwa wakaelewa hii shida ya maji vijiji kama Dodoma sisi maji yako ardhini mengi tu, kwa hiyo shida ya maji itaisha dakika tu lakini tukiweka kodi tena huko itakuwa ni jambo ambalo; halafu tukategemee Serikali ndio peke yetu tuwe tuna-*provide* maji hatutaweza. Visima vya maji vya Serikai kila siku mgogoro mnatuma mtu akanunue *spare* anakuja ananunua India kuna *spare* inaitwa India badala ya kununua ile *genuine* ile *part* ananunua kitu fulani mkifunga siku mbili imekwisha bei iliyonunuliwa ni ya ile *genuine*, matatizo ni mengi ya uendeshaji.

Lakini pia kama walivyosema wenzangu gharama za miradi ya maji vijijini mimi sisemi za mjini, ni vijijini gharama ni kubwa sana. Ni vijiji vichache vinahitaji milioni 800, 600 ni vichache kama hii Dodoma sijui huko Usukumani huko kwa sababu wanahitaji mtandao wa mabomba mengi. Sisi hapa kwenye kijiji hata kiwe kikubwa kikiwa na vyanzo viwili vya maji usisambaze wewe weka bwalo kwenye kijiji kikubwa mbili, weka na vitenki vyake pale umemaliza tatizo. Sisi hiyo *luxurya* kusema maji yaje mpaka mlangoni tangu lini kwanza mnatuharibia utaratibu wa maisha sisi mila zetu jioni mabinti wanapoenda kuchota maji kule kilometra mbili kule sasa na vijana nao kidogo watu wanapata wachumba, sasa maji yako hapa hapa sasa watu watawaona watu wapi sasa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, kwa kweli tunajua na tunatambua kama Bunge mnajitahidi sana ni wizara ya watu waadilifu sana, huu

upigaji huko huko kwetu huko lakini na hawa wakandarasi washauri. Kila mshauri anataka mradi uwe na hela nyigi zaidi kwa sababu ye ye analipwa kwa *percent*.

Sasa ukiwa mradi wa milioni 100 ye ye atapata nini kwa hiyo wa milioni 100 anafanya milioni 300, 400, 500 ili asilimia yake iwe kubwa zaidi matokeo yake wanatandika mabomba ya plastiki kilometa kwa kilometa. Wewe mradi wa milioni 800 ukawaachie kijiji ukishaharibika nani atengeneze hakuna inakuwa *white elephant*, malalamiko yanakuwa ni kila siku yale yale kumbe tukiwawekea chanzo wanaweza ku-*Maintain* wenyewe nakadhalika. Na wanaweza katika ku-*Maintain* wenyewe wakachimba hata cha kwao kingine cha tatu na cha nne hali ya huduma ya maji ikazidi kuwa bora zaidi.

Kwa kweli tunawapongezeni sana tunawapa moyo na tuko pamoja msijione mko peke yenu hapana, shida ya maji ni kubwa kubwa kubwa. Matarajio yetu ni makubwa mno kuliko mnavyoweza kufanya lakini mnajitahidi sana maneno yetu yasiwavunje moyo mkaona kwamba mbona hawaoni hapana tunaona lakini matarajio ni makubwa mno. Kwa hiyo Katibu Mkuu na timu yako jipeni moyo jamani tatizo ni kubwa sana ndio maana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo kwa hapa tulipofika basi naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili leo jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Nafikiri tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na Mheshimiwa Dunstan Kitandula jiandae.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii niweze na mimi kuchangia katika hoja hii muhimu inayogusa maisha ya kila mwananchi katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo katika hii Awamu ya Tano tumeshuhudia mapinduzi makubwa ambayo na yeye pia amekuwa kiongozi shujaa katika kutatua matatizo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, napenda niwashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu na wasaidizi wao kwa ujumla katika Wizara ya Maji kwa namna ambavyo wamekuwa wakichapa kazi kwa bidii na pindi wanaposikia matatizo wamekuwa mstari wa mbele kwenda kuangalia kuna matatizo gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kuchangia kabla sijasahau, la kwanza kabisa katika Mfuko wa Maji. Katika hali ya kawaida, mimi nafikiri hata Mheshimiwa Rais anatambua namna gani tulivyo na shida ya maji hasa tunaotoka vijiji. Anatambua kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa Serikali hii iliyo sikuvi tusiwe na kigugumizi, Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamechangia kwa namna ya pekee, walivyoona umuhimu wa maji, sitaki kurudia michango yao. Naomba Serikali ichukue suala hili na ikalifanyie kazi ili tuone kwa namna yoyote ile ni mahali gani wanapata vyanzo vyaa mapato ili tuweze kupata maji ya uhakika hasa katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kuishukuru Wizara hii kwa bajeti iliyopita waliweza kunitengeta katika Kata yangu ya Ikuba, Vijiji vya Kashishi, Itula ambavyo vyote sasa hivi vina maji. Sasa naomba, Kata hiyo tu ya Ikuba, Kata ya Usevya na Kibaoni ndizo zenye vyanzo vizuri vya maji

na wanapata angalau maji safi na salama. Naomba katika Kata ya Chamalendi sina maji kabisa katika vijiji vya Maimba, Mkwajuni na Chamalendi yenyewe, na Mwamapuli katika vijiji vya Lunguya, *Centre Pinda* na *Centre Clara*. Mheshimiwa Kalobelio kama yuko hapa, vijiji vyote hivyo ninavyovitaja anavifahamu kwa sababu aliwahi kuwa Mkurugenzi wangu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaombeni sana, sana, naomba Chamalendi mnipatie maji ya kutosha na visima. Sina maji kabisa kule, watu wanatumia maji yanayoporomoka katika Mto Msabya na yanayotoka katika Mto Kavuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaombeni sana, tupunguze matatizo ya wananchi wangu wa Kata ya Chamalendi, Mwamapuli ambao kila siku wamekuwa wakipigizana kelele na Askari wa *TANAPA*. Kwa hiyo, nawaomba sana, sana, tuondoe hiyo adha ya wananchi wale kugombana na *TANAPA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikirudi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 23, mmeongelea uamuzi wa ujenzi wa mabwawa ya kimkakati. Niliwahi kuuliza hapa masuala ya umwagiliaji yako wapi? Hayaongelesi siku hizi huku. Nina umwagiliaji Kirida, nina umwagiliaji Mwamapuli, ambapo Mwamapuli mwaka 2017 mlitutengea hela ya upembuzi yakinifu kupitia Wizara ya Maji, lakini mpaka sasi sioni kinachoendelea. Ni mradi mkubwa na mradi wa Mwamapuli mliuondoa kwenye Halmashauri mkaupeleka kwenye mikakati ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa wangu Waziri wa Nchi uko hapa, wananchi wangu wale wana mashine na mitambo mikubwa ambayo takribani ina miaka saba haifanyi kazi kwa sababu hatuwezi kuendelea na kilimo kwa ajili ya mvua zilizoharibu ile mitambo. Nimesema ni umwagiliaji Kirida pamoja na Mwamapuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea hivyo najua utanijibu hicho kilimo, lakini ni masuala mtambuka; na utanijibu hicho kilimo kwa kunikwepa tu, lakini katika ukurasa wa 23 mmeandika kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji umeme. Katika kilimo cha umwagiliaji ndiyo nimeweka mradi wa Mwamapuli pamoja na wa Kirida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye uzalishaji umeme, nilimwomba Mheshimiwa Prof. Mbarawa aweze kukutana na Mheshimiwa Dkt. Kalemani waangalie ni namna gani tunaweza tukazalisha umeme katika Kata ya Majimoto, kwenye chanzo chetu cha Majimoto pale. Kwa hiyo, naomba pamoja na hii mipango mliongoyandika humu, basi na Majimoto mpafikirie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi katika mradi wa kutoa maji katika Ziwa Tanganyika. Nimeona kabisa kwamba upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii imeshafanyika. Tunasubiri nini sasa kuanza kufanya usanifu wa kina ili tupeleke fedha kule? Kwa sababu haya maji ninaamini yanakuja mpaka kwenye Halmashauri yangu ya Mpimbwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wangu wa kule tatuwapunguzia adha ya kupata haya maji. Kwa hiyo, naomba tu, ni lini mtaanza kufanya huo usanifu wa kina ili tuweze kuanza mara moja namna ya kutafuta fedha kwa ajili ya kutoa maji Tanganyika kupita Karema, Mpanda, Kavuu na kufika Mpimbwe kabisa kule Jimboni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, naomba niongelee suala lingine. Pamoja na kwamba nimeshaongea mambo ya Jimboni kwangu sasa naomba niongee kama mwananchi ninayetoka Mkao wa Katavi. Naomba niongelee kuboresha mfumo wa maji katika Mji wa Mpanda, nimeona kuna fedha pale imetengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mradi wa Ikorongo, una miaka kadhaa, maji Mpanda ni tatizo. Ni mji pale, ni tatizo, ni tatizo ni tatizo, naomba litatuliwe. Wananchi

wamekuwa hawataki kulipa *bill* kwa sababu tu maji wanapata mara moja kwa wiki; kwa sababu tu maji yanatoka mara moja kwa wiki. Huyo mtu akifanya mahesabu yake kwa *bill* na lita alizotumia, lazima atakukatalia kulipa *bill*. Mtaanza kuwakatia maji, mtagombana bila sababu za msingi. Kwa hiyo, naomba hilo pia mliangalie vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala moja ambalo kwa mimi binafsi naona kama ni kero; ankara kutolewa kwa njia ya kielektroniki, yaani kwenye simu. Kwanini tusitoe karatasi pamoja na meseji kwenye simu? Kama mimi mwenye simu nimesafiri, basi nyumbani pale inabaki karatasi wale watu wanalipa *bill*, na siyo muda wote mtu atakuwa na simu mkononi kuangalia *bill* yangu imeingia ya maji ya mwezi huu, kwa hiyo lazima niende nikalipie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naowaomba mfanye utaratibu; na hizi ni Kanuni, siyo kwamba ni amri za Mungu. Hizi ni Kanuni tu tunatunga. Kwa hiyo, huo utaratibu mimi nimeona una malalamiko na una matatizo. Kwa hiyo, ni vema sasa mkatoa karatasi na pia mkatumia hiyo njia ya kielektroniki. Siyo muda wote watu wana simu kama hizo na nimekuwa nikisema kila wakati, kwa hiyo, nilikuwa nawaomba pia mwangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Oman ambayo imeleta mradi wa kuchimba visima 100 kwa shule za sekondari. Mimi kwangu sijaona hata shule moja. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, nipatie sekondari hata mbili tu; au shule za msingi hata tano tu ili wale watoto kule wapate maji. Sina maji katika shule hizi. Sina maji katika shule za msingi wala za sekondari. Kwa hiyo, nawaomba, nipatiensi hata visima viwili tu vya sekondari, vitano nipe vya shule ya msingi; vingine nitakuwa naomba pole pole angalau wanafunzi wangu wapate kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni mwalimu, nikienda naingia darasani kufundisha. Nikitoka natafuta kidumu cha mwanafunzi kiko wapi ndiyo ninawe maji chaki. Sasa hii siyo nzuri, naomba tupate angalau usawa.

Kwa nini maeneo mengine yapelekewe hivi visima, maeneo mengine hayapati? Nataka tujue, mtakapokuja nawaomba kabisa katika hili mwangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la miundombinu. Wakandarasi wamekuwa wakinunua vifaa ambavyo siyo vizuri ni vibovu. Mpira badala ya *class C*, sijui mnatuletea mpira gani. Mwananchi au Mwenyekiti wa Kamati ya Maji Kijijini anajua huu mpira ni *class C?* Hiyo nayo iangaliwe.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia, malizia Mheshimiwa.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Maombi yangu naomba yachukuliwe kama nilivyoyaleta kwako Mheshimiwa Waziri na ninaunga mkono hoja ili nipate maji. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimwa Kitandula, jiandae Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia uzima na sisi wote leo tuko hapa tukiwatumikia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Wizara kwa kutupatia fedha za maji. Mwaka 2018 tulitengewa shilingi bilioni 1,400, tumepata shilingi milioni 960, tunazungumzia takribani asilimia 67. Nawashukuru sana. Wakati nikishukuru, nikumbushe tu kwamba kuna kiporo cha shilingi milioni 461, tunategemea fedha hizi zitapatikana ndani ya kipindi cha mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikisema hayo vilevile natambua katika bajeti ya mwaka kesho tumepangiwa shilingi bilioni 1,139 kwa ajili ya miradi ya kule Mbuto,

Mwakijembe, miradi miwili ile ambayo ili ikamilike tunahitaji shilingi bilioni 2,300. Hii maana yake nini? Maana yake tuna upungufu wa shilingi bilioni 1,160 ili miradi hiyo iweze kukamilika. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye kazi kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nizungumzie tatizo la maji katika nchi yetu kwa ujumla. Nilikuwa nasoma taarifa ya *World Bank*, inaitwa *Reaching for SDG The Untapped Potential of Tanzania Water Supply Sanitation and Hygine Sector* ya mwaka 2018. Taarifa inatuambia kwamba takribani Watanzania milioni 20 hawapati maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposikia jambo hili, siyo jambo zuri hata kidogo. Kwa vigezo vyovoyote vile, haiwezekani kama nchi tukaona Watanzania milioni 20 hawapati maji safi na salama halafu tukaona ni jambo la kawaida, lazima tuchukue hatua. Hapa ndipo linapokuja suala hili sasa kwamba lazima tutafute maarifa mapya ya kuhakikisha kwamba kama Taifa tunatoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili liliazimia, moja ya maarifa iliyotumia Bunge ni kuongeza fedha za Mfuko wa Maji. Najua wenzetu wapo wanaosema kwamba tuklongeza kule tunaweza ku-*trigger inflation*, lakini *statistics* zinatuonesha kwamba kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita tumeweza ku-*control inflation*. Kwa mwaka huu ndiyo tumeweza kupata kiwango kikubwa sana cha *inflation* iliyochangiwa na Sekta ya Usafirishaji, maana yake mafuta yako humu. Wakati tumefikiwa kiwango hicho, bado *inflation* yetu ni asilimia 3.1. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Hii maana yake tusijifiche kwenye kichaka cha *inflation*, bado tuna *room* ambayo tunaweza kufanya tukatumia Sekta hii Mafuta kupata fedha za maji na hatimaye tukaondoa tatizo hili kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la maji ni kubwa vilevile Mkinga; na hili nimekuwa nikilisema mara kwa mara. Mkinga imegawanyika katika maeneo mawili, kuna eneo la milima na ukanda wa Pwani. Maji yanayotumika katika Mji wa Tanga, chanzo chake ni Mkinga, katika Kata ya Bosha na katika Kata ya Mhinduru. Tangu kuumbwa kwa dunia watu wa Kata hizi mbili hawajawahi kuona maji ya bomba. Hii haiwezi kuwa sawa hata kidogo. Watu wale wamejitalidi kuhakikisha wanalinda vyanzo vya maji. Maji yale yananyewa Tanga Mjini, wao hawana huduma ya maji. Haiwezi kuwa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikileta maombi, Halmashauri tumekuwa tukileta maombi kwamba tujenge miradi ya maji kwenye maeneo yale, tumekuwa hatupati majibu. Mwaka huu tumeleta maombi, tunahitaji shilingi bilioni nane ili maeneo katika Kata ya Mhinduru, eneo la kwa Mtiri, Churwa, Muheza, Mhinduro, Bamba, Mazengerero, Kichangani na Segoma na vile vile maeneo ya Bosha, Kuze, Kibago, Bosha, Kwamtindi na Buzi Kafishe yaweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wapeni maji watu hawa, ndio wanaotunza vyanzo vya maji vinapeleka maji Tanga, ndio wanaotunza vyanzo vya maji vinavyopeleka maji sasa Muheza wao hawana maji safi na salama, haiwezi kuwa sawa hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la pili ni ukanda wa Pwani. Ukanda wa Pwani hatuna Mito, tungetegemea tupate maji kwa kuchimba visima, lakini kila visima tunavyochimba, chumvi inakuwa ni nyingi mno, kwa hiyo, maji yale hayafai kwa matumizi ya binadamu. Sasa wakati ikiwa hivyo nataka mwelewe kwamba Watanzania wenzenu wanakunywa maji yasiyo safi na salama kwa sababu tu tumeshindwa kuapelekea maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja Mheshimiwa Kamwelwe akawaahidi watu wale kwamba suluhisho la tatizo

lile ni kutoa maji Mto Zigi kuyapeleka kule. Maji yale leo hayajapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule uliambiwa utengenezwe ili wananchi wa Mkinga wapate maji, nimeambiwa Wizara ilitoa tangazo la mradi ule, amepatikana Mhandisi mwelekezi, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea. Tangu mwezi wa Kumi nasikia Mhandisi amepatikana, lakini kuna majadiliano yasiyoisha juu ya mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, nimeangalia vitabu hivi vyta bajeti, mradi ule haupo. Hivi mnataka watu wa Mkinga tukapate wapi maji? Mheshimiwa Waziri alikuja mpaka Horohoro akaiona kadha ile, watu wetu wanaenda kuchota maji Kenya. Tuondoleeni aibu ile. Aliwaahidi watu wale kwamba tutapata mradi wa maji wa *quick-win*. Aliagiza watu wa Tanga, *UWASA* walete mapendekezo; nimeambiwa mapendekezo yako Wizarani kwake, tunaomba fedha hizo ili tatizo lile liweze kuondolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua, amefika Mkinga, Makao Makuu ya Wilaya hayana maji. Hivi tunakuwaje na Wilaya ambayo haina maji? Tuna mradi pale wa ubabaishaji tu, tunatoa maji kutoka kwenye Kijiji jirani ndiyo ki-save Makao Makuu ya Wilaya. Hii haiwezi kuwa sawa. Tusaidieni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema jambo hili tangu Mzee Maghembe ni Waziri, ameondoka Mheshimiwa Prof. Maghembe wamekuja wengine, sasa uko wewe, imani ni yangu ni kwamba jambo hili litapatiwa ufumbuzi. Tusaidieni tuweze kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Mkinga ndiyo eneo lenye Ukanda mkubwa wa bahari kuliko Wilaya nyingine zote katika Mkoa wa Tanga. Kwa hiyo, tuna *potential* ya ujenzi wa mahotelii katika ukanda

ule, lakini tunashindwa kujenga mahoteli kwa sababu hatuna maji. Mahoteli yanajengwa upande wa pili wa nchi ya Kenya, upande wa Mombasa, sisi tunaangalia. Nawasihi sana, tusaidieni tupate maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakusudia kujenga kiwanda kikubwa kabisa cha uzalishaji wa cement katika nchi hii. Mapato yanayotegemewa pale ni shilingi bilioni 450 kwa mwezi. Kiwanda kile kitafanyaje kazi tusipokuwa na maji? Kiwanda kile kinategemewa kuvutia viwanda vingine 11 pale Mtimbwani, tunajengaje viwanda vile kama hatuna maji?

Mheshimiwa Waziri, tusaidieni, watu wa Mkinga wana shida ya maji, tupeni maji ili tuweze kupiga hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Makanyaga, jiandae Mheshimiwa Mipata.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii ya bajeti ya Wizara ya maji, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Raís wetu kwa kazi kubwa anazoendelea kuzifanya ambazo zinatudhihirishia na zinatupa matumaini makubwa sana kwamba mpango wetu wa kuingiza nchi katika uchumi wa kati mwaka 2025 tutaufikia bila wasiwasi wowote kwa kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa kazi zao kubwa wanazozifanya pamoja na timu yao nzima Wizarani pale. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyowasilisha taarifa yake hapa jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Maji ni kila kitu, maji ni uhai kwa binadamu, kwa wanyama na kwa mimea, maji ni uhai kwa kila kitu chenye uhai hapa duniani. Maji safi na salama ni afya. Maji safi na salama ni afya kwa binadamu. Kwa mpango wetu tulinao wa kuivusha nchi yetu kuipeleka kwenye uchumi wa katika tunahitaji watu wenye afya njema. Bila maji safi na salama itakuwa ngumu kufika huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nichukue nafasi hii niipongeze mipango mizuri sana ya Wizara ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri jana ambayo iko kwenye kitabu hiki imejieleza kwa uzuri sana. Tumeona kuna mipango inazungumzia ujenzi wa mabwawa ya mikakati. Mabwawa ya mikakati yametajwa hapa, moja kati ya mabwawa hayo liko bwawa la Farkwa lilioko Chemba hapa Dodoma. Bwawa hilli linakusudiwa pamoja na mambo mengine liweze kuwa chanzo kikubwa cha matumizi ya maji hapa Jijini Dodoma na viunga vyake vyote, Wilaya ya Bahi, Chamwino na Wilaya ya Chemba yenye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia jinsi watu wanavyo-*flow* Dodoma sasa hivi, ukizingatia sasa ofisi zote za Wizara zote, Serikali nzima sasa iko Dodoma, sasa wako Mtumba, hata wale wachache waliokuwa wanazembea zembea, wanategea tegea kuja Dodoma sasa hawana namna inabidi waje. Mji huu utafurika watu sana muda sio mrefu. Maji yako wapi? Maji ya Mzakwe, sawa! Hadi wakati huu bado yanajitosheleza, lakini kwa *flock* ya watu itakayokuja muda sio mrefu tutaanza kulia tatizo la maji. Kwa hiyo niombe sana Wizara waangalie sana suala zima la kukamilisha miradi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ukarabati wa mabwawa ya zamani. Yako mabwawa ya zamani na yametajwa kwenye kitabu hiki ukurasa wa 56, kati ya mabwawa hayo, yako mabwawa ya Dodoma, liko bwawa la Ikowa ambalo liko Wilaya ya Chamwino na liko bwawa la Buigiri ambalo pia liko Wilaya ya Chamwino. Mabwawa haya awali kama ilivyo leo kwenye kitabu yalijengwa kwa maana

ya kudhibiti mafuriko lakini tulivyoendelea hivi kuja kilimo chetu kimekuwa shida mabwawa haya yamekuwa yakitumika sasa kama ni chanzo kikubwa sana cha kilimo cha umwagiliaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa hayo sasa yameingia shida. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Wizara nzima kwa ujumla lakini Waziri aliye pita *Engineer Kamwelwe* alipata nafasi akatembelea mabwawa ya Buigiri na mabwawa ya Ikowa akayatolea kauli kwamba mabwawa haya yata shughulikiwa ili watu wa endelee kufaidi na kunufaika na mabwawa yale kwa kufanya kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, mpaka sasa kimya! Tatizo tunaweza kuwa tunalijua, ndio hapo tunaposema, tusione shida wakati mwingine, ni kweli kunaweza kuwa na ujisadi wa watu kuhujumu fedha za umma kwenye miradi ya maji, lakini sio kila sehemu na ukiangalia sehemu kubwa sana ni ukosefu wa fedha kufika kwenye maeneo husika. Fedha za maendeleo hazifiki jinsi zinavyopangwa, shurti zingefika hata hizo kidogo, basi tusingekuwa hapa tulipo leo. Suala hili tunaomba Wizara ihakikishe inakamilisha miradi yake mapema inavyowezekana ili watu waweze kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti na uchimbaji wa visima mbalimbali ni jambo zuri sana. Hii ni mikakati mizuri ambayo tunasema Wizara yetu imekuja nayo na tunaomba mikakati hii basi itekelezeke kweli kweli. Katika mikakati hii, katika utafiti na uchimbaji wa visima hivi bahati nzuri na wilayani kwangu, Wilaya ya Chamwino, tume pata visima 14. Katika visima 14, visima nane viko kwenye Jimbo langu la Chilonwa. Pamoja na visima hivi nane vilivyo chimbwa juzi, leo hivi nazungumza nina visima 20 katika Jimbo la Chilonwa peke yake ambavyo vimechimbwa, sawa, maji yamepelekwa maabara yameonekana yako safi na salama kwa matumizi ya binadamu lakini maji bado yapo chini, hakuna *pump*, hakuna chochote, tunamaliza miaka miwili. Sasa watu wanafika mahali fulani, kama sisi wa CCM tunasema utekelezaji wa Ilani, Ilani ya CCM ndio inavyotuambia sasa wameNtuchimbia maji wanasesma maji yako chini, yako wapi? Tunayataka maji tuyatumie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niombe sana suala zima la kuiomba Wizara ihakikishe kwamba miradi yote iliyowekwa hapa itimie, ikamilike ili wananchi waweze kufaidi matunda ya kazi ambazo zinafanywa sasa. Nichukue nafasi hii mimi niunge mkono wale ambao wana hoja ya kusema maamuzi yetu tuliyoyafanya vikao vyta nyuma kwamba tupate Sh.50 toka kwenye mafuta ili iweze kusaidia Mfuko wa Maji wa Taifa naliunga mkono kwa kweli, kwa sababu naamini hilo linaweza kusaidia upatikanaji wa fedha ili kuweza kutatua matatizo haya ya miradi isiyokamilika kwenye maeneo yetu mbalim bali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, kwa nafasi hii tena niseme naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini naomba sana ukamilishaji wa miradi hii ufanyike mapema. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Desderius Mipata, jiandae Omari Kigua.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana jkwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Maji. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima na niende moja kwa moja kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uchapakazi. Wametutembelea kwenye wilaya yetu, lakini pia wametutembelea kwenye majimbo yetu yote mawili, tumeona mchango wao na umetusaidia sana. Nipongeze watendaji wa Wizara, wanatusikiliza vizuri na tunaomba waendelee kutusikiliza sisi wawakilishi wa wananchi pale tunapowapelekea maelezo sahihi juu ya miradi ambayo inatekelezwa kwenye majimbo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na miradi mitatu ya Benki ya Dunia. Mmoja ni Mradi wa Kisura, Mheshimiwa Naibu Waziri aliutembelea mradi huu lakini mpaka sasa wananchi hawajapata maji. Alipokuja, tunakushukuru sana aliweza kutusaidia tukapatia milioni 150 na mradi umejengeka umekwisha. Kinachotakiwa sasa ni nishati tu, sasa kile kijiji kinapata umeme lakini Wizara

wametupendekezea tununue *generator*, sasa *generator* haiwezi kutusaidia kwa sasa, tunaomba hilo tusifikirie, wabadirilishe mawazo ili umeme unaokuja pale watusaidie pesa tufunge mashine pale tupeleke umeme kwenye chanzo, itatusaidia sana. Ni kisima ambacho kinatoa maji mengi na ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili, ni Mradi wa Mpasa. Mradi wa Mpasa una maneno mengi, lakini naomba wanisikilize vizuri. Mradi ule unaenda vizuri na uko asilimia 80. Wamejenga miundombinu mizuri kabisa na unaenda vizuri kiasi kwamba unatia moyo na wakati mwingine tukiwaharibu watu wakati wana spidi nzuri ya utekelezaji tunawavunja moyo, uko asilimia 80, wamejenga matenki yote, sasa hivi wamejenga *DP* karibu zote. Sasa hivi bado kuunganisha tu kidogo kutoka kwenye njia kuu kupeleka kwenye vijiji. Pale ndiyo wamepata hela kidogo, tena itakuwa *certificate* ya mwisho na utakuwa umekwisha kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yanapokuwa maneno mengi mara nyingi mradi huu unakwama wanachelewa kutupa pesa na wametuma tume nyingi kama tatu au nne, hawatuamini tukisema kwamba unaenda vizuri, *DC* yupo, Mkuu wa Mkoa yupo na anafuafilia vizuri na mimi nipo. Kwa hiyo watuelewe vizuri, mradi huu unaenda vizuri. Sisemi hivi kwa kumpendelea mkandarasi, hapana, lakini mradi unaenda vizuri na spidi iko vizuri na mimi ndiyo nauangalia kwa karibu. Ulikuwa na matatizo na matatizo yanaweza yakawepo ya kawaida kama sehemu nyingine, lakini spidi ya mradi huu ni nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mradi wa Isale; mradi huu pia Mheshimiwa Waziri amekuja kuutembelea, ameuona jinsi unavyokwenda, tunamshukuru Mungu unaenda vizuri, mpaka sasa uko asilimia 50. Mradi huu ni wa shilingi bilioni tano na milioni mia tano, ni mradi mkubwa. Mkandarasi amejenga asilimia 50 mpaka sasa na amepokea shilingi bilioni moja na milioni mia moja na sasa wamempelekea milioni 400, kazi inaenda vizuri. Mheshimiwa *DC* pale anasimamia vizuri, ameshirikisha vijiji vile vya jirani, wanachimba mitaro,

wanapata visenti kidogo pale na vinasaidia kwenye miradi ya vijiji. Kwa hiyo mradi huu nao unaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia mradi huu upeleke maji Nkata, upeleke maji Kitosi, Ntuchi A na Ntuchi B pamoja na Ifundwa, pamoja na Isale na Msilihofu. Kutakuwa na kakijiji kamoja kamebaki hapa China, nilimwambia Mheshimiwa Waziri alipokuja kwamba wataalam wanasema kwamba *design* haioneshi kwamba maji yale yanaweza yakaja pale, pana mwinuko, naomba kwa sababu ndiyo bomba linapita kwenye Kijiji hicho cha China, atufanyie utaratibu wa kisayansi utakaowezesha watu wale wapate maji, bila hivyo miundombinu inaweza ikahujumiwa jambo ambalo litatupa shida sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwiningine ni Mradi wa Nkundi. Bwawa la Nkundi, la Kala Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri walilitembelea wakaona changamoto zilizokuwepo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri juzi ametoa uamuzi, ametuletea milioni 65 na sasa hivi ninavyosema nilitembelea pale nimekuta wameweuka umeme tayari, kwa hiyo nishati ile iliyokuwa inasuasua sasa tatizo lile litakuwa limekwisha. Nina imani kama kikwazo kilikuwa ni nishati, mradi huu sasa wananchi wataanza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa naongea na *Engineer*, wananchi wa Kalundi wameanza kupata maji lakini Nkundi kuna tatizo, bado maji hayafiki. Sasa inaelekea Nkundi hapa kuna shida katika *BOQ*, inawezekana ujenzi wa *BOQ* haukizingatia *design* ya Wizara katika ujenzi wake. Nimewahi kusikia fununu hii kwamba mkandarasi atakuwa aliwarubuni labda vijana wetu, wakaweka *BOQ* ambayo haikuwa imependekewa na Wizara ili maji yaweze kufika pale, kwa sababu kuna mwinuko, wamepeleka bomba jembamba, sio kubwa, *design* ya Wizara inasema bomba linalotakiwa kuanzia pale kwenye chanzo mpaka kule liwe ni inchi tano, sasa nasikia wamepeleka tatu, kwa hiyo maji yanafika kwa shida na wakati mwiningine una-pump siku mbili, tatu ndiyo maji yafike, hayawesi kukusaidia. Wafuatilie kwa makini kama

Mheshimiwa Waziri alivyokuja wakati ule akafuatilia na Mkuu wetu wa Mkoa yuko makini sana, ataweba kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mwininge wa maji wa Wampembe. Wampembe ni Makao Makuu ya Tarafa na kuna mwinuko na chanzo kizuri cha maji ya kutiririka. Wataalam wangu wamefanya utafiti wakasema kwamba wametoa mapendekezo Wizarani japo hawajafikisha hapa, tunaomba wataleta mapendekezo hivi karibuni, tukipata ule mradi uthisha vijiji karibu vitano na ni maji ya mteremko. Awali halmashauri ilikuwa imefunga huo mradi, miundombinu yake ikafa, ukifufuliwa utakuwa umetusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa mwisho ambao nafikiri utatusaidia ni wa Kijiji cha Chonga; Kijiji cha Chonga kinakosa maji. Wataalam wangu wameleta mapendekezo hapo na inaonekana kwamba shillingi millioni 300 ndiyo zinatakiwa ili kijiji hiki kiweze kupata maji. Tayari miundombinu kama tenki lipo, limeshajengwa muda mrefu, ni njia tu ya maji kutoka pale Kijiji cha Nchenje kuja Chonga kama kilometra nne hivi, lakini tenki lipo na linaweza kufanya kazi vizuri.

Naomba kwa unyenyekevu mkubwa na uchapakazi wao wanaisaidie nipate shillingi millioni 300 ili mradi uweze kufanya kazi. Niwatoe wasiwasi, pesa za maji pia zinasimamiwa Wilaya ya Nkasi, si vile kama zinapotea potea, maana wanakuwa na wasiwasi na wakati mwininge, haziji kwa wakati, wanaunda tume nyingi nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wakati fulani *DC* yupo, Mkuu wa Mkoa yupo, Usalama wa Taifa wapo, *PCCB* wapo, wote wapo ni watu wanaoangalia miradi ya Serikali. Hakuna mtu ambaye atakaa tu pesa zinapotea bila kuangalia, hili tuliangalie sana, lisitie Wizara kigugumizi cha kutuletea pesa Wilaya ya Nkasi. Zinasimamiwa na sisi wenye Mwenyekiti wa Halmashauri yupo, Mkurugenzi yupo, wote tunasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, mchango wangu ni huo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omari Kigua, hayupo, Mheshimiwa Qambalo, jiandae Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Maji ni hitaji la msingi na ni haki kwa kila mtu, kwa hiyo tunapochachamaa na kudai huduma hii muhimu ya maji tunadai jambo ambalo ni la msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na miradi ya maji ambayo inajengwa chini ya kiwango. Mwaka jana wakati tupo kwenye hotuba kama hii, Wabunge wengi walitaka kuazimia Tume huru ya Bunge ili kwenda kuchunguza mingi ya maji iliyojengwa siku za nyuma hasa ile ambayo iko kwenye ule mpango wa *WSDP*, lakini baadaye Wizara ikasema tuwape nafasi ya mwisho wenyewe waende wakafanye kazi hiyo illi watuletee ripoti. Sijui na sidhani mpaka leo kama ripoti ile imeweza kupatikana. Kwa hiyo naomba Wizara hii itupe taarifa ya wataaaam wao walipokwenda kukagua miradi ile, tatizo hasa ni nini ya ujenzi ule kuwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana mimi natokea Karatu, timu hiyo ilikuja Karatu, walipokuja Karatu badala ya kupelekwa kwenye miradi ambayo ina hali mbaya sana, walipelekwa kwenye miradi ambayo ina unafuu mkubwa. Ukipata Daktari Bingwa anakutembelea kwenye hospitali yako nadhani namna bora ni kumpeleka kule kwenye wagonjwa walioko *ICU* sio kwa wale wagonjwa wa nje wanaokuja na kurudi, lakini wale wataalam kwa baadhi ya maeneo walipelekwa kwenye miradi ambayo walau inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Miradi ya Vijiji Kumi kila Wilaya, pale Karatu tuna miradi 10 lakini miradi mitano kati ya 10 haifanyi kazi hadi sasa. Ukijumlahisha fedha zilizotumika ni zaidi ya shilingi bilioni nne, Mradi wa Matala, Kansay, Buger, Getamock na Mradi wa Endonyawet, miradi hiyo yote haifanyi kazi. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Karatu tukamweleza kwenye kikao cha wilaya na aliahidi kupita kwenye miradi hiyo, lakini tangu wakati ule mpaka leo

hajaweza kurudi. Jambo hili sisi Viongozi wa Wilaya limetushinda, Viongozi wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa ameshakwenda mara kadhaa imemshinda, sasa tunaomba huu mzigo hebu wakaubebe wao. Watu hawa wameiibia Serikali, wakandarasi na wataalam hawa wamewaibia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuombi fedha mpya, tunataka fedha zilizotumika, ziende zikafufuliwe ili wananchi wapate huduma ambayo ilikuwa imekusudiwa. Kwa kweli haipendezi mradi unakaa miaka saba, miaka kumi haufanyi kazi na huku wananchi bado wanahangaika na shida kubwa ya maji iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, niwaombe hili suala la miradi ya Benki ya Dunia ambayo imechakachuliwa kwa sehemu kubwa, tunaomba walivallie njuga, wafike kwenye maeneo hayo ili watusaidie kuwaleta site wale Wakandarasi waliofanya kazi hiyo, wale Wahandisi, Washauri waliosimamia lakini pia wale Wahandisi wa Halmashauri ambao na wenyewe walikuwa na nafasi kwenye kuhakikisha miradi hiyo inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la vyombo vyatua watumia maji. Naamini kujenga mradi wa maji kimiundombinu ni jambo moja, lakini jambo la pili ambalo nalo ni muhimu sana ni kuhakikisha miradi ya maji inakuwa endelevu. Kwa maeneo ya mjini tunazo Mamlaka za Maji Mijini, lakini kwa maeneo ya vijijini kwa sehemu kubwa vyombo hivi vyatua watumia maji ndivyo ambavyo vinasimamia na kuendeleza miradi hii ya maji. Vyombo hivi, vinatambuliwa katika nchi hii. Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inavitaja, hata kwenye hotuba ya Waziri vinatajwa, lakini pia Sheria mpya ya Maji Na.5 ya Mwaka 2016 pia imevitaja. Ni vyombo ambavyo tukivisimamia vizuri vinaweza vikapunguza matatizo ya maji kwenye badhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwetu Karatu tuna vyombo vitatu vinavyotoa huduma. Tuna Mamlaka ya Maji ya Mji wa Karatu ambayo imeundwa ina karibu miaka

mitano, ambayo inatoa huduma ya maji kwa asilimia 6.7, lakini tuna Bodi ya Wadhamini, chombo ambacho kimeundwa na wananchi, kilichosajiliwa kisheria ambacho kimekuwepo kwa muda wa miaka 20 na ambacho kinatoa huduma kwa zaidi ya asilimia 76 kinaitwa *KAVIWASU*. Pia tuna watoa huduma wachache, watu binafsi ambao wana visima vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naomba nieleze kwamba hivi karibuni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, barua hii hapa, ameandika barua kusitisha zoezi la kisheria la kupata wawakilishi wa wananchi ili waweze kusimamia mradi huo wao nilioutaja wa *Karatu Villages Waters Supply*. Kama kweli tuna nia njema ya kuona miradi ya wananchi inayofanya kazi, mradi wa Karatu ni wa mfano. Ukitaka kuona mradi wa *PPP* ambao pia wananchi wameusimamia kwa ufanisi mkubwa ni huo mradi wa Karatu lakini Mkurugenzi ameandika barua kusimamisha uchaguzi kwa sababu Bodi iliyokuwepo muda wake umeisha, sasa wanataka kuchagua bodi nyingine lakini Mkurugenzi anasimamisha eti kwa maelekezo kutoka juu. Eti kwa sababu Wizara sasa hivi inatunga kanuni kwa ajili ya hizi sheria mpya, hivi vinahusiana wapi na wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karatu tuna machungu, Karatu tuna makovu ya matatizo ya maji ya miaka iliyopita. Naomba msiturudishe huko. Inawezekana kwenye jambo hili kuna siasa, lakini siasa inaingia wapi kwenye huduma ya maji. Niseme tu wazi, Mheshimiwa Humphrey Polepole, Katibu Mwenezi wa CCM alikuja Karatu na ndiye aliyetao maagizo ya kusimamisha uchaguzi huo, inaumiza sana. Inaumiza sana kwa sababu wananchi mradi huo wameuendesha peke yao miaka 20 bila hata kupata ruzuku ya senti moja kutoka Serikalini. Leo zoezi la kisheria ambalo wananchi wako tayari kuendesha mradi wao, linasimamishwa kwa hisia tu za kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache niseme kwamba, mradi huo wakati wadau wa maendeleo pamoja na wananchi wameumaliza na Bodi ilipokabidhiwa miaka

20 iliyopita, walikuwa na mtandao wa bomba wa kilomita 57, leo wana kilomita 421. Wakati huo walipokabidhiwa wana vituo vya umma 37 leo wana 86. Walipokabidhiwa walikuwa na kisima kirefu kimoja leo wana visima saba. Walipokabidhiwa walikuwa na matenki 10 leo wana matenki 23. Walipokabidhiwa walikuwa na *private connections* sifuri (0) leo wana 2,661. Walipokabidhiwa walikuwa hawana mfumo wa kulipia kabla (*prepaid*) leo wana vituo karibu 15 vya *prepaid* na mambo mengine mengi. Ndiyo maana nilisema kama kuna mradi unaweza kuona jinsi wananchi wanavyosimamia miradi yao na kuiendesha ni mradi wa Karatu lakini leo mradi ule unataka kuzimika kwa sababu tu ya hisia ambazo siyo za kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo hili inasemekana limetoka ofisini kwenu Mheshimiwa Waziri, hebu niwaombe mtuache Karatu tuendeshe mradi wetu kwa namna ambayo tunaweza. Wananchi wako tayari, fomu za kugombea wamechukua lakini sasa zoezi limesimama na matokeo yake hata mishahara ya watumishi hawawezi kulipa kwa sababu wale watendaji wamebaki wenyewe, wale wawakilishi wa wananchi kwa maana ya Wajumbe wa Bodii hawapo. Leo hata madeni ya maduka ya vifaa hawawezi kulipa kwa sababu ya kusimama kwa zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa vile inasemekana jambo hili limeanzia kwenu naomba mruhusu wananchi wa Karatu na vijiji vya jirani waweke viongozi wao. Kama kuna matatizo mengine, hata muende mkaautembelee na mtaona, Naibu Waziri nashukuru ulikuja Karatu lakini hata ulivuyokuja, hata kuambiwa kwamba kuna mradi unahudumia asilimia 76 ya maji katika Mji wa Karatu na vijiji vya jirani haukuambiwa. Kwa hiyo, ujue katika sura hiyo jinsi ambavyo kuna tofauti na harufu ya kisiasa kwenye jambo hili. Kwa hiyo, naomba kadri itakavyowezekana...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta halafu Mheshimiwa Omar Kigua, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Timotheo Mnzava wajialande.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hoja iliyo mbele yetu ya bajeti ya Wizara ya Maji. Mimi ni mjumbe wa *LAAC*, kwa hiyo, tunapata nafasi kubwa ya kutembelea miradi mbalimbali ili tuweze kuona utekelezaji wake lakini pia na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi kuna mtu mmoja alichangia kwa jazba akasema kuna mambo ya hovyo hovyo yanatendeka katika miradi hii ya Wizara ya Maji. Mimi labda nisitumile neno hilo, niseme katika miradi ya maji kuna mambo makubwa sana ya usanii na Mawaziri ninyi hamuwezi kufika kila mahali, kwa hiyo, tunapotoa mawazo yetu, hatuna maana kwamba tunawachukia au tunafanya mambo ya kisiaza hapa, tunatembea tunaona ni namna gani miradi ya maji inavyotekelawa ndivyo sivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi labda niulize, kuna nini kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Maji na Halmashauri zetu? Hii miradi ya nyuma yote ilikuwa ina-*originate* Wizarani. Ina maana Wizara walikuwa wanatoa Mhandisi Mshauri, Mkandarasi, kule Halmashauri wala hawakuwa *answerable* na miradi hii. Walichokuwa wanafanya Wizara ya Maji wanaleta Mhandisi Mshauri ambaye anakuja kufanya uoembuzi yakinifu ambavyo sivyo. Matokeo yake atasema hapa kuna maji, halafu yule anayekuja kuchimba maji anakuta hayapo, ameshakula fedha ameondoka na miradi mingi sana ya maji ina fedha nyingi, ni ya mabilioni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya mwaka ya *LAAC* tulipendekeza kama alivyosema Mheshimiwa aliymaliza hapa kwamba iundwe Tume iende itazame miradi hii, iangalie ni miradi gani ambayo haikufanyika kwa ufanisi lakini pia mjue gharama zilizotumika. Inawezekana

hamna ukakika hata wa gharama zilizotumika katika miradi hii. Ni jambo la kusikitisha kwa sababu Watanzania wanalipa madeni ya miradi ambayo haina ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitembelea miradi, hawa watu wa Idara ya Maji, wakishapata taarifa kwa mfano Kamati ya *LAAC* inakuja maji yanatoka kesho yake. Tukifika, wananchi wanatuambia Waheshimiwa Wabunge mmekuja na maji na mtarudi nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi mingi ambayo imetengenezwa haifuati hata *BOQs*. Kwa mfano, tumekwenda katika mradi mmoja huko Ngara, tumekuta wametengeneza tenki ambalo *BOQ* inasema watatumia matofari ya *block*, wao wametumia mawe na wamejenga tenki ambalo walipoweka maji likanza kuvuja. Halafu mtu anakwambia mradi umekamilika. Miradi ya namna hiyo ni mingi sana katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe mchunguze miradi hii, acha hii miradi mipya ambayo inatengenezwa sasa hivi, hii miradi ya nyuma yote imekaa hovyo hovyo. Wananchi hawapati maji ni uongo na Wahandisi wanadanganya na mahali pengine hata Wahandisi wenyewe ambao kwa kweli wana ujuzi wa kuendesha miradi hii hawapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda mahali pengine unakuta wametengeneza miradi chini ya viwango, anaweka mabomba ambayo ni tofauti. Mimi siyo mtaalamu wa mabomba ya maji lakini wataweka mabomba membamba, wakipampu maji mabomba yote yanapasuka. Kwa hiyo, hiyo ndio hali halisi iliyoko *on the ground*. Kwa hiyo, tunaomba mhakikishe mnachunguza miradi hii kama Kamati ya *LAAC* tulivyopendekeza na wengine ndani ya Bunge *from there* mtawenza kuona ni miradi ipi inakwenda vizuri, ipi ambayo imetengenezwa kiusanii na gharama ni ipi, muweze kutambua kwama nchi hii imeingia katika ujisadi mkubwa kwa kupitia miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda Serikali haina vipaumbele, nawaomba tuhakikishe maji tunayaweka katika *priority*. Watanzania wanateseka, inawezekana sisi tunakaa mijini, mkienda kule vijiji ni mtaona watu wanavyo-suffer kusema ukweli, utawahurumia watu hawaogi. Wanawake wanalamika, maisha hayaendi vizurio ndani ya familia, kama hamuogi mnakaaje? Hili jambo ni *serious*, tunaomba Waziri na Serikali ihakikishe maji ambayo watu wamesema maneno mengi, ni uhai na kadhalika kwamba miradi yote inatekelezwa na wananchi wa Tanzania wanapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee kuhusu vyanzo vya maji vijiji ni. Nina uhakika kwamba Serikali haiwezi ku-supply maji kwa kila mtu Tanzania hii lakini iko mito ambayo ni vyanzo vya maji ambapo kutokana na shughuli za binadamu imekufa. Kwa mfano, katika mkoa wetu sisi yako maeneo mengi watu wanapanda miti na wengine ni wanasiaya, wanapanda miti wanaharibu vyanzo vya maji, kwa hiyo, huwezi kupata mito ambayo inatoa maji mazuri. Kwa mfano, Mkoa wa Kagera, tunayo mito mizuri ambayo inatoa maji mazuri, lakini yote imekufa.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba wanaoangalia vyanzo vya maji ni watu wa mazingira, tunaomba na Wizara ya Maji isaidiane na Wizara hiyo pamoja na TAMISEMI kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji na mito zile chemichemi zinalindwa ili kuweza kusaidia watu wa vijiji ambao inawezekana wasipate huduma ya maji ya bomba ambayo tunaiongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la kuongeza fedha katika mafuta. Ni kweli tulipitisha miaka mitatu na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Chenge, hatukatai kukata hiyo shilingi 50, je, *implementation* yake itakuwaje? Hata za REAhaziendi zote. Kama miradi ya REA fedha mnaziweka kwenye Mfuko Mkuu mnafanya mnavyotaka, maana Serikali hii ya CCM sasa hivi hata bajeti hamuiheshimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapitisha bajeti hapa, tunatengeneza na sheria zile zinazofuata pale za kutekeleza bajeti lakini hata wakati mwingine haifuatwi.

WABUNGE FULANI: Wakati wote.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Wanasema ni wakati wote. Kuna miradi mikubwa mingine hatusemi ni mibaya, lakini je ilikuwa katika bajeti na kama inakomba fedha zote, zile fedha ambazo zingeweza kuhudumia jamii ya Watanzania zitatoka wapi. Je, mnatuhakikishiaje kwamba zile fedha zitakuwa kwenye mfuko wake ili wananchi wawewe kupata maji. Maana Watanzania wanapojojitelea kukatwa shilingi 50, ujue kwamba unawaongezea na gharama nyingine. Watakatwa ya maji, wanakatwa ya umeme, wanapenda kuleta maendeleo yao lakini fedha zitapelekwa kule ili miradi iweze kutekelezeka? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sipingani na hilo lakini lazima kama Wabunge tuhakikishe kwamba hizi fedha zinakwenda kutekeleza jambo ambalo sisi tumelipanga hapa. Sasa Serikali imekuwa haiheshimu Wabunge na Bunge na sisi Bunge tumekuwa na kauli za naomba, jicho la huruma, jicho la huruma gani, *we want the government to do it!* Tunaitaka Serikali itekeleze miradi hiyo kwa sababu tunalipa kodi na kodi zinakusanywa, hatuwezi kukaa kubembelezabembeleza jicho la huruma, jicho gani, Serikali tunaiombaomba, tunaomba jicho la huruma, ndiyo maana wanatufanya haya. Tuwaambie *we want the government to do this*, tunakutaka Waziri Prof. Mbawala utupe maji, siyo tunakuomba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema haya kwa sababu maji yanaumiza na mnatulipia fedha za walipa kodi tunakwenda *seriously*. Watu wanakwenda kule, wengine wanavaa hata kabtula kupanda milima, unakuta miradi ya maji mpembusi yakinifu pampu anaweka kule korogoni ambako anajua Mbunge hata wewe Mheshimiwa Jenista ukipanda kule ukitoka unakufa kwa sababu kupanda ile milima watu wengine mpaka wasukumwe. Pampu iko

korongoni halafu maji yanakwenda mlimani, yanatoka mlimani yanashuka, hayo ndiyo mambo mnayotufanyia. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, unga mkono hoja. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Kigua atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara ya Maji leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri wa Maji Prof. Mbarawa, Naibu Waziri mdogo wangu Mheshimiwa Aweso na viongozi wote wa Wizara ya Maji kwa jinsi wanavyopambana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza mdahalo huu toka tumeanza majuzi utaona kwamba kilio kikubwa cha Wabunge ni juu ya changamoto ya miradi ya Maji ambayo haikamiliki. Mimi binafsi najiuliza, tatizo liko wapi kwa sababu ingekuwa hakuna tatizo Wabunge wasingekuwa wanalamika juu ya miradi yetu,

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sababu katika hotuba yake amekuwa mkweli sana kwa kuainisha changamoto za Wizara hii. Ziko changamoto kama nne hivi, mojawapo ni upatikanaji wa fedha. Mimi hii siwezi kumlaumu Mheshimiwa Waziri, hata kidogo, kwa sababu mambo mengine ni ya kiserikali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zaidi changamoto namba mbili ambayo inasema uwezo mdogo katika usimamizi wa miradi. Hapa ndipo kwenye tatizo na

Iazima nikubali na tukubaliane kwamba hapa pana *syndicate*, kuanzia Halmashauri mpaka Mikoani. Wahandisi hawa tunaowapa miradi, mimi Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, nimeona pana mabadiliko katika Wizara pale lakini hili zoezi iazima liende mbali zaidi ikiwezekana unda timu ndogo ianzie kwenye malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba kwa nini miradi inalalamikiwa, kwa nini kuna ujisadi kwenye miradi, utakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuweza kujua sababu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu na nitamwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake watafute ripoti moja tu ya *CAGambayo* inahusu *performance audit* kwenye miradi ya maji. Ukiipitia taarifa moja utapata picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuanzisha *RUWASA* kwamba ma-engineerwale wa Halamashauri moja kwa moja watawajibika Wizarani lakini inawezekana ikawa ni mvinyo wa zamani kwenye chupa mpya. Watu ni walewale na utaratibu ni uleule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa aliyekuwa Waziri wa Maji alianzisha utaratibu wa kufuatilia miradi ya maji kwa kutembelea Tanzania nzima kuangalia *status* ya miradi ya maji. Kuonyesha pana *syndicate* kubwa, siku moja wakati Wizara imeltwa kwenye Kamati ya *PAC* nilimwambia Katibu Mkuu Profesa kwamba vijana wako hawakufika Kilindi na maafisa pale Kilindi wakasema hawa tumekutana nao Handeni tu, hawakufika. Kwa hiyo, taarifa kuhusu miradi ya maji Kilindi ni ya uongo. Hii ndiyo kuonyesha kwamba pana *syndicate* kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefanya ziara Jimboni Kilindi alijionea hali halisi ya changamoto ya maji na nikakuomba kwamba Kilindi haitofautiani na Handeni Vijiji na Handeni Mjini, wao wamefaidika na mradi wa *HTM* sasa huwa mbapa leo najiuliza hao wataalamu ambao walisema kwamba mradi wa maji ufile Handeni ambayo ina changamoto sawa kabisa

na Wilaya ya Kilindi, hivi hawakuiona Kilindi? Hayo tuyaache.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia Mheshimiwa Waziri tunahitaji mradi mkubwa unaofanana na HTM kwa sababu Wilaya ya Kilindi tuna vijiji 102 na vitongoji 615 ni vijiji 30 tu kati ya 102 vyenye maji. Ili tuweze kupata suluhu ya kudumu ya maji lazima tupate mradi mkubwa kuanzia Mto Pangani ambaao uko Korogwe sawa na ambavyo watu wa Handeni wanapata. Hii itakuwa ni suluhu ya kudumu Wilaya ya Kilindi kupata maji. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uliangalie hili, najua kwa bajeti ya mwaka huu haiwezekani lakini kwa mwakani ututazame kwa jicho la tatu kwa sababu wananchi wa Wilaya ya Kilindi wana changamoto kubwa sana ya maji. Nadhani nilikuambia jambo hili, naomba nikukumbushe kuitia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikumbusha kwamba Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya mradi mkubwa wa vijiji vitatu, Vijiji vya Mtakuja na Nyamaleli lakini mpaka leo Mheshimiwa Waziri havitoi maji na uliahidi utafanya ziara kwenda kuangalia inakuwaje Serikali itoe fedha za kutosha lakini hakuna hata tone la maji ambalo linatoka pale. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kulifanyia kazi suala hili. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mheshimiwa Waziri, naomba nizungumzie namna ambavyo hizi mamlaka ndogondogo ambazo huwa hazina uwezo wa kusimamaia miradi, mathalani Kilindi na Miji mingine midogo unakuta Tanga UWASA wao wanasmamia mradi wa Kilindi, Muheza, Handeni, hii ina changamoto kubwa sana Mheshimiwa, changamoto yake ni kwamba unakuta kwamba miradi hii inakuwa ni mingi watu wa Tanga UWASA hawawezi kusimamia miradi yote kwa pamoja wakati mwingine unakuta kwamba Mhandisi au Mkandarasi analalamika kwamba watu wa Tanga UWASA hawajafika kwenye *site*, ni jambo zuri kabisa Mheshimiwa Waziri kwa sababu mamlaka yetu

haina uwezo au mamlaka hizi za wilaya nyingine hazina uwezo, lakini lazima tutazame na namna nyingine ya kusimamia ili miradi hii iweze kwenda kwa speed nzuri sana, nilikuwa naomba Mheshimiwa utazame hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linakuja pale pale kuhusu miradi hii kuna mradi huu Mheshimiwa Waziri wa Maji wa Jiji la Arusha ambao Serikali imepata mkopo kutoka *ADB African Development Bank*, ni mkopo wa dola bilioni 233.9, ukizi-cover hizi ni takribani milioni 530. Lakini nikuambie mradi ule haujaka sawa unakwenda taratibu sana, nakuomba Mheshimiwa Waziri tupia jicho pale tuisubiri ripoti ya *CAG* ije iseme kwamba mradi ule una ujisadi. Na mimi Mheshimiwa Waziri nakuomba sana hebu katika Wizara yako anzisha kitengo cha ufuatiliaji cha tathimini na ufuatiliaji *Monitory and evaluation* itakusaidia sana Mheshimiwa Waziri kujua *status* ya miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge huku tunapata mengi sana Mheshimiwa na sisi tunapozungumza hapa yapo mengi tunayasikia mradi huu wa Jiji la Arusha uangalie sana haupo katika taswira nzuri, Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla wameona kwamba Jiji lile ni Jiji la utalii lazima maji ya uhakika lakini mambo hayaendi vizuri, mimi nakuomba sana litazame hili utapata uhalisia wa kitu hichi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Mheshimiwa waziri nikuombe tena ultuhaidi kutuchimbia bwawa la kisasa kwenye Kata ya Mafisa ni eneo ambalo takribani miaka 50 wananchi wale hawajawahi kupata maji, nikushukuru sana ultupatia visima vitano, lakini kwa hali halisi ya eneo lile ni kwamba maji hayapatikani suluhu ya kudumu ya kupata maji pale ni kuchimba bwawa la kisasa kabisa katika Kata ya Mafisa ambayo ina takribani wakazi 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri ultazame hilo. Pia nikuombe tunayo Kata ya Tunguli ambayo ina wakazi takribani 10,000 sasa kuna mradi wa Kata ya Kibati ambao upo katika Wilaya ya Mvomero, ni karibia ni kilometra kumi tu. Nikuombe utume wataalamu wako wawewe

kuangalia namna waweze kutupatia maji sisi kutokea Wilaya ya Kilombero itaweza kutusaidia kwa sababu tuna vijiji vingi sana ukiangalia kwa asilimia maana yake vijiji 30 kat i ya vijiji 102 ina maana ni asilimia 20 au 30 tu ya wakazi wa Wilaya ya Kilindi ndiyo wanaopata maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri, nipongeze Taasisi hizi ambazo sizo za Kiserikali kwa kuna watu wa *World Vision*, *AMREF*, wao wamekuwa ni wadau wazuri sana, wametusaidia sana kuchimba visima kwa kweli tuwapongeze katika hili. Baada ya kusema hayo mimi naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri nikupe moyo sana, nasema naunga mkono asilimia, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Aboud, Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mheshimiwa Amina Makilagi.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja hii, pili nachukua nafasi hil kuipongeza sana Serikali kwa juhudhi na dhamira yake ya dhati kabisa katika kuwapatia watanzania maji safi na salama, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa wanavyojitoa kwao kuhakikisha wananchi wa watanzania wanapata maji na kufuatilia miradi ya maji vijijini huko iliko pamoja na Mijini, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wetu na watendaji wote kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuhakikisha watanzania tunapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, maji ni uhai, maji ni afya, maji ni uchumi na kwa maana hiyo maji yakiwa ni uchumi kilimo kinahitaji maji, ufugaji unahitaji maji, mimea, miti na sisi binadamu tunahitaji maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi nashauri Serikali iongeze fedha za maendeleo katika kuhakikisha miradi hii ya maji inafanikiwa, na katika kuongeza fedha hizo za maendeleo naungana na Wabunge wenzangu waliosema kwamba katika mfuko wa maji tunahitaji kuongeza fedha ili

tutekeleze miradi ya maji, Serikali itafute vyanzo vya mapato kuhakikisha mfuko huu unakuwa mkubwa ili kuhakikisha miradi ya maji inatekelezeka ili kufikia malengo yetu tuliojijiwekea ifikapo mwaka 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchelewa au kusuasua kwa miradi hii ya maji baadhi ya miradi ya maji imekwama kutokana na ucheleshaji ulioko bandarini kukosekana kwa misamaha ya kodi kwa vifaa vya maji. Ucheleweshaji huo unakwamisha pia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji, pamoja na hilo ucheleweshaji pia unakuwa kwenye utoaji wa vibali vya kazi kwa wataalam wa maji ambao wanatoka nje ya nchi, wanachelewa kupata vibali vya kazi kwa hivyo miradi hii inachelewa kuanza kutoka na kukosekana kwa wataalam hao. Hili ni la kufanya kazi kwa Wizara zinazohukia ikiwemo *TRA* pamoja Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuhakikisha masuala haya tunayafanya kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi kuna changamoto nyingi zinakwamisha utekelezaji wa miradi, ikiwemo upungufu wa wataalam wa maji, Wizara inahitaji wataalam wa maji wapatao 3,910. Hili ni pengo kubwa sana kwa sababu kukosekana kwa wataalam hawa 3,910 wa kusimamia miradi katika maeneo yetu mbalimbali ya Tanzania inachangia sana kukwamisha utekelezaji wa miradi hiyo na pia kusababisha kununuliwa kwa vifaa ambavyo viko chini ya kiwango na utekelezaji wa miradi ambayo iko chini ya kiwango. Naomba Serikali isaidiane kutekeleza kazi hii ya kutoa vibali vya ajira kwa wataalam hawa wa maji ili waajiriwe na wakasimamie miradi yetu ya maji vijijini huko tunakohitaji mahitaji ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukwamisha pia upanuzi wa miradi ya maji katika miradi hii ya maji kuna madeni karibu bilioni 29 ni zaidi ya bilioni 21 Mamlaka za Maji zinadai kwa Taasisi za Serikali. Hili linakwamisha sana Mamlaka za Maji, kutengeneza miradi ya maji pamoja na kutanua hiyo miradi yenyeve ya maji huko vijijini, tunaomba madeni haya Serikali itafute mbinu ya kuyalipa au kuyakata huko huko

Wizara ya Fedha ili mamlaka hizi zipate fedha zake zitekeleze miradi hii. Naipongeza sana Wizara kwa kazi iliyoanza ya kuweka *prepaid* mita ili kutatua tatiozo hili la madeni. Lakini nashauri pamoja na kuongeza hizo *prepaid* mita hizo zilizokuwepo zianzwe kufungwa kwenye hizo Taasisi ambazo ni wadaiwa sugu wa maji wakawafungie huku badala ya kuwafungia wananchi, waanze na hizo Taasisi ambazo zinadaiwa mabilioni haya ya fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika miradi midogo midogo ya maji huku vijijini wananchi wanapata mzigo mkubwa wa kufidia au kulipia gharama za dizeli. Nashauri miradi hii mingi ya Vijiini ambayo ni miradi midogo midogo basi tuende na kutumia *Solar System* ambazo zitakuwa na betri zake ili hata wakati wa mvua ziweze kufanya kazi kusukuma maji katika visima hivi. Hii itapunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji, pia itampunguzia mzigo mwananchi wa chini ambaye hana uwezo au kipato chake ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri uhamasishaji wa nguvu ufanyike pamoja na kutoa elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua. Maji yetu ya mvua ni salama hayahitaji madawa, yanahitaji tu kuwekewa miundombinu ili tuyavune tuweze kuyatumia. Na katika kupanda mimea maji ya mvua yana rutuba kuliko maji mengine yoyote, hata huo ujenzi wetu uzingatie miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri uhifadhi wa vyanzo vya maji, elimu itolewe katika kuhamasisha wananchi juu ya kuhifadhi vyanzo vya maji na utunzaji wa mazingira. Na katika kuhamasisha wananchi nashauri Wizara pia itambue sasa mwananchi mmoja mmoja au vikundi, au taasisi vitakavyokuwa vinahifadhi vyanzo vya maji na vinatunza mazingira viwatambue na kuwapa tunzo au motisha maalum ili iwe hamasa kwa wengine nao kushawishika kutunza vyanzo vya maji na kuhifadhi mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namalizia kwa kusema kwamba maji safi na salama ndiyo yanayozaaa maji

taka. Kwa hivyo kama maji safi na salama ndiyo yanayozaa maji taka ni vyema basi miundombinu ya maji safi iende sambamba na miundombinu ya maji taka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naipongeza Serikali kwa yote yanayofanywa tuko pamoja Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri tuko pamoja kukusaidia katika kutatua changamoto hizi, kukushauri kila tunapohitajika. Naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mnzava, Mheshimiwa Bilakwate, Mheshimiwa Makilagi.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujalia uzima, aliyenipa uwezo kuwepo Bungeni leo na kuweza kuchanglia bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake, wanafanya kazi nzuri Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana tunampongeza sana anafanya kazi kubwa na kazi nzuri. Pia tumpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, kwenye Wizara hii siyo kwa Waziri na Katibu peke yake hata wataalam wao wale watu wa Idara ya Maji Vijijini Mkurugenzi na Msaidizi wake wanafanya kazi nzuri, wanatoa ushirikiano wa kutosha huwa nawasumbua wakati mwengine mpaka usiku nikiwa na changamoto za maji kule kwetu Korogwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru sana Serikali, kwa muda mrefu watu wa Korogwe tumekuwa tukiangaika na vibali vya mradi wa Vuga, Mlembule, na mradi wa Lusanga, lakini mwezi wa pili hatimaye tumepata vibali vile na miradi ile tayari taratibu zimeanza manunuzi kwa ajili ya wakandarasi kuendelea na kazi zile, tumesubiri kwa muda mrefu kwa hiyo tunaishukuru sana na kuipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri nikushuku sana kwa ile kazi ya ujenzi wa tenki pale Mombo

tulikuwa na changamoto ya mtambo kwa ajili ya kutibu maji, tumeshamaliza michoro, imeshaletwa Wizarani tunaomba mtusaidie ile kazi ifanyike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana dada yangu Mheshimiwa Mboni, alizungumza kwa uchungu sana kuhusu kero ya maji kule Handeni; na ni kweli Handeni kuna shida kubwa sana ya maji, na miongoni mwa njia za kutatua kero ya maji Handeni ni mradi ule wa HTM, na Wizara ilishafanya mpaka usanifu wa kupanua na kuboresha ule mradi. Sasa ukienda kule Korogwe kuna Kata inaitwa Kata ya Mswaha, ina vijiji vitano, kijiji kimoja kinaitwa Kijiji cha Tabora, ndipo kwenye chanzo cha maji cha mradi huu wa HTM na kuna vijiji vingine vinne Kijiji cha Mswaha Darajani, Mswaha Majengo, Kijiji cha Mafuleta, na Kijiji cha Maulwi Rutuba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi vilifanyia usanifu pia kwamba vitafaidika na mradi huu wa uboeshaji na upanuzi wa mradi huu wa HTM ni muda mrefu wananchi wale wanasubiri Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana kazi hii ifanyike na itakapofanyika msiwashau watu wa Korogwe kwenye Vijiji hivyo maana Kata hiyo ndiyo kilipo chanzo cha maji cha HTM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Korogwe kuna eneo linaitwa Bungu, tuliwahi kuwa na mradi wa maji tulipata ufadhili wa watu *World Division*, tukawa na mradi wa shilingi milioni 969, na ule mradi ulikamika na ulinufaisha vijiji tano, lakini maji yale ni mengi yana uwezo wa kunufaisha vijiji vingine vitatu, Kijiji cha Mlungui, Kijiji cha Kwemshai na Kijiji cha Ngulu. Tunaiomba sana Wizara tuko kwenye maandalizi ya mwisho ya kuleta maombi kwenu ili mtusaidie tuweze kupata fedha za kusambaza na kupeleka maji kwenye maeneo hayo ambayo nimeyataja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa maji wa Mwanga, Same, korogwe, mradi huu umesemwa muda mrefu ni mradi muhimu sana unanufaisha Wilaya za Same, Wilaya ya Mwanga na Wilaya ya Korogwe, nimeona kwenye

kitabu cha Mheshimiwa Waziri kwenye mwaka wa fedha unaokuja tunasema tumetenga bilioni 29 sijaona kama ndiyo tunakwenda kukamilisha ule mradi au bado tutaendelea kusubiri kwa miaka mingine na awamu nyingine zijazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida ambayo tunaipata watu wa Korogwe ambaao na sisi tumesubiri kwa muda mrefu mradi huu sisi ndiyo tuko mwishoni, tuna Vijiji vitano kwenye Kata ya Mkomazi, Kijiji cha Manga Mikocheni, Kijiji cha Manga Mtindilo, Kijiji cha Mkomazi Kijiji cha Bwiko na Kijiji cha Nanyogie. Vinanufaka na mradi huu na sisi ndiyo tuko mwishoni na tunaambiwa kuna bilioni 29, je mradi huu unakwenda kukamilika? Maana sisi watu wa Korogwe ambaao ndiyo tuko mwishoni tunanufaika na mradi huu ukiwa umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri ukumbuke kwamba tumeusubiri kwa muda mrefu, na changamoto ya maji kwenye vijiji hivyo ni kubwa sana tunakuomba sana utakapokuja kufanya majumuisho utuambie maana mwanzoni pia kwenye vikao vya maandilizi na utekelezaji wa mradi huu watu wa Korogwe tulikuwa tunahusishwa, lakini baadaye kumekuwa na kama sintofahamu hivi hatujui hata kinachoendelea ni nini. Utakapokuja utuambie ni kweli bado watu wa Korogwe ni wanufaika kwenye mradi huu? Na kama ndivyo matumaini yetu yale lini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeleka Wizarani taarifa ya usanifu wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mgwashu na kwa Kibomi tangu mwezi wa tatu, hatujapata taarifa yoyote kwamba tutapa lini kibali. Nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Waziri najua watu ni wasikivu kule Wizarani tusaidie tuweze kupata kibali ili mradi huu angalau ukaanze tutekelezwa kwenye maeneo ya Mgwashu na Kwakibomi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi fedha za *PBR*, sisi ni mionganoni ambaao tulikuwa tunatumaini kwamba

tutanufaika na fedha hizi, lakini kwa mwaka huu wa fedha tulikuwa nao mpaka sasa hatujapata hizi fedha, na sisi tulikuwa tumelenga kwenda kutatua changamoto za maji kwenye baadhi ya maeneo ndani ya Jimbo letu kwa kwenda kufanya ukarabati mdogo wa vyanzo vya maji. Tulikuwa tunategemea kupata fedha hizi kwa ajili ya ukarabati vyanzo vya maji kule Magoma, tulikuwa tunategemea kupata kwa ajili ya kukarabati chanzo cha maji kule Mazinde, tulikuwa tunategemea kwenda kukarabati chanzo cha maji Kerenge na baadhi ya Vijiji vya Kata ya Mashewa. Lakini mpaka leo hatujapata hizi fedha nimejaribu kuuliza Wizarani sijapata majibu ambayo yamekaa vizuri, naomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie tupate hizi fedha twende tukatekeleze hayo mambo kwenye hayo maeneo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ulikuja Korogwe tulikuomba fedha kwa ajili ya kupeleka maji kwenye eneo tunalojenga Hospitali ya Wilaya na tunashukuru kwamba ulikubali na tuliandika ikaja Wizarani baadaye mkaturudishia tulete mchanganuo tukaandaa, tukaleta mchanganuo Wizarani na ukatuhaidi kutupa shilingi milioni 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya sana maji tuliyokuwa tunataka kuyatumia pale chanzo chake ilikuwa ni maji ya kisima, lakini tumegundua chanzo kikubwa na kizuri cha maji ambacho kitakuwa na maji ya mtiririko kwa ajili ya hospitali, pia kwa ajili ya maeneo na Makuyuni na maeneo ya kwa Sunga Mpirani. Kama utaridhia Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba ulikubali, na ukahaidi kutoa milioni 95 nakuomba sana kwa unyenyekevu najua wewe ni msikivu, wewe ni muungwana sana hebu ukubali tukuletee haya marekebisho ili badala ya kutumia chanzo kile cha kisima tutumie chanzo hiki kingine cha maji ya mtiririko na vijiji vingine vya karibu na maeneo yanayojengwa hospitali na vyenyewe viweze kunufaika na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Bunge limeanza la bajeti tangu bajeti ya kwanza nilikuwa nataka kuchangia naenda uhamishoni, lakini leo sijaenda uhamishoni

nachangia nikiwa kwenye kiti hiki, kwa sababu maji ni jambo muhimu ndiyo maana hata humu unaona kumetulia. Ukiroma vizuri hata kitabu hivi vitabu nya hotuba nya rangi hii nadhani mnanielewa nikisema nya rangi hii kwa mara ya kwanza nimeona hotuba ambayo imegusa vitu tofauti na nyine utakuta Wizara tatu, Wizara nne hotuba ni hiyo hiyo, lakini leo nimeona hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumesema hapa na nimesema Mheshimiwa Waziri kila mahali nasema tunaomba tunaomba niliposoma hutuba yako kwenye kitabu hichi ukurasa wa 106 changamoto ya kwanza unaionesha ni ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, pamoja na maombi yote haya ambayo tunayaweka kama hatuna fedha bado changamoto ni kubwa ni miradi hii itakuwa na shida kwenye kutekeleza, yamekuwepo mawazo humu kwamba iongezwe shilingi 50 na wengine wamesema kwenye mafuta, pia iko hofu kwamba inaweza ikasababisha mfumuko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nishauri tunahitaji kweli ongezeko la fedha kwa ajili ya miradi ya maji kwenye nchi yetu. Ukiangalia lengo tulilokuwanalo la kufika upatikanaji wa maji mwaka 2020 na asilimia tuliyokuwa nayo sasa bila kuwa na mkakati madhubuti wa kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maji tutapata shida kwenda kufikia lengo letu. Niombe tu kuishauri Serikali wametusikia Waheshimiwa Wabunge hebu ufanyieni kazi huu ushauri wa Wabunge uliotolewa, ungeniambia kwenye mafuta kunakuwa na mfumuko wa bei nikasema bado yako maeneo mengine, kuna maeneo kwenye mawasiliano kuna watumiaji wengi, tunaweza kuangalia namna ya kuongeza huko...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupate fedha ajili ya kuweza kusaidia kugharamia miradi ya maji, baada ya kusema hayo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, hotuba yangu kwa ujumla imelenga kwenye maombi, naomba sana maombi

yangu myapokee, naomba myafanye kazi naomba muwasaidie watu wa Korogwe ili tuondokane na changamoto hii ya maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, kwa asilimia 100. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bilakwate, Mheshimiwa Makilagi, Mheshimiwa Obama.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu kuendelea kuwatumia wananchi wa Jimbo la Kyerwa. Pia nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Maji kwa kazi nzuri inazofanya. Pamoja na changamoto ambazo wameeleza, lakini tumeona Mheshimiwa Waziri na timu yake wakienda maeneo mbalimbali kutatua kero ya maji. Kwa hiyo, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na tunaamini juhudhi hizo zitaendelea ili kuhakikisha tunapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, pamoja na changamoto ambazo zipo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa miradi ambayo inaendelea kule Jimboni kwangu Kyerwa. Tunao mradi mkubwa ambao tumemaliza usanifu, mradi wa kimkakati wa Kata 18 kwenye vijiji 57. Mradi huu tunaamini mpaka hatua tuliyofikia ya usanifu, sasa kazi iliyobaki ni kazi ya kutangazwa tenda na kuutafutia pesa ili mradi huu uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sana Mheshimiwa Waziri, hali ni mbaya kwa Wanakyerwa, naomba sana mradi huu uangaliwe ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. Tunajua maji ni uhai, maji ni kila kitu, maji ni uchumi. Bila kuwa na maji safi na salama mambo mengine hayawesi yakaenda hata tunaposema tunaingia kwenye uchumi wa katika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uchumi wetu uweze kustawi, uweze kusonga mbele ni pale ambapo tutakuwa na maji safi na salama kwa sababu tunategemea kule vijiji ni ndiko kuna uzalishaji mkubwa na hawa wananchi wakipata maji safi na salama ule usumbufu wa kuamka usiku kwenda kutafuta maji utaondoka na wataingia kwenye shughuli za uzalishaji na uchumi wa Taifa letu utaweza kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri mradi huu nimeshakutana na wewe ofisini, nimeshakutana na Naibu Waziri, nimeshakutana na Katibu Mkuu lakini nimekutana pia na Waziri wa Fedha, ninaamini Mungu atasaidia mradi huu utapatiwa pesa ili uweze kuanza na wananchi wa Kyerwa waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilisemee kwa upande wa Kyerwa, tunao mradi wa Kata ya Mabira unaendelea vizuri lakini kuna mradi wa Kata ya Kaisho, Rutunguru na Isingiro, mradi huu Naibu Waziri ulipofika Kyerwa walikueleza Mkandarasi kwa kweli hana uwezo na uliamuru Mkandarasi yule asimamishwe lakini tangu umetoka kule hakuna kazi inayoendelea, mradi umesimama na huyu Mkandarasi kwa kweli mimi niombe asije Wizarani kuwadanganya, hana uwezo kabisa. Wakati mwingine unajiliza, hivi hawa Wakandarasi wanapatikanaje? Mtu ambaye anaendesha kampuni yeye na mke wake ndio unakuta wako *site*, ndio wanaofanya kazi, yaani hakuna kitu kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba sana na Mheshimiwa Waziri ikiwezekana muunde Tume ya kwenda kukagua hii miradi na kuangalia uwezo wa hawa Wakandarasi kweli uwezo wao ni mdogo na wanakwamisha hii miradi isiweze kukamilika. Hili Wabunge wengi wameliongelea, maeneo mengi kwa kweli Wakandarasi hawana uwezo na wakati mwingine unaweza ukafikiri labda hizi kampuni wanapeana ni zile za urafiki au za kutafuta 10 percent ili waweze kupata chao waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna nia ya dhati ya kuweza kuwapa maji safi na salama Watanzania, lazima tuhakikishe tuna wataalam wenyewe uwezo wa kuweza kusimamia miradi hii, lakini pia hata wale wanaotoa hizi tenda tuwafuatilile kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamwamini Mheshimiwa Waziri, anafanyakazi zake vizuri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote lakini lazima waangalie wataalam walionao kule chini, wanaweza wakawakwamisha ili wasiweze kufanikisha zile juhudzi zao. Kwa hiyo, naomba sana hili waliangalie na pia kwa mfano, kama kule kwangu Kyerwa kuna watalaam wawili, Mzee moja ambaye ni Injinia kwa kweli ni mzee ambaye afya yake haijaka vizuri, anahitaji msaada. Kwa hiyo, Kyerwa ni kama tuna mtaalam mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie. Tunaposema tunataka tuwe na chombo ambacho kinajisimamia kuhusiana na maji, lazima tuwe na wataalam wa uhakika. Hata tukisema tutaunda chombo, bila ya kuwa na wataalam, tutakuwa tunapoteza muda. Nawaomba sana hilo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni kwenye Wizara ya TAMISEMI, wameunda *TARURA*. Kwa muda mfupi *TARURA* wamefanya kazi nzuri sana, ni kwa sababu wamepeleka wataalam wenyewe uwezo. Nami nawaomba sana wapeleke wataalam ili waweze kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Waheshimiwa Wabunge wameongea sana kwamba ili tuweze kutatua tatizo la maji, tumeomba sana huu mfuko wa maji uweze kuongezewa fedha. Bunge lilishaazimia shilingi 50/=, lakini nashindwa kuelewa, ni kwa nini hili jambo linapata shida sana? Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aeletee kweli tuweze kuridhika. Hatuwezi tukaridhika kwa maneno tu, tunahitaji wananchi wetu waweze kupatiwa maji safi na salama ndiyo tunaweza kuelewa. Vinginevyo kwa

kweli Jumatatu wakati unahitimisha, kama hutakuwa na majibu ya kuongeza shilingi 50/= kwa kweli hatutaelewana kama Wabunge wote walivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nilikuwa najiuliza, hivi tukiamua leo Watanzania, maana tumeamua kuwapatia huduma Watanzania; tukiamua kila vocha ya shilingi 1,000/= ikatwe shilingi mbili tu, hebu jaribu kupiga mahesabu ni vocha ngapi ambazo zinaweza kuingizia pesa nyingi kwenye mfuko wa maji na tukaweza kutatua tatizo la maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, tunavyo vyanzo ambavyo vinaweza vikatupatia maji safi na salama. Watanzania tumeamua kupiga hatua, ni pamoja na kujifunga mkanda. Vinginevyo, tutakuja hapa tutaeleza mambo ya siasa, tutasema tunawapelekea maji lakin hakuna hatua yoyote ambayo tutachukua. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri hili uliangalie tuweze kuwafikishia wananchi wetu maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli baada ya kusema hayo, naishukuru Serikali, wanasesma hata kwa kile kidogo uweze kushukuru. Kwa Kyerwa kwa kweli Awamu ya Tano angalau tunaweza tukasema kuna chochote tunachokiona, kama nilivyosema tunao mradi wa kimkakati wa vijiji 57 kwenye Kata 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuomba sana, Mheshimiwa Waziri mradi huu ndiyo unaweza ukawa mkombozi kwa wananchi wa Kyerwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Makilagi halafu Mheshimiwa Obama na Mheshimiwa Maige wajiandae.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama na kutoa mchango wangu katika bajeti hii muhimu ambayo ni bajeti ya maji, bajeti ambayo kwa kweli ndiyo uhai wa Taifa letu. Kwa kweli maji ni uhai na bila maji hakuna chochote ambacho kinawenza kufanyika ikiwemo hata masuala ya kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuleta salam za wananchi ninaowawakilisha ambao ni wanawake wa Tanzania walionipitisha kwa kura zao zote za kishindo tena kura zote za ndiyo. Wamenileta nilete salamu; wale wananchi wanaotoka katika maeneo yaliyopata maji kwa asilimia 64 wanaishukuru Serikali kwa kazi njema waliyoifanya ya kujenga miundombinu. Hao ni wale wa vijijini wamenituma nije niishukuru Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta salamu za wananchi wanaoishi maeneo ya mjini na hasa katika Makao Makuu ya Mikoa kwa kiwango cha maji kwao sasa ni asilimia 80. Wanawake hawa wamenituma nije kusema ahsante sana maana Serikali imewatendea haki. Vile vile wapo wanawake walionituma wanaoishi katika miji midogo midogo, kwa kiwango cha asilimia 64 wamepatiwa maji safi na salama na wenyewe wanasema ahsante. Hata maandiko ya dini yanasema, mtu anayeshukuru huwa anaomba tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilete salamu za wanawake wa Tanzania, kama alivyosema Mheshimiwa Kitandula, bado kuna Watanzania zaidi ya 20,000 hawapati maji. Wanawake ambao nawawakilisha ambao wamekuwa wakitembea kwa umbali mrefu, ambao wamekuwa hata hawafanyi kazi wanashinda barabarani, ambao wamekuwa hata hawapati nafasi ya kukaa na familia, kulea familia zao, kila wakati wako barabarani na wenyewe wamesema nilete kilio chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanaomba Serikali yao Tukufu, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, ambapo kwa kweli ni wanawake wa Tanzania, wanawake

wa nchi hii, ambao ndio walioiweka madarakani, wanaomba Serikali ithubutu, itafute fedha na hata kama ni za kukopa na kama ni kuongeza vyanzo nya mapato kwenye kodi ya mafuta, kwenye mitandao ya simu na namna yoyote ile wanavyoona inafaa, fedha zitafutwe kwa ajili ya kipeleka maji vijijini, wanawake wa Tanzania waweze kuhudumiwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenituma niseme wanawake wamevumilia kwa muda mrefu sana, wanapata adha kubwa sana. Kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tumewaaahidi kuwatua ndoo ya maji kichwani. Hebu Serikali yetu na tunajua inaweza ikathubutu, itafute hizi fedha kwa namna inavyojua na kwa vyovyote vile miradi itekelezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilete salamu za wananchi wa Mkoa wa Mara. Tunashukuru sana kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa leo, tumeona kuna miradi mingi inakwenda kutekelezwa katika Mji wa Mugumu. Katika ile Miji 29 na Mugumu ni wadau. Tunaomba tulete shukurani zetu, ahsante Serikali kwa kisikiliza kilio cha Wana-Mara, Mji wa Mugumu sasa upate maji safi na salama. Ni kwa muda mrefu wananchi wa Mji wa Mugumu wamekuwa wakitumia maji kama tope. Tunaishukuru Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaishukuru sana Serikali inakwenda kujenga mradi wa maji Tarime ambapo kwa muda mrefu sana tumekuwa tukileta kilio. Naomba kwa niaba ya wananchi wa Tarime, Majimbo yote mawili; Tarime Mjini na Tarime Vijijini nilete shukurani zao kwa mradi unaokwenda kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta shukurani kwa wananchi wa Ranya na hasa wananchi wa Mji wa Shirati, Mji ambao ni mkongwe, Mji ambao umekuwepo miaka mingi. Wananchi wanazungukwa na ziwa lakini kwa muda mrefu wamekuwa hawapati maji. Kwa awamu hii sasa naona Serikali inakwenda kuwatendea haki. Kwa kweli kipekee nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wako,

tumeona ambavyo mmekuwa mkifuatilia katika Mkoa wetu kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Mara wanapata maji kwa sababu ni haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara unazungukwa na Ziwa Victoria, Mto Mara, Mto Suguti na Mto Simiyu, lakini kiwango cha upatikanaji wa maji Mkoa wa Mara kwa vijijini ni kwa kiwango cha asilimia 50.8 na kwa upande wa mjini ni asilimia 60. Kwa hiyo, bado naona kwa kweli hali ni mbaya. Ni imani yangu na ni imani ya Wabunge wa Mkoa wa Mara na wananchi wa Mkoa wa Mara na hasa wanawake, miradi hii ikienda kutekelezwa tena kwa wakati itaongeza kiwango kikubwa cha maji na wanawake wa Mkoa huu wataachana na adha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mradi wa Mgango-Kyabakali - Butiama mradi ambaa nimeusikiliza kwa muda mrefu sana, tangu Mbunge akiwa Marehemu Dkt. Magoti, Mwenyezi Mungu amjaalie. Akaondoka, akaja Balozi Ndobo, ameupigia kelele katika Bunge ameondoka; amekuja Mheshimiwa Mkono, vipindi vyote viwili ameupigia kelele, hakuna kilichofanyika; amekuja Profesa Muhongo; nami tangu nimeingia Bunge hili, Awamu ya Kwanza nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Maji, tumeupigia kelele, kila jibu tunalopewa, mradi utajengwa kupitia *BADEA*, mradi utajengwa kupitia *Saudia*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013, Serikali ya Tanzania ilisaini mkataba na *BADEA*, ilisaini mkataba na *Saudia* na tukakubaliana kwamba ifikapo 2015 mradi utakamiliwa. Nimefurahishwa kwenye kitabu hiki nimeona mradi unaendelea na mipango nimeiona ni mizuri na ninaona mambo ni mazuri. Naomba Mheshimiwa Mbarawa ambaye umekuwa ukiniambia hata huko nje na Mheshimiwa Muhongo hata juzi mlikaa naye, hebu wewe tuambie wananchi wa Mgango na Butiama wanapata maji au hawapati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi unaanza lini? Kwa sababu kusema kweli nimepitia vitabu vyta hotuba nydingi, kila

wakati inazungumzwa *BADEA* Iakini mradi hauanzi. Mheshimiwa Waziri alipokuja na Mheshimiwa Rais alituambia mradi tunakwenda kutangaza tenda na siyo muda mrefu mradi utanza. Leo tunakwenda kumaliza mwaka, napenda leo tusikilize kauli yake, atakapokuja kuhitimisha hii hoja, wananchi wa Mgango wanamsubiri, wananchi wa Butiama nyumbani kwa Baba wa Taifa wanamsubiri, akina Mzee Msuguri waliotumikia nchi kwa uaminifu na weledi mkubwa wakapumzika, wanahaingaika na maji. Jamani hamwoni aibu ndugu zangu tupige kelele kila siku? Hebu Mheshimiwa Waziri tuambieni mkakati ni nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshituka hapa, naona huu mradi kwa kiwango kikubwa unategemea fedha za nje, *BADEA* na Saudia, nafikiri ndiyo maana hautekelezeki. Leo Mheshimiwa Mbarawa nakupongeza kwa sababu umeweka fedha nyingi zaidi ya shillingi bilioni nane kwa fedha za ndani. Nitoe ushauri kwako, nami najua ni Waziri msikivu ambaye umekuwa ukitusikiliza Wabunge na umesikiliza Watanzania wote; hebu hizi shilingi bilioni nane, ni fedha nyingi, mradi basi uanze hata wananchi wawe na matumaini ili Saudia na hao *BADEA* watakapokuja, watukute tuko barabarani. Kusema kweli tumeshaongea kule maneno yote yamekwisha. Kila wakati, wananchi wanapoteza imani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe alipokuja Butiama siku ile na Mheshimiwa Rais alipoelezea huu mradi kama alikuwa anafuatilia, wananchi walinyamaza kimya kwa sababu viongozi wengi walishawaambia hivyo. Alianza Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa aliwaambia hivyo, hakuna kitu; akaja yule Mheshimiwa Profesa Mwandosya, hakuna kitu; akaja Mheshimiwa Profesa Maghembe, tena ye ye alikwenda kabisa mpaka kwenye chanzo na tuliongozana naye, hakuna kitu; amekuja juzi Mheshimiwa *Engineer Lwenge* hakuna kitu. Kwa hiyo, hata ye ye alipokuwa akiwaambia siku ile mbele ya Mheshimiwa Rais, walikuwa wanaona hakuna kitu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu leo Mheshimiwa Waziri toa neno la matumaini kwa wananchi wa Wilaya ya Butiama, nyumbani kwa Baba wa Taifa, kuliko na kaburi, tusiendelee kuomba maji hapa hata kwa ajili ya kumiminia lile kaburi lake kumwagilia maua Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie upatikanaji wa fedha. Mwaka 2018 Serikali ilitenga fedha nyingi sana, lakini kwa mujibu wa Bajeti hii fedha hazikutoka zote. Nami naungana na wenzangu kwamba fedha sasa zitole. Lipo tatizo kubwa ambalo nalionna, hawa Wakandarasi ambao wanawazungumza wenzangu, kwa kweli baadhi ya maeneo Wakandarasi ni wa ovyo sana. Hawana uwezo, wengine sio waaminifu, wengine wamefikia hatua wanakimbia miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fanyeni tathmini, hivi tunao Mainjinia wa miradi ya maji? Kwa sababu Tanzania naona tunazalisha Mainjinia nchini na wengi hawana kazi wako majumbani, hivi kweli...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri; na Waziri amekusikia.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Albert hayupo, Mheshimiwa Maige halafu Mheshimiwa Mwilima na Mheshimiwa Katani A. Katani wajiandae.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naomba nianze kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudii kubwa ambazo zinafanyika katika kukabiliana na tatizo la maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumza kwamba tatizo la maji kwa sasa liliyvo ni tatizo kubwa sana ambalo naiomba sana Serikali yangu ilitazame kwa mtazamo tofauti. Ni janga ambalo kwa kweli karibia kila mahali kuna kilio kikubwa na jitihada zisipofanyika tukaendelea na mwendo huu tulionao, naamini kila wakati tutaendelea kupokea malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinadharia Jimbo la Msalala kama miradi yote ambayo imepangwa na Serikali kutekelezwa na kama ikitekelezwa katika muda tulipopanga wa kufikia 2020, Jimbo letu litakuwa limebakiza Kata mbili tu ambazo hazina maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali hasa kuanzia Awamu hii ya Tano lakini pia hata Awamu ya Nne kuna baadhi ya miradi mikubwa ilianza kutekelezwa. Kwa kutaja tu baadhi ya miradi, ukurasa ule wa 31 Mheshimiwa Waziri amezungumzia mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambao kwa sasa uko kwenye awamu ya pili ya utekelezaji unaogusa vijiji 100 na Jimbo la Msalala lina vijiji vyake kadhaa ambao unaendelea kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine mkubwa sana wa zaidi ya shilingi bilioni 15 unaotekelizwa kwa ubia kati ya mgodi wa Bulyanhulu (*Acacia*) pamoja na Serikali yetu. Unatoa maji Mhangu hadi Kijiji cha llogi kwenye Kata ya Bugarama. Kuna mradi mwingine mkubwa tu na wenyewe wenyewe zaidi ya shilingi bilioni 24 ambao unapeleka maji kwenye Mji wa Kagongwa na Isaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii yote ikitekelezwa; na yote ina sura ya awamu. Kwa mfano, mradi wa Isaka na Kagongwa una awamu mbili, mradi wa Mangu, llogi na wenyewe una awamu mbili; na miradi hii ikitekelezwa kwa ukamilifu, itaweza kutatua tatizo la maji tulilonalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ifanye juhudzi za kutafuta ufumbuzi. Bahati nzuri wazo la kutafuta

ufumbuzi au jibu la tatizo tulilonalo limeshatolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa. Ukiangalia miradi yote inashindwa kukamilika mapema kwa sababu ya upatikanaji wa fedha ama fedha zinapopatikana kidogo zinakuwa ni zile ambazo ni za mfuko wa maji peke yake, zile za Bajeti Kuu na za wafadhili hazipatikani kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameshapendekeza hapa, nami niungane nao na niseme tu kwa sababu nijambo ambalo tulishaliama hapa, ni vizuri sana Serikali ikakubaliana na ombi letu la kwamba angalau tuongeze tozo kwenye mafuta ili tuweze kutatua tatizo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii niliyoitaja kinadharia ukiisikiliza ni mizuri sana, lakini miradi karibu yote utekelezaji wake uko kwenye viwango tofauti tofauti hakuna ambaao uko zaidi ya asilimia 80 na hapo ndiyo tatizo kubwa linapoanzia. Nikanza kwa mfano na ule Mradi wa Viji 100; mradi huu tuliuibua hapa Bungeni mwaka 2014, Waziri wa Maji akiwa Profesa Maghembe, tukasema viji 100 vilivyoko pembezoni mwa bomba kuu la kutoka Ziwa Victoria hadi Shinyanga vipatiwe maji, Jimbo la Msalala lilikuwa na viji 16 katika orodha ya viji 100. Mpaka tunavyozungumza hivi sasa viji ambavyo vimepatiwa maji ni viji vitano tu, kwa hiyo bado viji tisa toka mwaka 2014 havijapata maji, hili ni tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi wa pili niliousema wa kutoa maji Mangu hadi Ilogi kuititia Wilaya ya Nyang'hwale pamoja na Wilaya ya Msalala, naishukuru sana Serikali na hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu wote wawili Katibu Mkuu mwenyewe Profesa Mkumbo na *Engineer Kalobel* wameusukuma sana mradi huu hadi kufika hatua hii ya kuanza kutekelezwa. Tuliubuni namgodi wa *Acacia* mwaka 2012 na toka 2012 hadi mwaka 2014/2015, hakuna utekelezaji uliofanyika, lakini 2016, baada ya Serikali hii kuingia madarakani ikatoa fedha na mradi umeanza kutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa uko asilimia chini ya 50 na lengo lilikuwa kufika Desemba, 2018 bomba Kuu la kutoka Mangu hadi Ilogi liwe limewekwa, hivi sasa halijakamilika. Awamu ya pili ambayo ni kusambaza maji kwenye vijiji vilivyo jirani na yenyewe haijaanza. Naiomba sana Serikali ikubali hili ombi la kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Maji ili fedha hizo ziweze kutekeleza awamu ya pili ya kupeleka maji kwenye vijiji ambavyo viro pembezoni mwa hilo bomba kuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kagongwana Isaka na wenyewe tulisema uwe na awamu mbili, awamu ya kwanza ni ile ya kupeleka bomba kuu na kusambaza maji pale Kagongwa na Isaka penyewe, lakini kuna kata tatu ambazo ziko pembezoni ndani ya kilomita 12 zinapitiwa na bomba hilo; Kata ya Mwalugulu, Kata ya Mwakatapamoja na Kata ya Isaka na Kata ya Jana. Vijiji hivi tunaenda kutengeneza matatizo, wanaona maji yanapita kwenda kwa wenzao wa Isaka wao hawapati maji. Tulisema hii ni awamu ya kwanza, vumilieni hadi kufika 2020 wananchi hawa watakuwa wameanza kuona na wenyewe wakitekelezewa mradi huu. Naiomba Serikali yangu wakubali hili ombi ili awamu ya pili ya kupeleka maji katika vijiji vilivyo kopo pembezoni mwa hilo bomba kuu uweze kutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulibahatika pia kupata ule mradi wa mkopo wa Benki ya Dunia vijiji 10 kila Wilaya. Halmashauri ya Msalala tuna Kijiji kimoja cha Segese kinadai shilingi...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri sana. Mheshimiwa Mwilima, atafuatiwa naMheshimiwa Katani na Mheshimiwa Kapufi.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, kwa hiyo naomba tu Kijiji cha Segese

kinadai milioni 30 ya kufunga pampu, milioni 700 zimewekwa pale, lakini mradi haufanyi kazi. Tunaomba Serikali isaidie ombi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nanashukuru sana kwa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwilima atafuatiwa naMheshimiwa Katani na Mheshimiwa Kapufi.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwakupata hii fursa uya kuchangia Wizara muhimu sana, Wizara ya Maji, maana bila maji hakuna uhai. Nianze kwa kumpongeza Profesa, Mheshimiwa Waziri maana yake juzi nililia kidogo kuhusiana na mradi wangu wa Nguruka Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wamenisaidia lita 2,000 za mafuta. Nawashukuru sanaMheshimiwa Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa namna ambavyo walivyoweza kuwasaidia akinamama wa Tarafa yangu ya Nguruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nzungumzie suala la miradi yangu ya maji iliyoko jimboni. Naomba nzungumzie Mradi huo wa Nguruka, namwomba Mheshimiwa Waziri, natambua kwamba ule mradi ni wamuda mrefu na kiasi fulani umekamilika, lakini bado ile *extension* ya kutoka pale Nguruka kwenda Kijiji cha Bweru na Kijiji cha Mlyabibi haijaanza kutekelezwa. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri,kwa sababu waliahidi wenyewe kama Wizara kwamba mradi ule chanzo chake cha maji kinatosha kupeleka maji yale mpaka Mlyabibi lakini sio tu Mlyabibi na Kijiji cha Bweru. Sambamba na hilo nimwombe tu Mheshimiwa Waziri ajaribu kumwomba Mkandarasi aweze kumaliza basi hayo maeneo mawili kwa maana ya Bweru, pamoja na Mlyabibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili naomba nzungumzie Mradi wangu wa Kandaga. Ninao Mradi waKandagaambao utekelezaji wake ulikuwa ni bajeti 2013/2014, lakini hadi leo hii Mheshimiwa Waziri ni shahidi tulifanya naye ziara, tulienda pale, maji yanatoka kiasi, lakini wananchi

bado hawajapata maji. DP zimewekwa, tanki lipo, maji yanatoka, lakini wananchi hawajapata maji, kwa hiyo wananchi wa Kijiji cha Kandaga wamenituma, wanasema wanaomba sana kama mama niko hapa, waliniamini na wanataka waniamini tena hapo baadaye, kwa hiyo naomba Mradi ule wa Kandaga uweze kutoa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu naomba nizungumzie Mradi wangu waKijiji cha Rukoma. Tunao mradi mkubwa katika Kijiji cha Rukoma lakini kwa bahati mbaya mradi ule una chanzo kikubwa cha maji, chanzo chake ni Mto Luegele, mto huu una maji mengi sana kiasi kwamba hata wenzetu wa Wizara ya Nishati wanatarajia kufua umeme kuititia chanzo hiki. Sasa ombi la kwanza naomba aidha niMheshimiwa Waziri au ni Mheshimiwa Naibu Waziri watafute siku tuambatane waende wakashuhudie ule Mradi wa Rukoma lakini wakashuhudie hicho chanzo cha maji. Chanzo kipo, tatizo ni utekelezaji wa ule mradi umesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba nizungumzie Mradi wa Ilagala, tunao Mradi mkubwa wa Ilagala lakini mradi ule unaonekana kwamba ulitekelezwa chini ya viwango. Kwa hiyo Ilagala sio mbali Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenda Rukoma nitaomba pia tuambatane twende Ilagalailiaweze kuona tunafanyaje hapo kuwasaidia wananchi wa Vijiji vya Ilagala na vitongoji vyake kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwenye kitabu chake ni jinsi gani Wizara wanajipanga kutekeleza Mradi wa Usambazaji Maji kutoka kwenye Maziwa Makuu kwa maana ya Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria pamoja na Ziwa Tanganyika. Mimi najiuliza maswali sipati majibu, Ziwa Tanganyika maji yake ni baridi, ni kama tu maji haya ya Kilimanjaro na maji mengine, kwa nini hakuna mkakati maalum wa kuvisaidia vijiji 34 ambavyo vinapakana na Ziwa Tanganyika. Ukiangalia wananchi wale wanakaa karibu na Ziwa lakini hawana maji safi na salama. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri watakapokuwa na mkakati wa makusudi, naomba basi watambue kwamba

Jimbo langu lina vijiji 34 vinavyopakana na Ziwa Tanganyika.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mpango mkakati wa Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo *by that time*, kwamba wanataka kutekeleza mradi mkubwa wa Mto Malagarasi. Sasa sijajua Mheshimiwa Waziri mradi ule umefikia wapi? Labda Jumatatu akija hapa kuhitimisha atuambie ule mpango mkakati wa Mradi huu mkubwa wa Mto Malagarasi umefikia wapi, kwa sababu kama sisi watu wa Kigoma tukiweza kupata Mradi kutoka Ziwa Tanganyika pamoja na wenzetu wa Katavi na Rukwa, lakini tukapata pia Mradi wa Mto Malagarasi hata wenzetu wa Kaliuwa, wenzetu wa Urambo pia watapata maji safi na salama kupitia katika Mradi huu mkubwa wa Mto Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niiombe sana Serikali iangalie namna ya kuwaongeza pesa wenzetu hawa wa Wizara ya Maji. Nasema hivi kwa sababu kwenye bajeti ya 2018/2019, Wizara hii ilipangiwa takribani shilingi bilioni 697 na ushee, lakini kwenye bajeti hii Wizara imepangiwa pungufu ya shilingi bilioni 66. Sasa niiombe sana Wizara ya Fedha, najua kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri yupo hapa, hii Wizara ni Wizara nyeti sana, wengi wameongea kila mtu ameongea kwa hisia zake kwa sababu sisi Serikali yetu kupitia llani yetu ya Chama cha Mapinduzi tunasema kwamba tutamtua mwanamke ndoo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri Mheshimiwa.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwakuunga mkono hoja nakuzidi kuwapongeza Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Katani, halafu Mheshimiwa Kapufi na MheshimiwaChikambo.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru sana, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kuja kwangu tarehe 18 Oktoba,2018 kujionea adha ya maji ambayo ipo kwenye Jimbo langu la Tandahimba. Mheshimiwa Waziri alivyofika nadhani ameona kwa machoyake, lakini kwenye mpango huu wa maji Tandahimba tunazungumza sana Mradi wa Maji wa Makonde ambao utahudumia Wilaya ya Newala, Tandahimba na Nanyamba. Shida yangu kwenye huu mradi wanaosema waKitaifa, tulipoingia Bungeni 2016/2017, kwenye kabrasha la kitabu cha bajeti ya maji, ukisoma ukurasa ule wa 78 umezungumzwa Mradi huu wa Makonde tukiwa tunatarajia fedha za mkopo kutoka Benki ya India. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyorudi Bungeni 2017/2018, tumekuja tena kwenye ukurasa wa 80, tumeuzungumzia tena Mradi wa Maji wa Makonde tukiwa tunasubiri fedha kutoka kwenye fedha ya mkopo kutoka India. Tumekuja kwenye bajeti iliyoofuata 2018/2019, ukurasa wa 64,Mradi huo wa Maji wa Makonde tunaoczungumza, tunazungumzia fedha za kutoka kwa wafadhili. Tumekuja kwenye bajeti hii ya leo hii tunayoisema ya 2019/2020 ambayo inawezekana kwa sisi wengine ikawa bajeti ya mwisho tunazungumzia fedha ambazo wanataka kukopa tenasijui wapi, *are we really serious tunataka mradi huu uendeleee?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia kila tukija kwenye bajeti fedha za Mradi huu wa Makonde tunazungumzia fedha za kutoka kwa wafadhili, kwa miaka minne mfululizo, hizo fedha za wafadhili hakuna, hazitoki, hawa watu kweli watapewa maji? Hebu niwaulize ndugu zangu Serikali ya Chama cha Mapinduzi wanayosema Serikali ya wanyonge ni mnyonge gani kama mwananchi hapati maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ndiyo bidhaa pekee ambayo wangekuwa wanawapa Watanzania shukurani yake ingekuwa ni kubwa kuliko kitu chochote kile. Leo zinatengwa fedha mabilioni zinakwenda kwenye

Stiegler's Gorge ambao watumiaji wake si wote, fedha zinakwenda kwenye reli watumiaji wake sio wote, fedha zinakwenda kwenye *bombardier* wa *bombardier* sio wote, waweke fedha kwenye miradi ya maji ambayo itawagusa Watanzania wote. Huu ndio ukomo wa huruma kwa Serikali ya CCM kwa Watanzania. Niwaambie kabisa, kama tunataka kupima ukomo wa huruma kwa Watanzania. (*Makofii*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Katani taarifa.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe rafiki yangu taarifa kwamba ukizungumzia *Stiegler's Gorge* ikiweza kufanya kazi kwa uwezo wake ule maana yake hata kipato chake kitakachoingiza ndani ya Taifa hata hataaulizia tena suala la maji ambalo tunaulizia hapa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia alichokisema, lakini nimkumbushe hata wakati tunazungumza Mradi wa Gesi ya Mtwara tulisema ndio itakuwa mwisho wa tatizo la umeme Tanzania. Leo bado tunalia na umeme, kwa hiyo sitaki kuipokea taarifa yake ile akakae nayo kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Taifa la Tanzania ambalo hatuna shida ya maji yenye, tuna Ziwa Victoria, kwangu Mtwara tuna Mto Ruvuma, tuna Ziwa Malagalasi amezungumza Mheshimiwa Hasna pale, tuna Ziwa Tanganyika, tuna kila vyanzo vya maji ukienda Kilimanjaro kuna maporomoko yanamwaga maji, miaka 59 toka tumepata uhuru tunarudi Bungeni tunazungumza tatizo la maji kweli miaka 59 ya uhuru! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, alizungumza hapa Mzee Mheshimiwa Chenge kwamba tunayoyaazimia Bungeni basi tuyasimamie, ile Sh.50 iliyozungumzwa, niombe Jumatatu Waheshimiwa Wabunge wote kwa tatizo la maji namna liliivyo, tusimamie kuona ile 50 inaongezwa ili watu wapate maji. Watu wamezungumza vyanzo vingi tu hapa, ukienda leo watumiaji wa simu bando tu, ukichukua fedha za kwenye bando ni matrillioni ya fedha, kwa nini tusichukue fedha tukapeleka kwenye maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mradi wangu mdogo ule waMkwihi, leo nimshukuru sana ameupa fedha, lakini ule mradi una *lots* tatu, *lot* ya kwanza ndio hii ambayo amepeleka fedha ya kutoa maji kule kwenye Mto Ngwele ambako pana tanki moja. *Lot* ya pili utatoa Mto Ngwele kupeleka Mangombyana *lot* ya tatu inatoka Mangombya kupeleka vijijini, lakini fedha iliyopata ni ya *lot* moja. Sasa ukiangalia hii *lot* moja maana yake tutakaa miaka tisa ndio kukamilishe *lot* tatu watu wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kamatuna *lots* tatu na fedha ikawa ipo ni bora wakaunganisha fedha wakawapa wakandarasi tofauti ili watu waone *social impact* ya maji ambayo wanafanya. Leo tutawaambia tuna Mradi waMaji wa Mkwihi lakini si ajabu tukamaliza miaka 10 watu hawaoni matunda ya mradi ule ambaao Mheshimiwa Waziri mwenyewe amejionea kwa macho yake. Kwa hiyo nimwombe sana ule mradi utawasaidia wale watu ambaao wanatembea kilomita 58 kutoka Mkwihi kwenda Tandahimba ni kilomita 58. Kwa hiyo nimwombe sana kwa unyenyekevu mkubwa, najua wanachapa kazi vizuri, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri lakini na watumishi wa Wizara ya Maji pia wanafanya kazi kwa usiku na mchana waone namna wanavyoweza kutusaidia. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Kapufi atafuatiwa Mheshimiwa Chikambo,

wajiandae Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Richard Mbogo na muda ukibakia attachangia Mheshimiwa Heche.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nami nianze kumshukuru Waziri Mheshimiwa Mbarawa, nafahamu aliweza kututembelea Mkoa wa Katavi na kwa pamoja tulikwenda kwenye chanzo cha Ikolongo lakini alifuatilia suala la Bwawa la Milala na akaona hali ya ugawaji maji katika Mji wetu wa Mpanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu umuhimu wa maji kama walivyozungumza wazungumzaji wengine waliotangulia na kwa kuanzia nikiwa nimetangulia na kuunga mkono hoja, naomba niliweke katika sura zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kugawa fedha / *meanile Sh.50 tunayoiomba sina matatizo nayo, rai na ombi langu tunapokuwa na pipa lenye tundu wakati tunaendelea kujaza maji kwenye pipa hilo, ufumbuzi ni kwenda kuziba tundu, vinginevyo tutaendelea kuhakikisha pipa lile halijai maji.* Kwa hiyo kupewa fedha, kuwaombea fedha sina tatizo nalo, lakini kudhibiti matumizi ya fedha hapo ndipo ilipo hoja ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, naomba, nafahamu kwa maana ya Jimbo langu la Mpanda Mjini tulipatiwa visima 15, uungwana unanituma kushukuru na visima vile vilishafanyiwa *pumptaste*, jambo linakwenda vzuri. Lilllobaki Mheshimiwa Waziri na wananchi wale wamesharidhika na kazi nzuri ya Serikali kama tumefikia hatua hii ya *pump taste* limebaki jambo moja tu la kufunga *pump*. Kwa hiyo niiombe Wizara tukamilishe zoezi hilo la kufunga *pumpili* wananchi wale waendelee kuwa na imani na Serikali yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikamilisha suala hilo la ufungaji wa *pump* kwa visima 15, naomba nishukuru tena, nafahamu tumesaini kwa maana ya Ikolongo namba mbili

na Mheshimiwa Waziri tulikwenda pamoja akakiona chanzo kile, Mji wetu wa Mpanda asilimia ya maji ambayo inagawanya pale ni katiba ya asilimia 30 ambayo ni kiwango kidogo na ukienda *field* inaweza ikawa chini ya asilimia 30, tuna maeneo ya Makanyagio, tuna maeneo ya Majengo kwa ujumla pale mjini kati mgawanyo wa maji ni tatizo na tunapata matatizo wakati vyanzo vimetuzunguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali wametusaidia kwa maana ya kusaini na Wakandarasi wako *s/ite* kwa maana ya Ikolongo namba mbili. Ninachokiombna fedha zile za awali zimetolewa lakini naomba basi ili tukiusukuma huo mradi wa Ikolongo namba mbili tatizo la maji kwenye eneo letu la Mji wa Mpanda itakuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza zaidi, najua tunakwenda kuusubiri mradi mkubwa kuyatoa maji Ziwa Tanganyika kuyaleta maeneo ya Mpanda na kwingineko. Najua mradi huu utakuwa ni mwarobaini wa matatizo ya maji katika maeneo yetu. Wakati tukiishi kwa matumaini kwa mradi huo, nilichokuwa nakiomba sana Ikorongo Namba Mbili itakuwa ni ufumbuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua pia tuna mradi mmoja wa Manga – Kasokola, toka tumeleta *certificate* katika Wizara, ililetwa tarehe 12 Desemba, 2018 ya shilingi milioni 47 mpaka leo haijalipwa. Mradi ule kwa maana ya Manga na Kasokola, mkandarasi amefika sehemu ya kukata tamaa. Nachokiomba, tukipatiwa fedha hizi akalipwa mkandarasi sehemu ile ya Vijiji vya Manga na Kasokola tatizo la maji nalo litakuwa ni historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona maeneo mengine wakizungumzia kuhusu vyanzo vya maji kwa maana ya mabwawa; sisi katika Mji wetu wa Mpanda tunalo Bwawa la Milala. Ni bwawa zuri lakini tatizo chanzo kile kama kimetelekezwa fulani hivi. Viboko wamezaliana, maji ni machafu, wakati wengine wanahangaika tutapata wapi maji sisi chanzo tunacho tatizo ni utunzaji na kuhakikisha

tunaya-*treat* yale maji ili kuongeza mserereko wa maji pale Mpanda Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanalamika watapata wapi maji, sisi maji tunayo chanzo kipo cha Milala. Historia itatuhukumu kama watu walifanya kazi nzuri kuhakikisha chanzo kile kimekuwepo leo chanzo kipo tunakitelekeza kwa makusudi. Naomba Wizara ikiangalie chanzo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana Bwawa la Milala limekuwa ni mazilio ya viboko limeanza kuwa ni hatari hata kwa wananchi wa Mpanda. Tuna Shule ya *Mpanda Girls* pale, viboko wale usiku na shule haina uzio ni hatari lakini wamekuwa wakitoka pale bwawani wanakuja mpaka Mjini Mpanda kuharibu mashamba ya watu lakini limekuwa pia ni tatizo kwa maana ya usalama wa wananchi wetu. Naomba hilo nalo mliangalie kwa namna ya pekee. (*Makofi*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waziri amekusikia, vyanzo anavyo Mheshimiwa Waziri msaidie maji Mpanda. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Chikambo, Mheshimiwa Gashaza, Mheshimiwa Mkundi na Mheshimiwa Mbogo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kusimama hapa na kuendelea kuchangia kupitia Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza

Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote katika hii Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema yale ambayo nakusudia kusema kupitia Wizara hii, naomba nieleze kwamba mimi ni Mjumbe katika Kamati hii. Nachofahamu mimi ni kwamba tumekuwa tukifanya kazi kupitia Kamati mbalimbali, naamini tunakuwa na Mwenyekiti wa Kamati ambaye anamwakilisha Mheshimiwa Spika lakini kunakuwa na Wajumbe kwenye Kamati zile mbalimbali ambapo tunakuwa tunawawakilisha Waheshimiwa Wabunge wenzenetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kupitia maneno ya utangulizi ambayo nimeyasema, naomba nieleze masikitiko yangu. Sisi kupitia Kamati yetu tumekuwa tukijadili mambo mengi mbalimbali na kuweka maazimio tukiwa tunaamini kwamba tunapoleta kwenye kikao hiki cha Bunge basi yanapata baraka, pengine kunatolewa ushauri kwenye maazimio hayo ili Serikali ifanye utekelezaji. Kinachoshangaza tumekuwa tukijadili mambo mengi, tunafanya maazimio lakini utekelezaji unakuwa wa kusuasua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ule ukurasa wa 18 tumetoa maoni mbalimbali ya Kamati. Naomba niseme machache kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Jambo la kwanza ninalolisema ni kuhusiana na suala la kutenga pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Tumelisema sana na tumekuwa tukitolea maazimio na kuleta mbele ya Bunge lakini jambo hili limeonekana ni sugu na halitekelezeki. Pesa hazipelekwi kwa wakati na pengine zinapelekwa kwa asilimia ndogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza suala la maji, sote tunafahamu kwamba maji ndiyo uhai na maji ndiyo kila kitu. Sisi kama Kamati tunaleta mbele ya Bunge lako Tukufu ili Waheshimiwa Wabunge wenzenetu watoe maoni yao na bahati nzuri Bunge limekuwa likipitisha maazimio lakini tatizo ni kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutapeleka pesa za miradi ya maendeleo kwa wakati hatuwezi kuwasaidia wananchi wetu. Haya yote tunayoyafanya itakuwa sawasawa na hakuna kitu chochote kile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, sisi kupitia Kamati yetu tuliazimia na tulileta kwenye Bunge Tukufu, lakini kabla ya Bunge lilipelekwa kwenye Kamati ya Uongozi, nafikiri huo ndiyo utaratibu, kuhusiana na suala la kuongeza shilingi 50 katika Mfuko wa Maji. Wabunge wengi wamesema na mimi naomba niseme kwa masikitiko makubwa sana. Sielewi tatizo linakuwa wapi kwa sababu sisi tunasema kulingana na matatizo tuliyokuwa nayo kwenye maeneo yetu na tulishawishika kusema hivi tukifikiri kwamba inawezekana lakini tukija hapa inakuwa shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waziri atakapokuja leo atuambie kwa sababu jambo hili sisi tulianza kuzungumza kwenye Kamati kwa nguvu sana, Wabunge tulisema sana. Bahati nzuri hili sio Bunge la kwanza kujadili jambo hili, kama sijasahau kuna Mabunge kama matatu tumekuja tunapitisha maazimio lakini wanapokuja kwenye Serikali wanapokwenda kwenye Kamati ya Bajeti majibu yanakuja sivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukuombe kwamba hili jambo sasa wakati umefika wa kutekelezwa. Hiki kiasi ambacho sisi kama Kamati tulipendekeza lakini kupitia Bunge pia wenzetu waliunga mkono na tulifanya maazimio, tatizo ni nini? Tunaomba tutekeleze, tutenge hizi pesa kwa ajili ya kutunisha kwenye ule Mfuko wa Maji ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. Kama sivyo tuombe safari hii tuambiwe na Serikali njia nydingine, kama tunaona shilingi 50 haitoshi basi watuambie mbadala wake ili sisi tupitishe maazimio kwa sababu wetu wana shida ya maji. Kama mnaona hiki sio chanzo stahiki basi tuleteeni chanzo kingine ili sisi tupitishe maazimio wananchi wetu wapate maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaseme haya na nimetanguliza kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati, toka tumeingia kwenye Kamati ile katika mambo ambayo

tunayazungumza ni kuona ni namna gani tunapata maji. Waheshimiwa Wabunge wenzetu sisi tunaomba hili mtuunge mkono kwa sababu tukiwa kwenye Kamati tunafanya kazi kwa niaba yenu ninyi na tunapoleta hapa tunaomba tufanye maazimio ili utekelezaji ufanyike. Sasa Waziri utakapokuja utatuambia tatizo liko wapi na kama siyo shilingi 50 basi tuambie ni nini kitakuwa chanzo ili wananchi wetu wapate maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kuyasema hayo maazimio ya Kamati ambayo tumekuwa tukiyasema na tunayaleta kwenye vikao na bahati nzuri Kamati hii mara nyingi inaleta kwenye Bunge lako mambo ambayo na wenzetu wanayakubali. Niombe tu Waziri aseme hili jambo tunalitekeleza kwa utaratibu gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya maji ni kubwa sana na mimi ni sehemu ya akina mama na nafahamu jinsi gani akina mama wenzangu wanapata shida katika suala la maji. Tunayo maeneo mengi katika nchi yetu yana tatizo la maji, maji ni ya shida sana. Sisi tulipo humu ndani bila maji hata hizi suti zisingekuwepo, tusingependenza; hata mitandio tunayoivaa isingeng'aa bila maji lakini hata kuoga nako kunahitaji maji, kama hakuna maji ni mtihani mkubwa sana, hili ni jambo kubwa sana. Tuombe Waziri atakapokuja aseme neno kupitia Serikali...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri sana Mheshimiwa Chikambo. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Gashaza, Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Mbogo na tutamalizia na Mheshimiwa Heche.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Maji. Niungane na Wajumbe

waliotangulia kuwapongeza viongozi wetu; Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu - Profesa Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu - Eng. Kalobel, Wakurugenzi wa Wizara kwa maana ya Mkurugenzi Mkuu ma Mkurugenzi Msaidizi, Eng. Christian na watendaji ambao wako chini yao kwa kazi kubwa wanayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niipongeze Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Maji Vijiji, Mijini na Usafi wa Mazingira (*RUWASA*). Tunaamini kwamba hii itakuwa ni suluhisho pia katika kuharakisha kupeleka huduma ya maji vijiji kama ambavyo tumeona mafanikio tulipoanzisha *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuanzisha ni kitu kimoja na ufanisi ni kitu kingine. Tumeona kuna upungufu wa watumishi; ili *RUWASA* waweze kufanya kazi vizuri lazima kuongeza watumishi lakini watumishi wenye sifa na ambao ni makini. Ili *RUWASA* waweze kufanya kazi yao vizuri na Mfuko wa Maji Taifa ni lazima kuongeza fedha ili waweze kutekeleza miradi ya maji kwa ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jinsi ambavyo Mfuko wa Maji wa Taifa jinsi ambavyo wameweza kufanya vizuri, asilimia 67 ya miradi iliyotekelizwa imetokana na fungu ambalo liko kwenye Mfuko huu. Kwa hiyo, kwa kutenga fedha za kutosha kwenye kwenye Mfuko hii, itapelekea kutekeeza miradi mingi ambayo imekwama. Niungane na Wajumbe wallotangulia kusema kwamba shilingi 50 iongezwe; inatoka kwenye mafuta, mitandao ya simu, inatoka wapi, jambo la msingi ni tuongeze fedha katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashukuru. Tumepokea shilingi milioni 208 kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kulipa wakandarasi wanaotekeliza miradi ya vijiji 10, Mungu awabariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Jimbo langu naweza nikagawa makundi ya miradi katika sehemu tatu, kama sio nne; miradi ya vijiji 10 ambayo imechukua sasa zaidi

ya miaka mitano haijakamilika. Tumeomba shilingi milioni 400 *certificate* kwa ajili ya kulipa wakandarasi waendelee kumalizia miradi hii. Niombe Wizara hizi fedha zilipwe haraka iwezekanavyo ili waendelee kukamilisha miradi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wa miji sita katika Mkoa wa Kagera. Ni mradi ambao ulianza kusanifiwa na Mhandisi Mashauri tangu miaka ya 2014. Huyo Mhandisi Mashauri akashindwa kuendelea na kazi akawa *terminated*. Nawashukuru kwamba sasa amepatikana Mhandisi Mashauri mwingine amesharipoti *site* tangu juzi. Kwa hiyo, niombe azingatie mkataba wa miezi nane ambao amepewa ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa sababu *uta-cover* eneo la Mji wa Ngara Mjini lakini pia na vijiji saba ambavyo vimeongezwa; Vijiji vya Mrukurazo, Nyakiziba, Nterungwe, Buhororo, Kumtana, Kabalenzi na kadhalika. Kwa hiyo, niombe kwamba usanifu wa mradi huu uweze kufanya kwa haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mradi wa vijiji vitano. Nishukuru Wizara kwamba tayari mmetoa *go-ahead, no objection* kwamba waanze kutangaza. Vijiji vya Mkalinzi; Mrugina, Kata ya Mabawe; Kanyinya, Kata ya Mbuba; Kumbuga, Kata ya Nyamagoma; na Ntanga. Naomba tunapoanza kutekeleza bajeti Julai basi taratibu zote ziwe zimekamilika ili vijiji hivyo ambavyo vina adha ya maji viweze kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe kwenye fungu hilo kwa sababu tuna chanzo cha Mto Ruvubu na kutumia Mlima Shunga ambao ndiyo mrefu kuliko milima yote Mkoa wa Kagera, vipo vijiji katika kata hilo ambapo ndipo maji na mlima uliopo. Vijiji vya Kenda, Kagali na Mlengo visiachwe katika mpango huu, viongezwe ili wananchi ambao wapo katika eneo hilo wasiachwe nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwenye Mto huohuo wa Ruvubu na mlima huohuo ambao mradi huu ulikuwa ndiyo suluhisho kwa ajili ya vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara. Kwa sababu Mhandisi Mashauri atakuwa yuko *site* kwa ajili ya kuanza kusanifu mradi

huu na chanzo ni hichohicho na mlima huohuo ambao utaweza kusambaza maji kwa mserereko wilaya nzima na hata nje ya wilaya. Ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais wakati namwomba mwaka juzi, 2017, alivutiwa kwa sababu alikuwa anaona ni mradi mkubwa unaweza ukatoa huduma kwa Wilaya ya Biharamulo, Wilaya ya Kakonko, tena wakati ule nilisema unaweza ukaenda mpaka Bukombe na Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mradi huu muuchukulie kama mradi mkubwa ambao unaweza ukatoa suluhisho kwa maeneo mengi ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji. Kwa hiyo, niombe katika bajeti hii, huu mradi wa Mheshimiwa Rais ambao tulimuomba uende sambamba na huu mradi wa miji sita kwa sababu chanzo ni hichohicho na sehemu ya ku-supply ni hiyo hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka kwenye mlima huu upo mlima mwengine mkubwa ambao kimo chake kutoka usawa wa bahari ni kama mita 1,400 hivi, huu wa Shunga ni 1,820, kwa hiyo huu Mlima wa Msumba ambao upo katika Kata ya Nyakisasa, Tarafa ya Rulenge, unaweza ukasambaza maji kwa mtiririko baada ya kupokea maji kutoka kwenye mlima huu kwa vijiji vyote vya Tarafa ya Rulenge na Tarafa ya Mrusagamba lakini ukapeleka hata Wilaya jirani ya Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe mradi huu Wizara muuangalie kama ni mradi mkubwa unaoweza ukatatau changamoto ya maji katika Wilaya ya jirani pia. Mhandisi Mshauri kama anao uwezo basi ni afadhali hii anayoifanya sasa hivi ya usanifu wa mradi wa miji sita aweze kuongezewa *phase two* kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa mradi huo mkubwa wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ambao unaweza ukawa ni suluhisho kwa maeneo hayo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeona jitihada za Wizara kwenye Wilaya ya Temeke, hususan maeneo ya Kurasini, pale ambapo tayari mmeshalipa nafikiri zaidi ya shilingi milioni 600 kama fidia kwa ajili ya kutengeneza

sewage system. Naomba tu-adopt sasa *technology* mpya ya *recycling*. Kwa sababu bado ku-discharge maji machafu kupeleka ziwani au kwenye mito ni kuendelea kuchafua mazingira lakini tunaweza tukaendelea kufanya *recycling* ukawa ni mkakati mahsus i kwenye majiji, miji na halmashauri za miji kwa sababu hata haya maji safi na salama yanatokana na maji machafu tu isipokuwa tunayafanyia *treatment* yanakuwa safi na salama. Kwa hiyo, tukiandaa *sewage systems*, mahali pa kupokea yale maji machafu halafu tuka-recycle tutajikuta kwamba tunaendelea kutunza mazingira lakini pia na kutunza maji. Hata kama itakuwa ni miaka mingapi ijayo tutakuwa na uhakika kwamba hatupungukiwi maji kwenye vyanzo vyetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niendelee kuwapongeza Wizara na niombi tuzingatie haya ambayo Kamati imeshauri kwa sababu Kamati ya Bunge ndiyo Bunge. Kwa hiyo, haya ambayo wameshauri, kama hii ya kuongeza fedha ili kuondoa changamoto hii ya fedha kwenye Mfuko huu wa Maji tuizingatie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishauri kwamba Wizara hii ya Maji lazima ifanye kazi sambamba na Wizara zingine; Ofisi ya Makumu wa Rais (Mazingira) na Wizara ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba tunatunza vyanzo vya maji. Tunapotunza vyanzo vya maji maana yake ni kwamba tunaendelea kuwa na uhakika wa maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha Sheria ya Watumiaji wa Maji, yapo maeneo ambayo lazima tuwe makini tunapoanza kutekeleza sheria hii hasa kwenye vyanzo kwamba watu wawe mbali na vyanzo vile vya maji. Hata kama kuna mahali ambapo *pipes* za maji zimepita, kuna umbali ambao hakuna shughuli za kibinadamu zinazotakiwa zifanyike katika maeneo hayo. Ni vizuri wakati tunaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo lakini wananchi waelimishwe zaidi ili waweze kujua sheria hizi na waweze kuzingatia ili wawe ndiyo watunzaji wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Mbogo na Mheshimiwa Heche.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza niunge mkono hoja ilio Mezani kwetu tunayoijadili lakini nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii. Kimsingi mnafanya kazi kubwa sana ingawa hamjafikia asilimia 100 kulingana na matarajio yetu, lakini niwapongeze mnafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii vilevile kumpongeza sana Eng. Sanga, amekuwa msaada mkubwa sana kwa watu wa Kanda yetu na hasa kwenye eneo letu la Visiwa vyaa Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa katika maeneo kama matatu kama muda utaniruhusu. La kwanza, nianze na eneo la Ukerewe. Ukerewe tuna miradi takribani mitano, inakwenda vizuri tunashukuru sana lakini nimepitia hotuba, ukurasa wa 64 unaongelea mradi wa vijiji 301 vitakavyofaidika na mradi ule wa maji kutoka Ziwa Victoria. Ni mradi mzuri, kwenye Jimbo la Ukerewe kama utakamilika utatusaidia vijiji takribani 33 na kwa ujumla wake utakuwa umesaidia tatizo la maji mpaka kufikia zaidi ya asilimia 80. Rai yangu tu ni kuomba utekelezwe mapema ili uweze kutusaidia hasa kwenye eneo la Visiwa vyaa Ukerewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, Ukerewe pale tuna mradi mkubwa sana wa maji, ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwaka jana; Mradi wa Maji wa Nansio. Ni mradi mkubwa sana lakini kwa mazingira yalivyo mpaka sasa

kimsingi uko *under-utilized*. Una wateja kama 2,900 pekee na una uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni kwamba Mamlaka ya Maji Nansio haina uwezo wa ku-*extend* ile *distribution network* matokeo yake Serikali sasa kupitia Wizara mmekuwa mna-*support* Mamlaka ile ili iweze kujiendesha. Ushauri wangu ili kuondokana na kila wakati kuisaidia Mamlaka kujiendesha mnge-*inject* fedha kwenye mradi huu ili Mamlaka ya Maji Nansio pale iweze ku-*extend* hii *network* ya usambazaji wa maji kwa vile ikiwa na wateja wengi inaweza ikajiendesha kwa kukusanya makusanyo makubwa badala ya kuwa mnai-*support* kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Wizara ifanye jambo hili, kwa sababu sioni kama ni tija sana kila wakati kuendelea kuiwezesha Mamlaka hii iweze kujiendesha kuliko kama mnge-*inject* tu kiasi fulani cha fedha ili mamlaka hii ikaweza ku-*extend* usambazaji wa maji; mtakuwa mmetusaidia sana. Pamoja na changamoto nyingine ndogo lakini mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna watu wana eneo wanahitaji maji pale Ukerewe. Mheshimiwa Waziri ulipokuja Ukerewe nilishauri jambo hili. Inawezekana uwezo wa ku-*apply* kupata maji ni mdogo; mngeandaa programu fulani ili ikiwezekana wananchi hawa wakafungiwa maji na baada ya kufungiwa maji, hata kama ni kwa madeni ili kwamba maji watakapoanza kulipa zile *bills* za maji watakatwa pamoja na kile kiwango cha pesa ambacho Wizara ime-*subsidize* wakati wa kuwaunganishia maji. Inawezekana miradi hii ikawa na wateja wengi na hatimaye mamlaka hizi ziweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hili nilitaka kushauri. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, miradi mingi ya maji inasuasua sana, kuna matatizo mengi makubwa. Hata hivyo kwa mtazamo wangu tuna tatizo kubwa sana la wataalam wa maji kwenye halmashauri zetu na maeneo yetu. ukichunguza matokeo makubwa

yanaanza hata kwenye usanifu wa miradi, matokeo yake tunakuwa na miradi ambayo inakuwa haina tija. Kwa hiyo tuhakikishe kwamba tunaajiri watu wa kutosha, hususan wenyе kada hii ya maji ili angalau miradi yetu iweze kukamilika na iwe na tija kuweza kutoa manufaa tunayoyatarajia kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani nilikuwa kwenye kamati ya *LAAC* tulitembelea miradi mingi sana. kwenye maeneo ya vijiji ni miradi hii ikishakamilika uankuta wananchi hawana uwezo wa kuiendesha miradi hii kwa sababu gharama za uzalishaji zinakuwa kubwa kwa sababu chanzo cha maji ama kinatumia mafuta au kinatumia umeme. Tunaweza tukaepuka hili kama tutaondoa kodi kwenye mashine zile zinazoingia kwa ajili ya kuzalisha maji. Vile vile kama tutatumia *solar systems* kwenye uzalishaji wa maji inawezekana *production cost* itakuwa ndogo na kwa maana hiyo wananchi wa kawaida hawa wanaweza wakamudu gharama hizi za kuendesha miradi hii ya maji na ikaweza kufanya kazi vizuri wananchi wakafaidika na miradi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kama mapendekezo yalivyoletwa na Kamati husika, sina shaka, ninaomba tuungane na mapendekezo ya Kamati hii kama ambavyo tumekuwa tukijadili kwa miaka mitatu. Kwa sababu matatizo mengi makubwa tuliyo nayo kwenye maji ni kwa sababu hatuna pesa za kutosha. Kama tukiongeza pesa kwenye mfuko wa maji inawezekana tukaondokana na tatizo hili kwa sehemu kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kunakuwa na kigugumizi, kwamba ama kutoa kwenye mafuta au namna gani, lakini kama Serikali ridhieni pendekezo hili, kwa namna yoyote itakayoonekana kwamba inawezekana, ama kutoa kwenye mawasiliano. *For instance* tukichukua labda kwa *gigabyte* moja tukitoa shilingi mia moja ninaamini tunaweza kuwa na makusanyo makubwa sana ambayo yanaweza kutunisha mfuko huu wa maji kuliko hiki cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tukiangali kwa bajeti ya mwaka huu inatolewa asilimia 51 ambayo ni ndogo sana kuweza kukabiliana na tatizo la maji tulilo nalo kwenye nchi hii. kwa hiyo ninaungana kabisa na mapendekezo ya Kamati, kwamba ni muhimu tukaboresha mfuko wa maji ili hatimaye usambazaji wa maji hususan kwa wananchi wa vijijini ukawa kwenye kiwango kikubwa ili tuweze kutimiza azma ya kumtua mama ndoo kichwani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Unga mkono hoja.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitangulia mkono hoja; kwa mara nyine ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. (*Makofî*)

MWNEYEKITU: Mheshimiwa Mbogo, tutamalizia na Heche.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hii nafasi. Kwanza naomba nianze kwa kuunga mkono hoja, pili naomba niipongeze sana Serikali kwa kuitendea haki Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na nchi kwa ujumla.

Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Profesa Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Kalobelio na watendaji wote ndani ya hii Wizara ya Maji kwa namna ambavyo wanatekeleza majukumu ya Serikali, na sisi Waheshimiwa Wabunge wanatupokea Wizarani, wanatusikiliza na kutekeleza yale ambayo tumeyaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba niipongeze Serikali kwa kuweka Mji wa Mpanda katika fedha za mkopo wa kutoka nchi ya India, takriban zaidi ya milioni 500, yaani kwenye fedha za dola. Ninatumaini maji yakifika katika Mji wa Mpanda yatafika pia na Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kuhusiana na changamoto ambayo Mheshimiwa Waziri alizieleza katika hotuba yake ya bajeti. Changamoto ya kwanza ambayo alilieleza ni kuhusiana na utekelezaji wa miradi ambao haujafanyika kutokana na changamoto ya kifedha, kutopata kwa wakati au kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali isikilize kwa makini na ilichukue jambo hili. Haiingii akilini, sisi Waheshimiwa Wabunge tunawakilisha vijiji takribani vijiji elfu kumi na mbili mia nane na kitu, ndio tunawakilisha hivyo vijiji; na ndio ambao tunajua changamoto zilizoko katika maeneo yetu ya jimbo na vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kule wanapenda sana na watafurahi sana kama watapata maji, katika mikutano yetu hakuna mkutano ambako utakwenda usipewe kero ya maji; akina mma hadi wanalia, na inatia uchungu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya 2020 kwa vijijini ni kwamba tufike asilimia 85, ni jambo ambalo tumbakisha miezi tisa ya utekelezaji, hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wote na Kamati kwa ujumla; kwamba kuongeza fedha ambayo itakuwa *ring fenced* iinglie kwenye Mfuko wa Maji ili kutunisha na tuwe na fedha ya uhakika ya kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo ya maji; aidha kwenye mafuta au kwenye mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano uchukue asilimia kati ya 2 mpaka 5 anapo-recharge kwenye aidha *MB* za *internet* au kwenye muda wa maongezi tutapata fedha za kutosha, kilio kina wenyewe, hatuwezi kutegemea zaidi mikopo na misaada kutoka nje ya nchi, lazima tujikamue sisi wenyewe. kuna watu wanasema hapa kuongeza tozo hizi unaongeza mziko kwa wanachi. Hivi nyumba yako ikuja jirani atakutengeneza? Lazima tufanye sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba Serikali, Juni 2016 tulihitimisha bajeti, lilitalamikiwa sana, Juni, 2017 lilisemwa sana, Juni 2018 limesemwa sana. Hebu ifike mahali tulikubali, jinsi gani wananchi wetu wanavyoteseke, wanatoka saa tisa, saa kumi kuchota maji ya kwenye madimbwi; wanakoswakoswa kuliwa na fisi na simba; sisi ndio tunajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ilichukue, kama kuonesha *u-serious* wa jambo hili, wananchi wanavyoumia na sisi ndio tunaowawakilisha, ndio tunawasikiliza, kama kuna namna ya kuonesha kwamba liko *serious* kweli; kama ukipensa kutembea uchi humu ndani niko tayari kutembea uchi kuonesha kwamba liko *serious*; *I am ready.* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Abraham aliambiwa atoe sadaka akamtoa mwanaye isaka baadaye akaambibiwa chinja kondoo huyu hapa. Kama kuna namna yoyote ya kutoa sadaka ili kuonesha kwamba jambo hili lina umuhimu sana mtuambie tufanye; lakini tunaomba Serikali, tozo hii ni ya umuhimu kuliko jambo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji tunachukua asilimia 65 ya wananchi walioko vijiji, watu takriban milioni 25, Mheshimiwa Waziri umeandika kwenye hotuba yako, lakini ndio watu wanaoongoza kwa kuteseka kupata maji safi na salama. Mfano mzuri Halmashauri ya Nsimbo, *as I speak now 41 percent* ndio wanaopata maji safi na salama, *41 percent*. Bilioni 351 asilimia 51 tunaisoma kwa sababu tulii kopa kwa wakandarasi kufanya *certificates* zikawa Wizarani, ndizo zimelipwa, hiki ndicho kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kwamba tumepeleka pesa, utaratibu kwa ajili ya kudhibiti (*control*) na ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma alichangia kwamba tukiongeza fedha ndiyo upigaji unaongezeka, *no!* Serikali imebadilisha utaratibu, una-*design* mradi unaleta wizarani wana-*approve* unarudisha, unatangaza ndio unapata mkandarasi anafanya. Sasa hivi mmesema kwamba akifanya kazi *work*

execution ya 30 percent ndiyo u-raise certificate, fedha inapigwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya RASlazima ikakague ndiyo *certificate* ije wizarani na wizarani wanarudi maeneo mengine wanaenda wanakagua ndiyo wana-*release* fedha kwenda kwenye halmashauri. Sasa upigaji, sawa upigaji unaweza ukawepo hao ni binadamu lakini *not to that extent* kama ilivyokuwa kule nyuma. Niombe sana maji ni uhai na maji ni siasa, *let us do everything* lakini kwenye maji *please the government accept this fifty or other charges.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usanifu wa miradi; tu-*improve* kwenye usanifu wa miradi. kuna mahali mtu ana-*design* mradi tumeshakutana kwenye Kamati ya LAAC, mradi umeenda kwenye mlima halafu tena tuna-*raise up* maji yakishindwa kwenda ni hoja. Mkandarasi anajenga *according to the line* na wengine wanapendekeza *force account* kwenye miradi ya maji, naomba niseme *not everything* unaweza kufanya kwa *force account*. Tumefanya kwa vituo vya afya lakini *technicalities* nyingine kwenye maji huwezi ukatumia *force account*; mambo ya *reversion, pressure* na nini, utaokota tu mtu barabarani aje ajenge kama kwenye nyumba, haiwezekani, hatuwezi kufanya kitu kwa *force account.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuna ahadi ya Serikali kwenye Jimbo la Nsimbo, alivyokuja Waziri Mkuu katika Mkoa wa Katavi, Serikali iliahidi kutoa maji Kolongo kuleta Katumba lakini pia maji Kolongo yapo Nsimbo yanalisha manispaa hatunywi hata tone. Kata ya Mtapenda iliahidiwa maji, naambiwa kwenye kanadarasi iliyopo sasa hivi haipo, kwa nini. wananchi wamesema hawataruhusu maji kupita Mtapenda kwenda llembو.

Kwa hiyo, naomba wizara muhakikishe Kata ya Mtapenda inakuwepo na tenki la zamani lipo na ni kilometra nne tu na ndiyo njia hiyo hiyo. maji hayatapita Mtapenda ya Ikolongo kwenda sehemu yoyote lazima Mtapenda wanywe maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wataalam; hii ni changamoto na Waziri amesema lakini tuombe muendelee kuwajengea uwezo na tukisema mtaalam huyu ana-*dilly-dully* na nishukuru tu tumeanzisha *RUWASA*, tumeondoa ukiritimba kidogo kwenye manunuzi. Nimewahi kuingilia manunuzi kwenye halmashauri yangu, Mkurugenzi akawa na wasiwasi na nini na nini, tukasema *what's for?* Tumevunja mkataba wa kwanza na huu, watu wanatumia hela zao *certificate* mpaka wizarani ndio watu walipwe, tuwe na mkandarasi ambaye yupo *committed* kwa hiyo ndio kidogo ikaenda. Kwa hiyo, ukiritimba huu naipongeza sasa Serikali kuanzisha *RUWASA* kwa hiyo, tunatumainia sasa kasi tunayoisifu kwenye *TARURA*, sasa ndio itaenda kwenye *RUWASA*, natumainia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RUWASA* ili iweze kufanya kazi kama tunavyosifu *TANROAD* na *TARURA*, lazima wawe na *cash flow* ya kutosha kwa hiyo naomba mruhusu sana hii tozo ya 50 kwenye mafuta au twende kwenye mawasiliano. Hilo ndilo ambalo tutaliunga mkono na tutakubaliana wote kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukubwa wa bajeti sio tija, tija ni utoaji wa...

MWENYEKITI: Malizia!

MHE. RICHARD P. MBOGO: tija ni utoaji wa fedha. Bajeti ya wizara hata ikiwa bilioni 450 lakini 100 percent zinapatikana, tunatekeleza miradi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe mamlaka zote ambazo zinakusanya fedha vizuri, ziondoke kwenye huu mgao, mgao tupewe halmashauri za vijijini ambazo hatuna mamlaka na hatukusanyi fedha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, asante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche dakika tano.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa dakika tano na mimi niseme kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Prof. Mbarawa ulikuwa na Mheshimiwa Raís pale Nyamongo na nafikiri ndiyo agizo kubwa nchi hii ukipewa na Rais sidhani kama kuna agizo jingine unategemea kusikiliza. Rais alisema maji kwa sababu watu wa Nyamongo madini yanatoka pale yanachangia pesa nydingi kwenye pato la Taifa, ni aibu watu wale kuendelea kunywa maji ya sumu au ya visima vyaa kuchimba kwa majembe na Mto Mara na Ziwa Victoria lipo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili maji kwenye Mkoa wa Mara, Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Kagera ambako kuna ziwa linatoa maji yanaenda huko mbali na watu wanapata maji, ni mambo ambayo hayaeleweki kweli kweli kwa wananchi. Kwa hiyo, mimi nafikiri Profesa tuna watu 42,000 pale Nyamongo wanahitaji maji. Mji ule kutokuwa na maji, mji mdogo kama ule mkubwa vile ulivyokuwa na una watu, *population* yake 42,000 ni sawasawa na Majimbo mengi tu ya watu ambaeo wapo humu, hauna maji mpaka leo sielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; wote tumekubaliana tatizo la maji ni kubwa kwenye nchi hii lakini tunatofautiana kwenye sehemu ndogo tu kwamba tatizo ambalo linatukumba ni *priorities*. Tunapangaje vipaumbele vyetu na sisi Wabunge tunasimamiae Serikali kwenye kutekeleza hivyo vipaumbele. Sasa leo kila Mbunge anasimama humu na ni kwa mara ya kwanza naona Wabunge wanashabikia kwenda kuwawekea wananchi maskini mzigo eti tozo za shilingi 50, inanishangaza sana. sielewi kwamba leo *solution* kwa sababu hatuna walimu, hatuna barabara, madawati, choo hatuna kwenye shule sijui nini tuweke tozo shilingi 50, hayo mafuta si yatafika 4,000 na nani atasafiri kwenye hayo magari kama mafuta yakifika shilingi 4,000. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema Serikali lazima ije na mpango kwanza zile pesa tulizotenga zenyewe kwenye bajeti kwa nini hazijaenda, kwa nini hazikwenda? Je, na tozo hizo mnazozungumza tumeweka kwenye *REA* zimekwenda shilingi ngapi kwenye hiyo tozo ya *REA*? Kwa sababu pia usimamiaji wa bajeti, je tunasimamia na tunatekeleza bajeti kama tulivyozipanga hapa au sisi Wabunge tumekuja tunapiga kelele humu baadaye wanaenda wanakaa kikundi cha watu 4/5 wanatengua kila kitu ambacho Wabunge walipitisha hapa halafu mnataka tuje hapa tupige makofi eti shilingi 5; mimi hata senti moja kuongeza kwenye mafuta napringa na napringa kwa sababu inakwenda kuongezea wananchi maskini mzigo... (*Makofii*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa!

MWENYEKITI: Heche taarifa

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumwambia rafiki yangu Heche kwanza namuunga mkono kwa suala la kusema tusichaji wananchi shilingi 50 lakini ya pili nilikuwa namshauri kwenye akaunti ya Wilaya yake ya Tarime kutohana na madini kuna bilioni 5 afunge macho atoe bilioni 2 hebu asambaze maji wakati yanangojea Mhesimiwa Prof. Mbarawa ampelekee maji, asante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru huyu mganga wa meno anajifunza bado Bunge linavyofanya kazi, kwa hiyo, sina haja ya kumjibu. Hapa tunazungumza mambo ya wananchi kwamba watu wana matatizo ya maji na tutoe *solution* kwamba Wabunge tusikwepe majukumu ya kuisimamia Serikali itoe pesa, kwa

sababu wananchi hawapo humu ndiyo wanyonge wenu mnataka leo muwapelekee mzigo; kila mtu anayesimama hapa weka shilingi 50, tukija hapa hiyo shilingi 50 haijaenda nani atasimama humu aseme shilingi 50 haikwenda? Kama mna uwezo huo mbona pesa za *REA* hazijaenda na hampigi kelele hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema Wabunge...

MHE. ABDALLAH S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. JOHN W. HECHE: watimize wajibu wao wa ku...

MWENYEKITI: Taarifa, Heche kuna taarifa nyingine.

TAARIFA

MHE. ABDALLAH S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge mzungumzaji wa sasa namuheshimu sana mtu makini ya kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi leo hii tarehe 3 tunavyozungumza Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Maji amesaini mkataba na Ujerumanil bilioni 330, kwa mara ya kwanza bajeti ya maji ya maendeleo inaenda kutimia kwa asilimia 100. Kwa hiyo, nampa taarifa Mheshimiwa Heche. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hao wenzetu bado wanataka kuaminika, kwa hiyo endeleeni mtaaminika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema, hoja ya maji wote tunaunga mkono lakini hoja yangu ni kwamba Wabunge wajibu wetu ni kuisimamia Serikali, amezungumza vizuri sana hapa mama Mheshimiwa Conchesta, amesema haya mambo ya kuja hapa tuna-*beg* naomba tumekuwa Matonya humu na vikombe, naomba

piga magoti, hapana lazima Serikali ijue Wabunge wanapozungumza hapa wanawawakilisha walipa kodi wa nchi hii ambao wamejikamua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunasema hapa tuongeze shilingi 50 kwenye mafuta ya taa kweli? Hivi ninyi mnajua vijiji ni wananchi wanaishi kijiji ambaye kutoa shilingi 2,000 ni tatizo kweli kweli na kama mna uchungu kiasi hicho, nani ame-*volunteer* mshahara wake humu, mnalipwa mamilioni; anzeni nyie kwamba tukatwe milioni moja moja kila mwezi iende kwenye maji kama kweli mna uchungu kiasi hicho... (*Makof*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Acha ujisadi kwanza wa madini wewe...

MHE. JOHN W. HECHE: Hatuwezi kukubali tuje kubana wananchi wanyonge eti ndiyo wanyonge wetu kwa sababu hawapo humu, tunakwepa majukumu shilingi 50. Na hiyo itakuwa siasa ambayo tutaizungumza kwa wananchi, muelewe kabisa, shukrani. (*Makof*)

MWENYEKITI: Asante, waheshimiwa Wabunge kuna tangazo. Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Esther Matiko anaomba kuwatangazia kuwa kesho kutakuwa na mechi kati *Bunge Queens* na CHANETA ambayo ilitambulishwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri saa 9 Alasiri, mnaombwa wote kuwepo kushangilia timu zote mbili kwa manufaa ya michezo nchini.

Nahairisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 6 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)